Kikao cha Saba – Tarehe 21 Oktoba, 2013

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Mwenyekiti, (Mhe. Mgeni Hassan Juma) Alisoma Dua.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya uwasilishaji wa taarifa ya serikali juu ya hoja zilizotolewa katika ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Utendaji wa Baraza la Manispaa la Zanzibar. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 35

Kuvuja Jengo la Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: (Kny: Mhe. Salma Mohamed Ali) - Aliuliza:-

Jengo la Baraza la Wawakilishi ni jengo jipya hivi sasa limekuwa na nyufa sehemu kadhaa (juu na chini) ya jengo hilo kiasi ambacho linatia huzuni sana.

Je, kuna maelezo gani kuhusu athari hii ya kutisha hasa kutokana na gharama kubwa iliyotumika katika ujenzi wa jengo hilo pamoja na kuwa ni muda mchache mno athari hiyo imejitokeza?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 35 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mjumbe juu ya kutokea kwa nyufa sehemu kadhaa katika jengo hili la Baraza la Wawakilishi. Napenda Wajumbe wa Baraza lako tukufu waelewe kwamba kuna nyufa ambazo zimejitokeza katika maeneo ambayo yameachwa nafasi wakati wa ujenzi wa jengo hili, kujengwa kwake limegawika katika sehemu tatu ambapo sehemu moja kwenda nyengine, kuna nafasi ijapokuwa wakati wa kuwekwa plasta sehemu hizo zilifunikwa.

Kwa maana hiyo, nyufa hizo kubwa zinajitokeza, ni kwa sababu hiyo na sio kwa sababu ya ubovu ule ambao tunadhani unaweza kuleta athari kubwa baadae. Mhe. Mwenyekiti, pia kweli zipo nyufa ndogo ndogo ambazo zimejitokeza katika jengo hili. Lakini tayari hatua zinaendelea kuchukuliwa kwa lengo la kusawazisha mapungufu hayo katika jengo letu. Aidha, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi tayari imeshaajiri mtaalamu wa majengo ili asaidie kuyafanyia utambuzi wa kitaalamu, kwa ajili ya kuyapatia ufumbuzi matatizo ya jumla yanayojitokeza katika jengo hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha 2013/2014 Ofisi ya Baraza la Wawakilishi imetenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya Jengo la Baraza la Wawakilishi. Hata hivyo, bado tunatarajia kuanzisha mradi maalum wa kulifanyia matengenezo makubwa jengo hili pamoja na vifaa vyengine vikiwemo vyoo katika mwaka ujao wa fedha, ili kuhakikisha kuwa jengo letu linakidhi viwango vya hadhi yake.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana aliyotoa mdogo wangu hapa Mhe.

Mohamed Aboud, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hili jengo ni miongoni mwa majengo ambayo yanatakiwa yawe madhubuti sana, kwa sababu ni moja kati ya mihimili mitatu ya nchi. Ukiachilia Ikulu, Mahakama Kuu na hili jengo la Bunge, ni miongoni mwa majengo makubwa matatu na mahiri na yanatakiwa yawe makini sana.

a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ukiachilia mbali na nyufa ambazo zimejitokeza sana, hata tatizo la *echo* serikali hadi leo hii imeshindwa kutatua. Je, hizi nyufa kushindwa kuziba ni ukosefu wa kwamba serikali haina uwezo kama ilivyokosa uwezo wa kuondosha *echo* katika jengo hili?

b) Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu jengo hili limetumia fedha nyingi sana na ni jipya na amesema watakuja wataalamu kuja kufanya utambuzi wa tatizo hili. Je, ni lini wataalamu hao watakuja, kwa sababu jengo tunaendelea kulitumia na kuna mabadiliko ya tabia nchi na sisi tupo karibu na bahari?

c) Mwenyezi Mungu tunusuru ikija ikitokezea rushka moja hapa itakuja kuwa ni tatizo. Je, ni lini wataalamu hao watakuja ili kufanya utambuzi yakinifu katika tatizo la kihandisi lililojitokeza katika jengo hili?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema kwamba jengo hili ni moja katika kielelezo cha nchi yetu na ni jengo muhimu sana na ndio maana serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, likahakikisha kujenga jengo zuri kama hili.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kumejitokeza matatizo katika ujenzi wa jengo hili, ambalo hayakutarajiwa yatokee lakini sasa ndio yametokea. Kutokana na hali hiyo na sababu zenyewe za ujenzi,

kama nilivyosema awali kwamba jengo hili limejengwa kwenye maeneo matatu na zile sehemu nyengine zimeunganishwa kwa plasta tu, tokea mapema hazikuwa zimeunganishwa pamoja, ndio maana zile nyufa kubwa tunaziona. Lakini sio zile ambazo zinatarajiwa zitaleta athari kubwa katika ujenzi na ndio maana tukasema tumeajiri tayari mtaalamu wa mambo ya majenzi atusaidie kufanya tathmini ya kina, ili matengenezo tutakayoyafanya yawe ya uhakika na ya muda mrefu.
Kutokana na hali hiyo na serikali kuona jambo hili, ndio nakubaliana kabisa na ushauri wa Baraza hili kwamba jengo hili lifanyiwe tathmini ya kina na tuanze mkakati wa mradi maalum wa kulijenga jengo hili ili lirudi katika hadhi yake na kufanya marekebisho yale yote yaliyojitokeza wakati huo wa ujenzi hapo awali. Kwa hivyo, sasa hivi tunachukua hatua ya kulirekebisha jengo hili ili liifikie ile hadhi inayotakiwa.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kufika hapa tukiwa katika hali ya afya njema, kwa mujibu wa kutimiza wajibu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba pamoja na tathmini, lakini ni vyema jengo hili likafanyiwa uchunguzi wa hali ya juu zaidi, kwa sababu miongoni mwa hizo nyufa pia ikinyesha mvua maji yanaingia mpaka ndani.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, nje ukitizama mule mulimotiwa vidude vya kupambia, kuna mashimo yaliyojitokeza itakuwa ni athari ya jengo hili. Je, atakubaliana na mimi kwamba si tathmini ni uchunguzi zaidi?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mjumbe, kwamba kufanya uchunguzi zaidi na ndio nia ya kuanzisha mradi maalum wa kulitengeneza jengo hili, kwa sababu tumeona matatizo madogo madogo yakijitokeza kama nilivyosema awali

yakiwemo ya vyoo, nyufa hizo kubwa, kuvuja kwa jengo pamoja na tatizo la echo na mambo mengine ambayo yanahitaji yatimizwe kwa hadhi ya Baraza hili.

Kwa hivyo, nakubaliana naye Mhe. Asha Bakar Makame ushauri wake wa kulifanyia uchunguzi wa kina jengo hili na ndio lengo hasa la mradi tunaouanzisha kwa nia ya kurekebisha kila mapungufu yaliyojitokeza kwenye jengo letu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri, lakini kabla ya kumuuliza, kwanza naomba nichukuwe nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumjaalia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kurudi Makka salama. Naomba Mwenyezi Mungu na sisi atujaalie mwakani twende Makka kama ndugu walivyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti baada ya shukrani hizo, sasa naomba niulize swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo: Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini kwamba jengo hili ni miongoni mwa majengo ambayo hayana kiwango, ukiangalia chini *tiles* zinazuka kwa sababu ya mchwa, kuta zinapasuka na hata paa linavuja kila siku zinaponyesha mvua.

a) Je, katika tathmini ambayo serikali itafanya, watakuwa tayari kushirikisha wadau kwa maana ya wawakilishi kujua ukweli wa jengo hili ili kuangalia ile dhana nzima ya *value of money?*

b) Gharama ambazo zitathibitika kwamba zimepotea na matengenezo ambayo yatafanywa, ni nani atatoa ni serikali au mjenzi aliyekabidhiwa kazi hii?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kupokea salamu zake za pongezi na shukrani kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa

kumtakia heri ya kurudi Makka, alipokwenda katika ibada ya Hijja, na sisi sote tunamuombea dua hiyo na Inshaallah na sisi wengine mwakani Mwenyezi Mungu atupe hatua tufike pamoja na Mhe. Hija Hassan Hija.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mhe. Hija Hassan Hija kama ifuatavyo: Mhe. Mwenyekiti, nia ni kulifanyia uchunguzi wa kina jengo letu na kugundua kila pale penye kasoro, na kwa vyovyote vile tutakuwa tayari wakati wowote kushirikiana na kila mdau, wakiwemo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili katika kufanya tathmini ya kina, ili kujua kwa undani mapungufu yaliyojitokeza katika jengo hili na kasoro zake zote. Kwa hivyo, kwa vyovyote katika jambo hilo hakuna kificho tunaunga mkono kufanya tathmini na kila atakayekuwa tayari kushirikiana na sisi basi milango yetu iko wazi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu fedha, kwa sasa nia yetu serikali itowe fedha, lakini pia tutaupitia mkataba tuone ni vipi mjenzi na yeye anahitaji kufidia gharama hizi, kwa sababu kwa kiasi kikubwa bado inaonekana haujamaliza ule muda ambao ungehitaji uwe ni *guarantee* kwa mujibu wa majenzi. Matokeo haya yametokea mara tu baada ya kukabidhiwa jengo. Kwa hivyo, ni vizuri katika kuona hili, pia na mjenzi akajua gharama zetu na kwa kupitia mkataba tuone ni namna gani na yeye tunaweza kumshirikisha katika kubeba gharama ambazo zitajitokeza mbele yetu. Ahsante sana.

Nam. 2

Ukarabati wa Maegesho ya Magari ya Chake Chake

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Baraza la Mji wa Chake Chake mara nyingi limekuwa makini katika kukusanya kodi sio tu kwenye maduka na wafanyabiashara wadogo wadogo lakini limekuwa madhubuti

sana katika kukusanya kodi za maegesho ya magari, magari ya Ng'ombe na hata Punda na Boda boda, jambo ambalo limesaidia sana katika kuingiza mapato yake.

Kwakuwa kodi za wananchi zinatakiwa ziwarejee wenyewe kwa kuwapatia huduma mbali mbali jambo ambalo Baraza hilo limekuwa likisua sua kulifanya

(a) Je, ni lini Baraza hilo litafanya ukarabati wa Maegesho ya magari pamoja na barabara ikiwemo ile inayotoka Mahakamani kupitia Hospitali ya Chake Chake kwenda soko la samaki (Qatar) hadi Uwanja wa mpira Tibirinzi?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 2, lenye vipengele (a) na (b), kabla ya kumjibu swali hilo naomba kutoa maelezo yafuatayo:

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Wawi, kwamba Mji wa Chake Chake na Vitongoji vyake ndio kwenye Makao Makuu ya mawizara na taasisi zake kwa upande wa Pemba. Aidha, ndio mji wenye shughuli nyingi za kibiashara. Hivyo, huwavutia wananchi wengi wa Pemba na wageni wanaotembelea Pemba kufika katika mji huo kupata mahitaji yao mbali mbali. Hivyo, husababisha magari yanayoingia na kuzunguka katika mji huo kuongezeka kila siku wakati miundombinu yake haiongezeki kwa uwiano ulio sawa na mahitaji.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa huduma ambazo mabaraza ya miji na manispaa yanapaswa kuzitoa kwa watu wanaoingia au kuishi katika mji husika ni pamoja na kutoa huduma za maegesho kwa vyombo vyao, iwe gari, pikipiki na vyombo vyengine vya usafiri wanavyovitumia kwa usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto kubwa inazozikabili mabaraza yetu na mengine duniani kote, ni ongezeko kubwa la vyombo vya usafiri na hivyo husababisha misongomano ya vyombo hivyo na kukosekana maegesho ya kutosha. Ili kukabiliana na changamoto hizo ni kuongeza ukubwa wa maegesho, lakini kwa vile maeneo ya miji yanakuwa na nafasi chache, basi mamlaka za miji zenye uwezo huwa wanajenga maegesho kwa kwenda juu, nikimaanisha katika maghorofa maalum na wakati mwengine huwatumia wawekezaji, kufanyakazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 2 kama ifuatavyo:

a) Mhe. Mwenyekiti, tayari Baraza la Manispaa limeshatenga eneo la Michakaeni, ambalo limepimwa na pia fidia imeshalipwa kwa wananchi ili litumike kama kituo cha daladala cha Mji wa Chake Chake. Aidha, tayari mtaalamu mshauri wa mradi wa "*Zanzíbar Urban Services Project*" (*ZUSP*) ameshafanya upembuzi wa mradi huo na Baraza linasubiri ripoti yake ili hatua zinazofuata zichukuliwe.

b) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuendelea kwa madereva wa mji huo kuegesha magari kiholela kunahatarisha usalama na usumbufu kwa abiria. Katika kuliona hilo na kuweza kulitafutia ufumbuzi tayari Baraza la Mji la Chake Chake kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya imeunda kikosi kazi cha kuhakikisha kwamba magari ya abiria hayaegeshwi barabarani. Kwa sasa kuna sehemu mbili zimetengwa kwa ajili ya kuegesha magari, ambapo magari ya abiria yanayotoka Kusini Pemba yametengewa eneo la uwanja wa Zimamoto la Chanjaani na kwa magari yanayotoka Kaskazini Pemba yametengewa eneo la karibu na Uwanja wa Gombani.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitumie fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri kwa jibu lake

zuri. Baada ya hapo naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kuwateremsha abiria wanaotoka Kusini. Kwa mfano Bogoa huku kwa Mhe. Haji Faki Shaali na kwa Dk. Shein wakati anakuja Chake Chake ukamteremsha Chanjaani, ni kumfanya atowe nauli mara mbili katika safari moja.

(a) Je, ni utaratibu gani ambao serikali imejiwekea kwa sasa, kabla ya kumalizika hiyo sehemu ya maegesho ya gari ya hapa Mava Mbarouk, ni utaratibu gani kwa serikali uliowekwa wa kuwapa nafuu jamaa kutoka Sikwese, Bogoa, Nanguji badala ya kuwateremsha pale na kuwafanya walipe nauli mara mbili. Ni utaratibu gani mliouweka serikali ili kuona wanapata nafuu ya nauli watu hawa kutoka Kusini?

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kuna gari zinaegeshwa hata hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, uliza swali. Nenda kwenye swali moja kwa moja.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Swali nimeshauliza Mhe. Mwenyekiti, kwamba serikali itatumia utaratibu gani kuwapunguzia gharama za safari wanaotoka Bogoa na Nanguji pamoja na Sikwese ukiwateremsha meli mbili, si itakuwa wanatoa nauli mara mbili katika safari moja? Hilo ni swali la kwanza.

Swali la pili Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wanaendelea kuegesha magari katika maeneo ya sheli pamoja na Afrikana jambo ambalo ni tatizo. Je, serikali ina utaratibu gani wa kuona kwamba pale hapana msongamano tena wa magari na hakuwezi kutokea ajali kama inavyotokea sasa hivi, kwa sababu bado gari zinaendelea kuegeshwa maeneo yale?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, katika jibu langu mama nilisema kwamba serikali kwa sasa hivi imeweka utaratibu wa maegesho ya magari katika eneo la Chanjaani na eneo la karibu ya Gombani. Kuweka eneo la maegesho sio maana ni kituo cha kushusha abiria. Inavyotakiwa gari ikiingia mjini ishushe abiria halafu irudi Gombani au Chanjaani kusubiri zamu ya ruti yake ili irudi kuja kuchukua abiria.

Kwa hivyo, utaratibu umewekwa mzuri sio kwamba wanaotoka Kaskazini wanashushwa Gombani na wanaotoka Kusini wanashushwa Chanjaani, hapana. Utaratibu ni kwamba gari inayotoka Kusini inakuja mpaka mjini inashusha abiria ikishakushusha abiria inatakiwa kurudi Chanjaani ikaegeshe. Inayotoka Kaskazini inakuja mjini ikimaliza kushusha abiria inarudi Chanjaani. Kule kwenye vituo vile vya maegesho kwa utaratibu wao madereva wana watu wao ambao wanaaweka zile tani za gari. Kwa hivyo, gari ambalo zamu yake imefika inaondoka inakuja kuchukua abiria mjini na kuendelea kwenye ruti yake kama kawaida.

Suala la magari ambayo yapo kwenye sheli. Niseme kwamba huo ni ukaidi tu wa madereva, kama kawaida ya baadhi ya madereva kutokufuata sheria na kutokutii amri na maelekezo wanayopewa wanaendelea tu kuvunja. Sasa labda kwa kupitia chombo hiki, niliagize Jeshi la Polisi kupitia askari wa usalama barabarani wawachukulie hatua wale ambao wanaegesha magari katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Mimi nina swali moja dogo sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba sehemu hiyo ambayo unataka kuekesha hayo magari ni sehemu ambayo haifai ina mabonde na ina mmong'onyoko.

(a) Je, kama ni hivyo huoni serikali kupeleka pale ni kuzitumbukiza gari zikaweza kutumbukia kwenye mashimo hayo?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kama nilivyosema hilo ni eneo la dharura, kwa hivyo katika dharura sio kweli kwamba sisi tutakwenda kuegesha magari pale pakiwa hali ile iliyo, ni lazima tutafanyia marekebisho ili kuondosha yale mashimo. Lakini serikali haikufanya hivyo kwa sababu ya kuwapa hasara wenye magari kwa ajili ya kuingia kwenye mashimo. Imeweka utaratibu huo kwa sababu ni utaratibu wa muda huku tukiwa na mpango kabambe wa kujenga kituo cha kudumu, kitakachokuwa hakina mashimo na kitakachokuwa ni cha kisasa kabisa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri. kwa kuwa gari inayotoka Mkoani inakwenda mpaka kituo cha mjini na baadae gari lile likarudi mpaka Chanjaani, halafu gari lile likapigiwa simu na kurudi mjini kuchukua abiria. Huoni Mhe. Waziri huu ni usumbufu wakati hakuwa na abiria wenyewe. Vile vile, na mafuta ni kumalizika mara kwa mara? Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, sioni kama hatua hiyo ni usumbufu kwa sababu utaratibu ni kwamba ni lazima dereva aje ashushe abiria halafu atafute pahala pa kuegesha na kule kuna utaratibu mzuri ambao umewekwa. Sasa juu ya utaratibu wa hasara, haiwezi kuwa hasara kwa sababu nauli imewekwa mwa mujibu wa ruti ambazo dereva anachukua abiria na kuwarejesha. Kwa hivyo, suala la hasara kwangu mimi sioni kama ni hasara, wala serikali haioni kama ni hasara.

Kwa hivyo, kama madereva wenyewe wataona kama ni hasara basi watawasilisha malalamiko yao kwenye chombo kilichowekwa, halafu serikali kwa kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inaweza ikapanga bei nyengine, lakini kwa sasa hivi utaratibu uliopo ni huo wala hakuna hasara, wala hakuna usumbufu.

Nam. 89

Mamlaka ya Kupambana na Rushwa Zanzibar

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Ni muda mrefu umepita tangu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. ali Mohamed Shein, aliposaini Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi.

a) Kwa nini Mamlaka hiyo imekuwa kimnya wakati rushwa inaendelea kuzagaa katika kila sekta ya huduma Zanzibar?

b) Kama Baraza la Wawakilishi limefanikiwa kuibua ubadhirifu mkubwa wa wizi wa mali za umma katika taasisi za serikali likiwemo Shirika la Umeme (ZECO), mamlaka imechukua hatua gani kufanyia kazi ripoti hizo?

c) Matarajio ya wananchi kuona mamlaka inapambana na rushwa kwa vitendo kwa nini imegeuka bubu tofauti na TAKUKURU ya Tanzania Bara?

Mhe. Waziri Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 89 lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2011 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipitisha Sera ya Utawala Bora, sera ambayo ilipendekeza kuwepo kwa sheria ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi. Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, imeanzishwa kwa sheria ya kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi Zanzibar nambari 1 ya mwaka 2012. Sheria hii ilipitishwa wakati wa Mkutano wa Sita wa Baraza la Nane na kutiwa saini na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika mwezi Mei, mwaka 2012.

Mamlaka hii ilianzishwa ramsi tarehe 15 Oktoba, 2012 baada ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kumteuwa Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo. Kabla
ya hapo Zanzibar haikuwa na chombo mahususi cha kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi. Kwa hivyo, makosa ya rushwa yalikuwa yakidhibitiwa kwa utaratibu wa kawaida wa makosa ya jinai.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi yoyote mpya inapoanzishwa, basi ni lazima ipate muda wa kujipanga, ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kuwa mamlaka hii ni mpya na hakukuwa na chombo cha aina hii kabla, ambacho kingeweza kurithi mahitaji muhimu kama vile watumishi, wataalamu, majengo na vifaa vyengine vya kiutendaji. Kwa hivyo, basi inalazimika kuchukua hatua za kujijengea uwezo ikiwa ni pamoja na kuajiri na kutoa mafunzo kwa watendaji wake, ili hatimaye kiweze kuwa ni chombo imara chenye uwezo wa kufanyakazi kwa umakini, uhakika na ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mamlaka imeweza au imekuwa ikifuatilia kwa karibu matukio mbali mbali yenye viashiria vya rushwa na uhujumu wa uchumi yakiwemo yale yaliyoibuliwa na Baraza lako tukufu. Kwa kuanzia mamlaka ichukua hatua ya kukusanya ripoti na kumbukumbu zote hizo kwa madhumuni ya kuzifanyiakazi. Kazi hizo zitaanza kufanyika mara baada ya

kujiridhisha kwamba watumishi wa mamlaka waliohitimu mafunzo hivi karibuni wana uwezo wa kufanya uchunguzi kwa mafanikio, ili hatimaye waweze kushauri kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar haijageuka bubu. Kwa kweli tayari imeanza kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria kwa nyakati tofauti na mamlaka imekuwa ikielimisha umma kwa njia mbali mbali ikiwemo ya kutumia vipeperushi inavyovibandika katika maeneo tofauti kwenye mikusanyiko ya watu au yanayohusika na utoaji wa huduma pamoja na kutumia vyombo vya habari, ambapo muongozo wa utoaji wa elimu ya uraia tayari umeshatayarishwa. Aidha elimu kwa umma pia inatolewa kupitia vyombo vya habari hasa redio.

Kwa upande mwengine, mamlaka imeanza kupokea malalamiko mbali mbali pamoja na ripoti ambazo zimeanza kufanyiwa kazi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Lakini kwanza kabla ya kuuliza swali langu, napenda nilipongeze Baraza hili kwa kutunga sheria ya Kusimamia haya ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi. Aidha nimpongeze Rais kwa kuisaini sheria hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba niulize swali kama ifuatavyo:

(a) Kwa kuwa chombo chenyewe cha kupambana na rushwa kimeanzishwa mapema mwaka 2012 na hivi sasa karibu Novemba, 2013 yaani karibu mwaka mmoja na zaidi, bado hawajajipanga. Je, ni kipindi gani ambacho taasisi ya serikali inayotakiwa kushughulikia mambo nyeti kama rushwa ni kipindi gani inajipanga, ili kufanya kazi yake ipasavyo?

(b) Mhe. Waziri pamoja na kupokea taarifa za uhujumu wa uchumi kama hizi mulizopewa na Baraza la Wawakilishi, kupokea ni upande mmoja na ufuatiliaji ni upande wa pili. Je, ni lini mutaanza kufuatilia hizi taarifa ambazo tayari mumeshazipokea kama alivyokiri yeye mwenyewe ni lini wataanza kuzishughulikia kisheria?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema ni kwamba hii ni taasisi mpya na taasisi yenyewe upya wake mbali ya hayo kwamba ni nyeti sana ina uzito mkubwa sana na ni kitu kipya hapa kwetu. Sasa umakini wa kujipanga ni suala la msingi sana na si kama wakati huo kwamba ilikuwa imekaa kimya tu. Lakini kulikuwa na kazi za ndani kwanza za kuweka au kupanga muundo wa utumishi, pia kuandaa muundo wa mamlaka yenyewe uwe vipi pamoja na muundo wa utumishi kuupata na halafu kuandaa mafunzo maalum kwa hawa vijana.

Vile vile, kama nilivyosema hii ni *special task*, ambayo inahitaji uadilifu, uaminifu pamoja na ukakamavu na vijana hawa imebidi wachukuliwe kutoka wizara mbali mbali. Kwa hiyo, katika kuwachukuwa peke yake inabidi uchague vijana ambao wenye sifa zinazohitajika, baadaye hao walipewa mafunzo katika mbinu za kujihami, kutoa elimu kwa umma pamoja na uwezo wa kushirikiana na taasisi nyengine.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba hicho kimya kilikuwa si kimya cha kukaa bure, isipokuwa kilikuwa kimya cha kazi. Lakini hivi sasa naomba Mhe. mwenyekiti kukuhakikishia kwamba kitengo hichi kiko tayari na sasa tayari kimeshaanza kazi rasmi.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Mwakilishi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine niwajuilishe hilo na sifa moja

kubwa sana ya kitengo hichi ni suala la ushirikiano au kushirikisha (*participation*), basi tunaomba sana Wawakilishi pamoja na watendaji wengine, ili ifanyekazi zake vizuri, basi kitawashirikisha kadri inavyomkinika wao katika utendaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ripoti hizi za Baraza tayari zimetoka siku nyingi lakini kazi bado. Kwanza nafikiri kuhusiana na ripoti serikali imetoa maelezo mazuri tu juzi na wakati wote serikali haikukaa kimya ilikuwa pia inayafanyiakazi haya. Kwa hivyo, kwa upande wetu sasa kwenye kicho kitengo kitafuatilia kwa upande wake, lakini hatimaye mwisho suala la msingi ni jambo la kuchukua hatua za kisheria kwa kuwashirikisha wadau wote hilo ni suala la msingi sana na wala kitengo kumaliza mambo peke yake na lazima kishirikiane na wadau wote katika kufanikisha au kutekeleza sheria.

Mhe. Shadya Mohamed Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza lenye sehemu (a) na (b).

(a) Mhe. Waziri, je kuna mfanyakazi yeyote aliyehusisha na rushwa?

(b) Nini mchango wa wananchi katika vita dhidi ya rushwa?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, samahani hili la pili sikulisikia vizuri naomba kidogo alirejee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Shadya Mohamed Suleiman, rejea swali lako la pili Mhe. Waziri hajalisikia vizuri.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nini mchango wa wananchi katika vita dhidi ya rushwa?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza hivi majuzi tu hao wanafunzi na hivi sasa tayari wameshakuwa wafanyakazi waliohitimu, kwa ujumla walilengwa wawe 30. Lakini kwa bahati mbaya waliohitimu yale mafunzo nimejuilishwa kwamba ni 29. Kwa hivyo, kwa ujumla hivi sasa kitengo kizima kina wafanyakazi wapatao 47 wakiwemo wanawake 21 na wanaume 26.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ushirikishwaji kama nilivyosema suala la msingi ni ushirikishwaji hasa unaokusudiwa hapa ni kushirikiana na taasisi ambao ni wadau katika kufanikisha haya mambo, kwa sababu haya mambo zaidi yanahitaji *intelligence*, yaani upelelezi mkubwa sana, ufuatiliaji, usimamizi, uwajibikaji na usiri katika mambo yake na wala sio mambo ya kutangazwa tangazwa tu.

Kwa kweli ni mambo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi ya uwajibikaji mkubwa sana. Kutokana na hali hiyo, kama nilivyosema kwamba hawatakwenda peke yao, lakini wanamiko yao (*ethics*) zao na hasa hayo ndiyo yalikuwa malengo ya mafunzo waliyoyapata.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mjumbe pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine kwamba wawe tayari kwamba kitengo kimeshaanza kazi na bila ya shaka kitahitaji msaada wenu mkubwa.

Mhe. Wavu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya mwisho ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza kwa Mhe. Waziri.

Kwa kuwa *experience* inaonesha kwamba inapoanzishwa taasisi serikali huchukua muda mkubwa sana kwa taasisi hiyo kuanza kazi zake kwa kisingizio cha kujipanga. Je, serikali haioni kwamba hivi sasa ipo haja ya kujipanga kwanza kabla ya

kuanzisha taasisi, ili kuondoa ile dhana ya taasisi hizi kudhaniwa kuwa bubu? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kimsingi niseme nikubaliane naye kwa asilimia 50 Mhe. Mjumbe, lakini hiyo asilimia 50 nyengine nasema hivyo kwa sababu. Kwa kweli unapoanzisha kitu lazima uipitishe ile sheria kwanza na wala huwezi kukianzisha kabla ya kupitisha sheria na hii tulianza na sera, ambayo ilikuja kama nilivyosema na baada ya kupitishwa Sera ya Utawala Bora, ndio ikazaa sheria na baada ya kuja sheria tukaijadili hapa na matokeo yake sheria ndio ikaruhusu sasa undeni hicho chombo na akateuliwa Mkurugenzi Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuteuliwa Mkurugenzi Mkuu, ndio akajipanga sasa yaani anapanga timu yake. Kwa hivyo, haya mengine lazima apatikane mtu au taasisi ama chombo, ili mambo yaende na usipoanzisha hivyo itakuwa tena kizungu mkuti.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwa kiwango fulani nakubaliana na yeye, lakini mengine nimeyaongezea na ni suala la utaratibu, ambao lazima tuufuate.

Nam. 53

Madereva wa SMZ Kupatiwa Mafunzo ya Kisasa

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa madereva wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni miongoni mwa watumishi wa serikali, na kwa kuwa kuna malalamiko makubwa kwa madereva kuwa hawapatiwi nafasi za masomo ya kujiweka sawa (*Refresher Course*), ili kuenda sambamba na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia ambayo inatumika kwa kutengeneza magari ya kileo ukilinganisha na yale ya zamani waliyoyazoea.

(a) Je, ni lini serikali itakuwa na utaratibu wa kuwapeleka madereva wao katika mafunzo, ili kuenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknologia inayotumika katika kutengeneza magari mapya?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 53 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi kwamba mafunzo yawe ya kujiweka sawa (*Refresher Course*) au mafunzo Elekezi ya Awali (*Orientation Course*) au mafunzo mengine yoyote ya kujiendeleza, ni muhimu sana kwa maendeleo ya watumishi. Ni kweli vile vile kwamba, mafunzo sahihi yatakapotolewa kwa wakati sahihi na kwa walengwa husika yatawasaidia sana walengwa hao kwenda sambamba na mabadiliko ya mazingira ya kazi zao ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya teknologia.

Serikali inaamini kwamba moja ya lengo la mafunzo ni kuwafanya watumishi kuacha tabia ya kufanya kazi kwa mazoea na badala yake wafanye kazi kwa ujuzi na maarifa. Mafunzo yanalenga kuwafanya watumishi kuzinduka na kufanyakazi kwa kujiamini zaidi. Sera ya Utumishi Serikalini nayo imesisitiza zaidi juu ya umuhimu wa mafunzo na wajibu wa mwajiri kumpatia mafunzo muajiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa muda mrefu imekuwa ikipeleka watumishi wake, ikiwa ni pamoja na madereva kwenye mafunzo, ili kuwajengea uwezo na kwenda sambamba na mabadiliko ya teknologia yanayotokea ulimwenguni.

Kwa kawaida, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar huwa inagharamia mafunzo hayo, kwa kuzitaka wizara kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika bajeti zao kila mwaka.

Ili kupunguza gharama za mafunzo kutokana na gharama kubwa za usafiri, malazi, chakula na kadhalika, na ili kuhakikisha kwamba madereva na wafanyakazi wengi zaidi wanapata fursa ya kushiriki mafunzo, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Chuo cha Utawala wa Umma katika mwaka wa fedha uliopita iliandaa mafunzo, kwa kuanzia kwa ajili ya madereva wa viongozi, na nafasi za mafunzo hayo kutolewa kwa wizara zote.

Hata hivyo, mafunzo hayo hayakuweza kuendeshwa kama ilivyopangwa kutokana na ufinyu wa fedha.

Kwa hivyo, wizara zilishauriwa kutenga fedha za kutosha katika bajeti ya mwaka huu wa fedha ili kugharamia mafunzo ya watumishi wao wakiwemo madereva. Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma itaendelea kuhimiza na kusisitiza juu ya umuhimu wa mafunzo kwa Watumishi wa Umma, lakini pia itaendelea kuandaa mafunzo mara kwa mara kwa kada mbali mbali, na kwa kada maalum wakati wowote itakapohitajika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe.Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa amekiri kwamba kuna mafunzo kwa wafanyakazi yanatolewa lakini mwaka jana walishindwa kutoa mafunzo kutokana na ufinyu wa bajeti.Vile vile, katika swali langu la msingi lilizungumzia madereva ambao ndio kilio kikubwa kwamba wao hawa wengine wameanza kuendesha gari tangu enzi zile za *Austin, Morris, Austin Mapua* na sasa kuna gari

zinazotumia mambo ya kisasa (*hydro-lick system*) na hadi leo hii ni madereva wa serikali na hawajapata mafunzo haya.

Hivi Mhe. Waziri anaweza akanieleza kwamba tukiachia huu mwaka jana ambao hawakupata kutoa mafunzo kutokana na ufinyu wa bajeti ni madereva wangapi katika kipindi cha nyuma ambao ni madereva wa viongozi, yaani anasema wameanza kutoa kwa madereva wa viongozi. Je, ni madereva wangapi ambao wametolewa kwenda kupata mafunzo ya kujiweka sawa na mumewapeleka katika nchi gani?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, niliposema kwamba bajeti haikuruhusu kuanzisha mafunzo kwenye Chuo cha Utumishi hapa Zanzibar haina maana kwamba hatukupeleka madereva wake kwenda kujifunza mafunzo yale nje ya Zanzibar.

Kwa kweli ni madereva kadhaa na wala siwezi kumpa idadi hivi sasa kwa sababu sijapata takwimu za wizara tofauti, lakini madereva wengi wamepelekwa Tanzania Bara kwa ajili ya kupata mafunzo hayo kwa ngazi ya kwanza, pili na tatu si chini ya madereva 6 ambao ninawajua mimi ambao wamepelekwa na wengine ambao wamepelekwa hatuna tarifa, basi tunaweza kuzikusanya na baadaye tukamjuilisha Mhe. Mjumbe.

Vile vile, ninajua kwamba dereva wa Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko amepata, pia dereva wa Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) naye amepata mafunzo mafupi, dereva wa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma, naye amepata mafunzo mafupi na wengine wengi nina hakika kwamba wamepata mafunzo hayo. Kwa hivyo, serikali imejitahidi na wala hatukuwaacha nyuma madereva tukawaona ni watu wa kada ya chini, tutaendelea na wamepata haki zote na *Alhamdulillah* mambo yao yamekuwa si mabaya.

Nam. 18

Mpango wa Kusaidia Wakulima wa Mpunga

Mhe. Mohammed Haji Khalid – Aliuliza:-

Chakula kikubwa cha Wazanzibari ni mchele lakini wakulima wa Wazanzibar bado hawawezi kuzalisha zao hilo kutosheleza mahitaji kwa kuwa kilimo cha mpunga bado kinategemea mvua ambazo unyeshaji wake sasa hauaminiki.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa wakulima wa Zanzibar wanalima kwa uhakika, ili kupunguza uingizwaji mchele kutoka nje?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 18 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kulieleza Baraza lako tukufu kwa mara nyengine tena, kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili linaendelea kutekeleza dhamira ya kuleta Mapinduzi ya Kilimo kwa kuwashajihisha na kuwapatia taaluma zaidi wakulima. Hivyo, suala la utoaji wa ruzuku ya pembejeo za kilimo ikiwemo mbegu bora, mbolea, dawa za magugu na huduma za matrekta litaendelea kwa azma ya kuendeleza zao la mpunga na mazao mengine ya chakula, ili kuongeza uzalishaji wa chakula cha ndani na kupunguza uagiziaji kutoka nje.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo na Maliasili pia ina mpango mkubwa wa kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde yote ambayo yanafaa kumwagiliwa Unguja na Pemba. Katika zoezi hilo jumla ya hekta 8,521 kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo duniani *Exim Bank*

Korea, USAID, TASAF na *KOICA*, ili kuhakikisha wakulima wa Zanzibar wanalima mpunga wa kutosha kwa matumizi ya chakula kwa familia zao na ziada kuweza kuuza na kujiingizia mapato.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri kiasi ya Mhe. Naibu Waziri. Katika jibu lake amesema kuwa serikali kupitia wizara yake ina mpango wa kutayarisha Kilimo cha Umwagiliaji, ili kuweza kukidhi mahitaji ya chakula cha mpunga.

Kwa kweli umwagiliaji maji na maji yanahitaji msukumo wa umeme. Kwa mfano katika jimbo langu liko bonde ambalo ni la umwagiliaji la Mtambile pale. Je, wizara yako ina mpango gani wa kufikisha umeme katika bonde lile, ili wananchi waweze kumwagilia. Vile vile, watakapofikisha kuna mpango gani wa kutoa bei nafuu kwa wakulima, ili waweze kumudu kuendesha hiyo kazi?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa jimbo lake lina wakulima wa umwagiliaji maji. Kwa hivyo, ninamuomba kwamba avute subiri na umeme utafikishwa katika eneo hilo.

Vile vile, suala la kuwapunguzia gharama za malipo ya umeme. Kwa kweli suala hili linazungumzwa sana, lakini kujua tatizo iliopo katika kilimo cha umwagiliaji maji kwamba kulifuatilia lile tatizo kujua kuna tatizo gani, suala ni bei ya umeme au nini. Sasa baada ya wizara kuona kuna malalamiko mengi juu ya suala la kuwapunguzia wakulima wa kilimo cha umwagiliaji maji gharama za malipo ya umeme.

Mhe. Mwenyekiti, jambo hili nimelifuatilia na tarehe 05/10/2013 nilikuwa na kikao na baadhi ya wakulima wa kilimo cha umwagiliaji maji ambao wamo kwenye mradi wa *TASAF*,

walizungumzia suala hili la kupunguziwa gharama za malipo ya umeme.

Kwa kweli tatizo tumeliona sio bei ya umeme na wala haliko hivyo, isipokuwa ni tatizo baada ya kuzungumza nao wameonesha kwamba kuna tatizo la kuboreshwa miundombinu kwa sababu kama ukiwa huna miundombinu ya udongo, basi bila ya shaka maji yanapotea kwa wingi pamoja na fedha zinatumika kwa wingi. Kutokana na hali hiyo, basi wizara imelifikiria ni kuboresha miundombinu ambayo ni mizuri nafikiri tatizo la kupunguziwa umeme litakuwa halipo.

Tatizo jengine ni kwamba sisi Wizara ya Kilimo na Maliasili tumetoa pembejeo zikiwemo dawa, mbolea pamoja na mbegu na suala la umeme liko kwenye Shirika la Umeme. *(Makofi)*

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kwa kuwa serikali ina mpango wa kuongeza uzalishaji wa kilimo cha mpunga. Lakini hivi sasa ni wakati wa kulima kilimo hichi katika Msimu wa Vuli na kwa upande wa wizara hivi sasa inawahamasisha wakulima hao wapande *Sunflower*.

(a) Je, Mhe. Waziri, suala hili analijua na kama analijua haoni kwamba mwaka huu wanataka kuwakosesha wakulima kuwahi msimu wa kupanda mpunda?

(b) Je, Mhe. Waziri, mauwa hayo yatavunwa wakati gani, ili wananchi hao wapate msimu wa kulima kilimo cha mpunga?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli nalijua suala hili la kilimo cha *Sunflower* katika wizara yangu lipo, pia ni kweli huu ni wakati wa msimu

na mauwa haya ni kweli baada ya kuvunwa tu mpunga yanatakiwa mauwa haya yapandwe na hili ni zao la biashara. Kwa hivyo, baada ya kuvunwa mpunga mabonde haya yanakuwa matupu kwa muda mrefu, lakini kwa mwaka huu kidogo tumechelewa na wamehamasishwa wakulima walime mwanzo na kilichochelewesha ni kufika kwa mbegu tu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuliona jambo tayari ilifuatilie nini athari yake baadaye na tumekaa na kulifuatilia. Sasa baada ya kuhamasisha wakulima na kuona kwamba mbegu hizi zimechelewa basi tuliwarudia tena wakulima. Kwa hivyo, zile konde zilizochimbwa kwa kulima *Sunflower* ukulima ule ule tayari hivi sasa watapanda mipunga wakulima, lakini mwenye kutaka yeyote kulima *Sunflower* kwa kipindi hichi anakonde yake ya eka mbili, ina maana atatoa roho eka kwa ajili ya kulima *Sunflower*.

Kwa hiyo, haitozuia msimu wa kulima mpunga na mauwa haya ni kulima miezi mitatu ina maana miezi mitatu unavuna, yaani hapa mwezi wa Disemba tayari yanavunwa. Vile vile, wataalamu walipokuja na ukulima huu hata kama hayajakauka wakati wa Disemba watavunwa na watakwenda kukausha katika mashine zao bila ya shaka wakulima watawahi katika msimu mzuri wa kulima zao hili la mpunga.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Kwa kweli kutembea ni kusoma kwa nini wakulima wetu wasipelekwe Mbeya na Shinyanga kwa ajili ya kwenda kusoma mambo ya kuweza kutuliza mchele wakati Shinyanga na Mbeya ndizo zinazoweza kutulisha mchele. Sasa kwa nini wakulima wetu wasipelekwe huko kwenda, jinsi wakulima wa huko wanatumia mbinu gani hadi wanaweza kutupa mchele na maharage hapa Wazanzibari wote? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, wakulima wetu kuna *Field Farmer School* wapo baadhi wa wakulima wanakwenda kutembea kila pahala kwa ajili ya kujifunza katika ukulima ambao tunalipa hapa kwetu. Kwa hivyo, kuhusiana na suala hilo Mhe. Mjumbe asiwe na wasi wasi kwamba wakulima wanatembea na kwenda kuona vilimo vya aina tofauti. *(Makofi)*

Nam. 14

Ufumbuzi wa Ugonjwa wa Mahepe kwa Wafugaji Kuku

Mhe. Salma Mohammed Ali – Aliuliza:-
Katika utaratibu mzima wa kuongeza kipato na kupunguza umasikini wananchi wengi wakiwemo akinamama wa vijiji vya Dukani, Vikuunguni, Ditia, Wawi, Mjenga banda na kadhalika wameelekeza maisha yao katika ufugaji wa kuku wa kienyeji na wale wa kisasa. Kwa kuwa ugonjwa wa "magwa" au "mahepe" husumbua sana mifugo hiyo na hatimaye husababisha vifo vya kuku hao jambo ambalo hurejesha nyuma kwa kiasi kikubwa kipato cha wafugaji hao.

Kwa kuwa dawa za kinga zinazotolewa kwa mifugo hiyo zinaonekana hazisaidii. Je, ni lini wizara yako itafanya utafiti wa kina na hatimaye kutoa dawa muafaka ya ugonjwa huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii tena kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 14 kama ifuatavyo:-

Ugonjwa wa Magwa au Mahepe (*New Castle Disease*) unaathiri kuku wa aina zote ambao hawajapatiwa chanjo kwa kukinga ugonjwa huo kwa wakati unaostahiki. Ugonjwa huu husababishwa na virusi. Uchanjaji wa kuku ni lazima ufanyike

kabla ya maradhi hayajatokeza katika eneo, kwani ukifanywa wakati ugonjwa huweza kuwakinga kuku kutokana na ugonjwa huu unaosambazwa kwa njia ya hewa.

Mhe. Mwenyekiti, uchangiaji wa kuku ni lazima uwe unafanyika kila baada ya miezi mitatu kwa kuku wote. Wapo wafugaji ambao wanafuata utaratibu huo na wanafanikiwa kuwakinga kuku wao kutoka na maradhi hayo, hasa wafugaji wa kuku wa kabila za kigeni wa mayai.

Aidha dawa za chanjo zinanzotumika Tanzania Bara na hapa Zanzibar ni za aina moja na zinatoa kinga ya kutosha iwapo zitatumika kwa utaratibu unaotakiwa. Baadhi ya wafugaji hawatumii kabisa chanjo hasa wafugaji wa kuku wa kienyeji na kuwapelekea kupata hasara kubwa sana.

Hivyo, ushauri wangu ni kwamba wafugaji washirikiane na wataalamu wa mifugo kila mara, ili kuwa na mpango bora wa uchanjaji wa mifugo yao na pia kinga dhidi ya maradhi mengine yanayoathiri mifugo na binaadamu.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Katika majibu yake Mhe. Waziri ametwambia kama dawa zinazotumika Tanzania Bara ndizo zinazotumika hapa. Lakini Mhe. Mwenyekiti, siku ya tarehe 16 mwezi huu, katika taarifa ya habari ya ITV nilisikia kama wenzetu Baraza Wizara ya Mifugo ilipiga marufuku dawa ya kinga zidi ya ungonjwa wa mdondo ambao ndio sawa sawa na huu wa mahepe, kwa sababu dawa hizo ni feki na kwa kuwa mara nyingi wafugaji huwa tunanunua dawa za kinga katika maduka ya watu binafsi kwa sababu serikali haina dawa hizi kwa sasa hivi. Wafanyabiashara hawa mara nyingi huwa wanachukua dawa zao kutoka Tanzania Bara.

a) Je, Mhe. Waziri atanambia serikali wamejipangaje kukabiliana na tatizo hili ambalo limetokea Tanzania Bara na sisi tunachukua dawa kutoka huko?

b) Atanambia serikali ina mpango gani wa kukagua maduka haya ya madawa na kama wanakagua maduka haya ya madawa, wanakagua mara ngapi kwa mwaka?

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa Mheshimiwa naomba uelewe kuwa hatufuati taarifa kutoka kwenye vyombo vya habari, tunafuata taarifa zilizokuwa muhimu na kuweza kuzijua. Chanjo ambayo tunaweza kuitumia ni chanjo ya I Two na hiyo mpaka sasa tumegundua inafanya kazi ipasavyo na ni bora zaidi. Lakini kuikagua sio tatizo kama taarifa tumepata zinaweza kututosheleza kutoka katika Wizara yetu ya Mifugo Bara tutawasiliana nao. Ikiwa kama upo uchakachuaji wowote, basi tutafata maarifa ili tuweze kujua tunafanya utaratibu gani wa kuweza kuzichunguza pamoja na kujua tunafanya katika maduka ya dawa mara kwa mara ili kubaini kama kuna watu wametoa uchakachuaji au laa?

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri, maswali ya Mheshimiwa Mjumbe yalikuwa ni (a) na (b) swali la (b) amesema kwamba mmejipanga vipi katika ratiba yenu ya upitiaji katika maduka yanayouza dawa, hilo ndio swali lake la (b).

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nadhani Mhe. Mwenyekiti, nimelijibu kwa pamoja nimesema kama tukipata taarifa za kudumu za uhakika tutaanza kufanya ukaguzi katika maduka yetu ya dawa ili kubaini kama kutakuwa na uchakachuaji au laa.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mwakilishi na kazi yangu ni kutetea wananchi pamoja na wafugaji, kwa sababu pia natokea katika mifugo. Mhe.

Mwenyekiti, taarifa zinazotoka katika vyombo vya habari ni taarifa za kuzifanyia kazi, hasa pale Mhe. Naibu Waziri alipotwambia kwamba Zanzibar tunatumia dawa kutoka Tanzania Bara, na sisi tunanunua dawa katika maduka ya wafanya biashara na wafanya biashara hao wengi wanachukua dawa kutoka Tanzania Bara.

Sasa hofu yangu kwa Mhe. Waziri, kusema kwamba kuna dawa ya aina fulani ndiyo inayotumika wakati wafugaji wao dawa wananunua katika maduka ya wafanyabiashara. Namuomba Mhe. Naibu Waziri alifanyie kazi hili asiseme kwamba wao hawana taarifa, taarifa imetoka katika vyombo vya habari na sisi tumeisikia na wafugaji hawajui wao wakenda kununua dawa pale kama hii ni feki au si feki.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda nimuulize Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza.

Wafugaji wengi kuku wao walipokumbwa na ugonjwa huu kwa sababu huamua kuwachinja na kuwafanya kitoweleo. Je, hakuna athari yoyote kula kuku wa aina hii?

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, mpaka sasa hakujawa na taarifa yoyote au uchunguzi uliofanywa kwa kuwa wananchi wanaweza kuathirika kwa kuchinjwa kuku wanaopata mahepe au magwe.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mhe. Mwenyekiti, wananchi wamekuwa na mazowea wale kuku wanaopata mahepe au magwa, suluhisho ni kuwachinja na kuwala. Je, kitaalamu kuku hawa wana madhari gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali lile lile nililomjibu Mhe.

Mohammed Haji Khalid na limekuja tena kama lilivyo kwa Mhe. Hija Hassan Hija.

Nataka kusema hatujafanya utafiti mpaka sasa ambao unaonesha una madhara kwa kuku wanaopata mahepe kuchinjwa na kuliwa na wananchi. Lakini hata hivyo taarifa hiyo nitaichukua na kuifanyia kazi ipasavyo.

Nam. 76

Ubovu wa Barabara ya Mkunazini Kuelekea Kisiwandui

Mhe. Saleh Nassor Juma Kny/Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa kipindi kirefu sasa barabara inayotokea Mkunazini kuelekea Kisiwandui imekuwa na ubovu katika sehemu mbaya ya mpindo (*corner*) ambayo inahatarisha usalama wa watumiaji wa barabara kama vile vyombo vya moto, baiskeli na waendao kwa miguu wakiwamo watoto wa skuli.

(a) Wizara haina habari na ubovu wa barabara ile na hatari iliyopo kutokana na ubovu ule?

(b) Lini wizara itachukuwa hatua ya kufanya matengenezo ya sehemu ile ndogo ili kuepusha usumbufu mkubwa wanaopata watumiaji wa barabara ile?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 76 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inafahamu usumbufu na changamoto zinazojitokeza kutokana na tatizo la mikunjo ya

barabara katika eneo hilo na Mkunazini katika taa za kuongozea magari mpindo wa kuelekea Kisiwandui. Katika mipango ya wizara tunategemea mapema mwaka huu eneo hilo tuweze kulisawazisha. Hata hivyo, kama sote tunavyofahamu kulikuwa na maeneo ambayo yameharibika vibaya sana na busara zikatuelekeza tuyanusuru maeneo hayo kwani bado eneo hilo liko afadhali ukilinganisha na maeneo hayo.

Maeneo ambayo tumeyachukulia hatua hizo ni pamoja na barabara ya Mkwajuni/Mkokotoni, barabara ya Mkwajuni/ Gamba, Upenja kuelekea Kiwengwa, barabara ya Gana kuelekea Kitope, Tunguu Mchavyani na baadhi ya maeneo korofi katika mji wa Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake yote mawili kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Wizara inaifahamu hali ya ubovu wa sehemu ya barabara kwenye makutano ya barabara hapo Mkunazini. Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa kutumia fedha ya Mfuko wa Barabara tunatengemea haraka baada ya kukamilika kazi ya ujenzi wa Amani/Mtoni eneo hilo kazi hiyo itafanyika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu swali la msingi la Mhe. Jaku Hashim Ayoub, linasema kwamba sehemu inayotokea Mkunazini kuelekea Kisiwandui katika kona pale inatatizo na ni kipande kidogo mno. Na kwa kuwa Mhe. Mwenyekiti, lazima tukubali kwamba Unguja Mjini ni sehemu ya uchumi wa nchi yetu hii hususan katika sekta ya utalii.

(a) Je, isingekuwa vyema Mhe. Waziri akazuia sehemu hii moja inayotengenezwa barabara akaja hiki kipande hiki wakakiweka sawa, ili wale watalii wasipate matatizo pale pamoja na wageni wetu na kuweka sura mbaya katika uso wa nchi hii yaani *Zanzibar Town* kwa kuweka

matengenezo katika kipande hicho kidogo? Ingekuwa ni vyema ukaacha huko ukaweka matengenezo pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli ushauri wa Mhe. Mjumbe ni mzuri lakini sisi Wizarani tunalizingatia hilo na kipindi hichi tupo katika hatua ya mwisho ya kuandaa mchakato wa kufungua zabuni ili kuweza kupata kampuni binafsi na kuweza kufanya ile kazi haraka kwa malengo ya kunusuru ile hali pale kama vile anavyosema Mhe. Mwakilishi.

Nam. 47

Athari za Kutumia Mkonga wa Mawasiliano kwa ZBC

Mhe. Salma Mohamed Ali Kny/Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-
Tuliambiwa kuwa ili kuweza kupata taarifa na ufanyaji kazi vizuri wa ZBC TV ni lazima mkonga wa mawasiliano uweze kutumika ipasavyo.

(a) Je, ujenzi wa mkonga huu umekwamishwa na nini katika kukamilika kwake?

(b) Je, kutopatikana taarifa na picha vizuri kunatokana na tatizo la kutokamilika kwa mkonga?

(c) Mhe. Waziri analiambia nini Baraza hili Tukufu (BLW) kutokana na kadhia hiyo?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 47 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa mkonga wa Taifa haujakwama, kwani hivi sasa kuna shughuli za kusambaza miundombinu ya mkonga huo kutoka vituo vya uunganishaji hadi kwenye sehemu za matumizi. Waya za mkonga huo zimeshafikishwa kwenye sehemu za matangazo ya Karume House na Redio Rahaleo, hatua inayofanyiwa kazi ni kupata viunganishi vya waya huo na mkonga na mitambo ya utangazaji.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kutopatikana kwa picha nzuri kunatokana na matatizo kadhaa likiwemo hilo la kutoanza kutumika kwa mkonga kupitisha matangazo, lakini sababu nyengine ni uchakavu wa studio za matangazo, sababu zote mbili zimeanza kufanyiwa kazi na serikali.

(c) Mhe. Mwenyekiti, ninaloweza kuliambia Baraza lako Tukufu, ni kwamba wizara yangu kupitia Shirika la ZBC imetiliana sahihi na Kampuni ya *Sony* kujenga studio mbili za kisasa Unguja na Pemba. Pia, Kampuni ya *Ágape* inarekebisha kasoro zilizoonekana katika kipindi cha majaribio ya Dijitali na Taasisi inayohusika na uendeshaji wa mkonga inaonekana ikisambaza waya wa mkonga hadi kwenye sehemu za matumizi. Mambo hayo matatu yakimaliza kurekebishwa hali ya upatikanaji wa taarifa, picha na matangazo ya ZBC yatakuwa vizuri sana na ndio malengo ambayo yanafanyiwa kazi.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Pemba mara nyingi huwa wanakosa matangazo ya ZBC jambo ambalo huwa linawaletea masikitiko makubwa. Na kwa kuwa wananchi hao wanategemea sana huu mkonga wa taifa kuwa ndio mkombozi wao wa tatizo hili.

(a) Je, kwa upande wa Pemba matangazo kupitia Mkonga wa Taifa yatapelekwa kwa njia gani na lini?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti,

a) Kisiwa cha Pemba kuna njia mbili ya kupeleka *signal* za Mkonga wa Taifa, njia ya kwanza ni kupitia Unguja kutoka hapa Mazizini hadi kwenye mnara wa Nungwi na kutoka Nungwi kupitia *Maikroweves* hadi Kichunjuu Pemba na ukasambaza katika Pemba nzima, hiyo njia ya kwanza.

b) Njia ya pili, kupitia kutoka hapa Mazizini kupitia *Sub- Marine Cable* iliyounganishwa kutoka waya wa umeme hadi Dar-es-Salaam na baadaye hadi Tanga na kutoka Tanga, kupitia *Sub-Marine Cable* iliyounganishwa na mradi wa umeme hadi Pemba.

Kwa hivyo, hizo ndio njia mbili ambazo Mhe. Mwenyekiti, Kisiwa cha Pemba kinaweza kupata matangazo kupitia Mkonga wa Taifa hadi Kisiwa cha Pemba. Shughuli hizo zinafanyiwa kazi kama nilivyosema. Na lini ukweli siwezi kusema hasa ni lini lakini ninachokwambia hivi sasa serikali kupitia taasisi zinazohusika inashughulikia kufikisha Pemba matangazo hayo ya Mkonga wa Taifa.

Nam. 79

Ukosefu wa Chakula Katika Hospitali ya Wagonjwa wa

Afya ya Akili K/Chekundu

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny/Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuulizwa swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub, naomba kwanza nitumie fursa hii kumpongeza sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwa kuweza kutetea sana wananchi katika suala zima la huduma za jamii. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Spika, kama kuna uwezekano wa

kumrudisha tena kwenye Kamati ile basi amrudishe katika Kamati ile ili aendelee kuwatumikia wananchi kwa kushirikiana na Naibu Waziri wa Afya (Dokta Sira Mamboya).

Mnamo tarehe 14/8/2013 na tarehe 15/08/2013, wapishi wa Hospitali ya Kidongo Chekundu waliambiwa waende zao kwa kuwa hakuna chakula cha kupika, hii ikimaanisha kuwa hawakuwa na kazi ya kufanya. Katika kikao cha Baraza cha Januari, Wizara iliahidi, na kumbukumbu zipo kuwa chakula kitapatikana katika Hopitali hiyo.

(a) Je, kwanini hadi sasa ni mwezi wa kumi ahadi hiyo haijatekelezwa na badala yake wapishi wanaambiwa waende zao kwa kuwa hakuna cha kupika?

(b) Wizara kwa kutotekeleza ahadi hiyo inakusudia wagonjwa wa Hospitali ile wafe njaa?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-
Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 79 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, nafikiri katika Baraza hili hakuna asiyefahamu suala la upatikanaji wa fedha katika kipindi cha bajeti. Fedha za OC ambazo ndizo zinazonunuliwa chakula, na mara nyingi zinaanza kupatikana baada ya bajeti kwisha. Bajeti ya mwaka huu Wawakilishi nyote mashahidi maana ndio mliolikuza Baraza likachukua muda mrefu kuliko siku zilizokadiriwa. Kama ilikuwa fedha zitoke kwa ajili ya OC itakuwa tumelipwa sie tulokaa Barazani, kwa sababu nnawasiwasi kwamba hakukuwa na bajeti ya siku zilizoongezeka na mfuko ndio huo huo hakuna mwengine. Lakini jambo ambalo nnahakika nalo kwamba wafanyakazi wakikosa cha kupika hawarudishwi nyumbani, atakuwepo japo kufanya usafi wa jikoni.

(b) Ahadi inatekelezeka kama cha kutekelezea kipo. Lakini hata hivyo wizara haikukaa tu, ikasubiri Baraza lishe na fedha zitoke. Watendaji wetu walihangaika kwa njia wanazozijua wao wenyewe, chakula kikaendelea kupikwa katika Hospitali ya Kidongochekundu, kama walibangaiza kwa chakula cha mchana hayo mengine, lakini asubuhi na usiku kwa uhakika mikate na chai vinapatikana. Wagonjwa wenyewe walijuilishwa hali halisi na watu wanaendelea kuwaletea wagonjwa wao chakula. Wagonjwa wasiokuwa na kuwaletea chakula ni watatu tu nao wanahudumiwa. Mhe. Mwenyekiti nataka nikuhakikishie "Hafi mtu kwa njaa katika Hospitali ya Kidongochekundu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya mdogo wangu Mhe. Naibu Waziri wa Afya, naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kanuni za chombo hichi zinatutaka mtu awe na uhakika wa kile anachokisema bila ya kujali kwamba yeye ni *back benchers* au yupo *front bench*. Sasa nilikuwa nataka hapa Mheshimiwa kwa bahari mbaya mdogo wangu Waziri wa Nchi, Ofisi wa Makamu wa Pili hayupo lakini Makamu wa Pili wa Rais yupo mwenyewe. Kwa sababu Mhe. Naibu Waziri, kasema kwamba anawasiwasi kwamba fedha ya OC ambayo Wawaheshimiwa Wawakilishi waliitumia baada ya kuongeza muda wa Baraza badala ya kugaiwa wizara kama OC ikawahudumia wagonjwa wa Kidongochekundu.

Sasa huku Mhe. Spika, katika kikao kile alikuwa akisisitiza kwamba jamani bajeti inamalizika, sasa tunatumia bajeti ya kikao kijacho alikuwa akitwambia hivyo. Leo Mhe. Naibu Waziri wa Afya anatwambia kwamba ni fedha za OC.

a) Je, lipi ni lipi, ukweli ni ule wa Mhe. Spika, au ukweli wa Naibu Waziri wa Afya? Naomba Mhe. Makamu wa Pili, atueleze ikiwa

tunapopitisha bajeti hapa tunapewa pesa za OC hatuna haja ya kuwadhulumu wananchi. Mimi nadhani atueleze ukweli tukitumia pesa za OC au tukitumia fedha hizi za vikao vyetu vya Baraza vilivyokuwa vya mbele.

b) Mhe. Mwenyekiti, amesema hafi mtu kwa njaa kwa sababu ana uhakika ikiwa kitakosekana chakuka cha mchana basi chai wakati wa usiku na asubuhi itapatikana kiuhakika. Mimi nadhani atueleze hii chai ya asubuhi na usiku inatolewa na serikali au inatolewa na Summa muwekezaji mzalendo. Serikali ina *play role* gani kuwapatia hicho chakula cha mchana wakati kuna taarifa kwamba Summa *LTD* hii kampuni ya Kizalendo ndiyo inayotoa chai ya asubuhi na chai ya usiku pale Kidongochekundu. Sasa ikiwa Summa anatoa hivyo, nyiye kwa nini mshindwe kama serikali ishindwe kutoa chakula cha mchana?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nani anajibu? Maana alitaka Makamu mimi ndio nijibu Ishallah.

Mhe. Mwenyekiti, ninachokisema nimesema hivi, nataka nirudie nilichokisema na nataka anifahamu vizuri. Nina wasi wasi kwamba siku hizi zilizoongezeka. Nakumbuka hapa na miye barabara hili hili nilikuwemo na Spika alipokuwa akisema nilikuwa hapa hapa. Sasa ufahamu nao kunakuwa na ufahamu tofauti, lakini tuliongeza siku nyingi mno mpaka Spika akawa sasa ana wasi wasi. Kama kuongezeka zinatakiwa ziongezeke siku 2,3,4 au 5, wiki tatu tunaendelea na Baraza hilo hilo, mpaka Sikukuu imefika hapa hapa, kweli hizo pesa zote zilikuwepo.

Lakini baada ya hapo na sisi kipindi kirefu kimepita bila ya kupata OC nifikirieni mtu kama miye ambaye ninayefikiria bajeti iliyopo na nchi yetu hii na mapato yanayopatikana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Naomba sana Mhe. Naibu Waziri, kanuni hazitaki ziwe na wasi wasi, ikiwa ana wasi wasi afute maneno.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Kanuni zinataka zisiwe na wasi wasi, ninachozungumza hapa ni kile ninachokiona kwamba hakukuwa na pesa zilizokuwepo, pesa zilizotumika kwa sababu hazikuwemo kwenye bajeti.

Mhe. Mwenyekiti: Swali la pili umemaliza kujibu?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Sijamaliza.

Mhe. Mwenyekiti: Haya endelea kujibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: (b) Anasema kwamba kwa nini serikali haikutoa pesa za chakula cha mchana wakati huo uhakika niliokuwa nao wa chakula kinatolewa na Summa asubuhi na jioni.

Swali la msingi linasema watu watakufa kwa njaa wakikosa kula. Nani anatoa kula, haimati. Mtu anaweza akatoa kula akiwa Summa akiwa mwengineo, lakini serikali inatumia pesa za OC na hazikuwepo kwa kipindi hicho. Kwa hivyo, hicho cha mchana hakikutoka kwa sababu OC haikuwepo. Summa akitoa, akitoa mwengine yeyote huo si msingi, msingi watu wamekula hawakula?

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu ambayo hayaridhishi sana ya Mhe. Naibu Waziri, naomba nimuulize swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza. Baraza hili limeendeshwa kwa fedha ambazo zimetengwa na Baraza kutupitia Tume ya Bajeti ya Baraza. Na Kidongo Chekundu wanaendesha mambo yao kupitia bajeti iliyotengwa na serikali kupitia Wizara wa Afya. Kwa nini Naibu Waziri asingizie matumizi ya Baraza kukwepa matumizi ya Kidongo Chekundu ambayo fedha imetengwa na Baraza hili kwa ajili ya wagonjwa wale?

b) Hivyo, miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar wagonjwa wale kula kwa msaada wa Summa si udhaifu wa serikali kupitia wizara yako?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti,

a) Wizara ya Afya hatukuwa na matumizi, Wizara ya Afya haikuwa na fedha za OC ndicho ninachoendelea kukisema. Ingekuwa OC zimetiwa chakula kingepikwa lakini kama hazikutiwa ina maana kwamba hatukuwa na matumizi kwa kipindi hicho.

b) Miaka 50 inakuja, ni kweli miaka 50 tunafanya lile tunalokuwa nalo na katika uwezo wetu. Sidhani kama tutapindukia, pesa za OC zikiwepo tutapika chakula, kama hazitokuwepo tutafanya kama tunavyofanya hivi sasa hivi, tutashirikiana na walionacho kwa kuhakikisha kuwa wagonjwa wetu wanakula.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri aliyeyatoa Mhe. Naibu Waziri wangu, naomba kuweka sawa suala la Summa na watu wengine kupeleka chakula kwenye hospitali ile. Ni suala la hiari, ni wenyewe waliotaka ni sadaka zao katika sadakatu jaria, hakuna aliyelazimishwa. Lakini hiyo haiondoi wajibu wa serikali kuwasaidia wagonjwa wale.

Naendelea kusema kama na Waheshimiwa na wao wanataka kuweka sadakatu jaria tunakaribisha wapeleke chakula kwenye wagonjwa wa akili. Si suala kwamba serikali haina uwezo au ni kwa sababu kwamba tumetimiza miaka 50 uwezo haupo.

Naomba hilo likuweka sawa kwamba ni wenyewe waliotaka kwa hiari, mimi namjua mmoja kila siku ya Ijumaa kwa miaka ya zaidi ya kumi sasa anapeleka chakula kama ni sadaka, hajalazimishwa wala hatumwambii kama leo hakuna chakula tuletee. Nilitaka kuliweka sawa hilo tu Mheshimiwa.

Nam. 59

Nyumba ya Kulelea Watoto Forodhani Kutumika Vibaya.

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kuna taarifa kuwa jengo lililokuwa likitumika kwa kulea watoto wenye mazingira magumu lililopo Forodhani hapo awali lilikuwa la *Islamic Academy* na maulamaa kadhaa kutoka Zanzibar na nchi za nje walisoma pale.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea jengo hilo apewe mwekezaji wa hoteli ya Pombe mara baada ya kuondoshwa watoto waliokuwa wakilelewa?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu :-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam 59 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, jengo lililokuwa likitumika kwa kulelea watoto wenye mazingira magumu liliopo Forodhani limekodishwa kwa muekezaji wa hoteli siku nyingi kabla ya watoto hao kuondoshwa.

Mhe. Mwenyekiti, muekezaji huyu amekodishwa sehemu ya chini ya jengo upande wa bustani ya Forodhani wakati eneo

ambalo lilikuwa likitumiwa kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu liko sehemu ya juu ya jengo hilo. Jengo hili liko chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Hifadhi na uendeshaji Mji Mkongwe na baada ya watoto hao kuhamishwa eneo walilokuwa wakilitumia hivi, sasa linatumika kwa shughuli mbali mbali za Mamlaka.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Swali langu ni kwamba mmilikaji wa jengo lile alikuwa ni *Islamic Academic* ambapo maulamaa wengi walipita pale, limekodishwa kwa muwekezaji anayetumia kwa mambo haya ya kuuza hizi pombe. Sasa naona Mheshimiwa sikupata jibu.

(a) Je, lilikuwa hili jengo linamilikiwa na taasisi ya kidini na sasa kapewa muekezaji anaeuza pombe hili suala ni kweli? Ndio nataka nijibiwe halafu niulize swali la nyongeza. Naona Mheshimiwa sikupata majibu naomba nijiwe?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli jengo hili lilikuwa linatumiwa na baadhi ya watu kama mashehe ambao walikuwa wanatoka sehemu mbali mbali na baadae jengo hili likawekwa *special* kwa ajili ya kulelewa watoto na hatimaye jengo hili sehemu ya chini limekodishwa muekezaji, lakini sehemu ya juu likawa linaendelea na kulelewa watoto. Lakini kwa sasa hivi watoto hao wameondoshwa, eneo ambalo lilikuwa linalelewa watoto lipo na tupu kwa sasa hivi, kubwa kinachofanyika ni kufanyiwa matengenezo na kutumiwa katika shughuli nyengine za kiserikali.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Saleh hujaridhika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Kwa sababu Mheshimiwa nilitaka nijibiwe lile la msingi lilikuwa halijajibiwa ndio kanijibu sasa hivi swali langu la msingi. Sasa ndio nasimama kwa ajili ya swali nyongeza. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na

majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, ninashukuru kwamba amekiri kwamba jengo lile lilikuwa la taasisi ya kidini na ambayo taasisi ile ilitoa kwa ajili ya kulelewa watoto walio na mazingira magumu. Lakini sasa Mhe. swali lipo hapa. Kwa sababu msingi wa jengo lile watu wa dini kulelea watoto na serikali imeamua kutoa sehemu moja ya jengo lile kwa ajili ya kuweka pombe, huku jengo lile asili yake ni mambo ya dini.

(a) Je, haoni kwamba serikali itasababisha mvutano baina ya watu wa dini na yeye mwenyewe serikali au na hao walioekeza hapo?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninamtanabahisha kwamba lile jengo halijawahi kuwa la taasisi ya kidini, jengo lile ni mali ya serikali kwa bahati ilikuwa imefanywa shule pale ikiitwa *Muslim Academy* kwa wakati huo. Baadae serikali ikachukua hatua ya kutafuta eneo jengine kwa ajili ya kuweka *Muslim Academy,* ndio ikajenga Mazizini kuifanya pale sasa hivi ni *Muslim Academy* yaani Chuo cha Kiislam kwa kuondoka pale.

Ni kweli kwamba pale walisoma maulamaa wengi wakiwa wanafunzi na wakatoka wakaendelea katika vyuo vikuu vyengine mbali mbali duniani hiyo ni kweli. Lakini hata hivyo, lile jengo ni mali ya serikali, kilichofanywa pale chini ni kwamba imefunguliwa *restaurant,* sasa hiyo *restaurant* labda imetokezea kwamba pamoja na vitu vingine inavyouza chakula na mengineyo pengine kuna na hizo *shurba* ambazo zinapatikana pale. Lakini tujuwe kwamba lile ni jengo la serikali na halijawahi kuwa la taasisi ya kidini.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mimi Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kujua utaratibu uliotumika wakumkodisha au kumpangisha huyo Mwekezaji. Pili, nataka kujua fedha inazopata serikali na ukodishaji huo ni wa muda gani ni miaka mingapi?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji Nishati: Mhe. Mwenyekiti utaratibu uliotumika kumkodisha Muekezaji ni utaratibu wa kawaida unaotumika kuwakodisha wawekezaji wote katika majengo ya serikali. Ama hesabu ya mapato nitamuomba aniachie nimletee kwa maandishi.

Utaratibu

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Naomba nitumie kanuni ya 37 inayoelekeza utaratibu wa kujibu maswali kwa usahihi na uhakika kabisa. Nilichouliza ni utaratibu gani uliotumika, lakini Mhe. Waziri, hakusema ule utaratibu uliotumika anasema utaratibu wa kawaida. Katika taratibu za kawaida ziko nyingi nilikuwa nataka nione ule utaratibu atwambie ambao umetumika katika kumkodisha Yule. Je, ilikuwa ni tenda kuna aina nyingi za ukodishaji au za huo utaratibu unaotumika? Sasa nilikuwa nataka nione ule utaratibu ambao yeye aliutumia katika kukodisha pale.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji Nishati: Mhe. Mwenyekiti, Baraza letu zuri siku hizi maana mtu anaweza kuuliza maswali mara mbili kwa wakati mmoja. Mhe.Mwenyekiti, utaratibu wa kawaida ni kwamba hata yeye Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, kama ameliona jengo mahala na anataka kufanya biashara huwa anaomba katika Idara ya Nyumba kukodishwa jengo lile. Lile jengo anakuwa kaliomba yeye, Idara inakaa kitako kufikiria kwamba inaweza kumkodisha, hatuwezi kumkodisha. Lakini serikali yenyewe inapoamua kukodisha hapo ndio huwa inatangaza tenda kwamba jengo fulani linakodishwa. Lakini kuna majengo ambao serikali haikutangaza kuyakodishwi lakini mtu anakuja anaomba na anakodishwa.

TAARIFA ZA SERIKALI

Taarifa ya Serikali juu ya Hoja mbali mbali za Kamati ya PAC ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Shirika la Umeme ZECO

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa wajumbe majadiliano leo yanaendelea tuna wachangiaji wanane wakiwemo Mhe. Hamza Hassan Juma na baadae Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa na baada ya hapo tutakuwa na Waheshimiwa mawaziri ambao nao, pia, wanataka kuchangia katika ripoti hii ambaye mchangiaji wa mwanzo katika Waheshimiwa Mawaziri atakuwa Mhe. Abubakar Khamis Bakary, baada ya hapo Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, atafatiwa na Mhe. Haroun Ali Suleiman, Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, baadae atakuja Mhe. Mwanasheria Mkuu na baada ya hapo tutakuwa na mwenyewe mwenye ripoti hii ambaye ni Mhe.Waziri, Mohammed Aboud Mohammed.

Waheshimiwa ninakuombeni sana tutulie kwa sababu leo tunatarajia hoja hii tuimalize mchana huu. Kwa hivyo, naomba sana tutulie ili sote tuweze kukubaliana kwa pamoja kupitisha ripoti hii.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nikushukuru kunipa nafasi hii nikiwa mchangiaji wa mwanzo katika ripoti hii ya serikali kuhusu hoja au kuhusu maamuzi ya Baraza kuitaka Kamati ya PAC kwenda kuchunguza utaratibu au ukiukwaji wa taratibu mbali mbali katika Shirika la Umeme.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo nataka kuugawa mchango wangu katika maeneo manne na maeneo manne hayo nitayachangia kwa mujibu wa nyadhifa zangu nilizokuwa nazo. Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati Mwalim Nyerere marehem Mungu amlaze mahali pema, yeye alikuwa na kofia mbili. Alikuwa na kofia ya

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, lakini vile vile, akawa na kofia ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sasa mimi leo mchango wangu nitachangia katika kofia nne nilizonazo. Kofia ya mwanzo nikiwa Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Kwamtipura, kofia ya pili nikiwa mjumbe wa Halmashauri kuu ya taifa ya CCM, lakini kofia ya tatu nitachangia kama Mwenyekiti wa kamati ya wenyeviti na kofia ya nne nitachangia kama Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una kofia nyengine ya tano, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Hiyo ndio ya mwanzo niliyoitaja Mhe. Mwenyekiti na hiyo ndio nitakayoanza nayo.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wa Kwamtipura hawakukosea kwa kumleta Mwakilishi wao makini katika Baraza hili ili kuja kuwatetea kwa maslahi yao mbali mbali ndani ya Jimbo la Kwamtipura pamoja na Zanzibar nzima. Pale wananchi ninapohisi hawakutendewa haki ni wajibu wangu kuwatetea ndani ya Baraza la Wawakilishi, lakini vile vile kwa mwananchi yoyote anayekwenda kinyume na taratibu za serikali ni wajibu wangu kusimamia kuhakikisha kwamba taratibu za serikali au za kisheria zinafuatwa.

Mhe. Mwenyekiti, naanza hoja yangu kwamba kwanza kwa niaba ya wananchi wa Kwamtipura, mimi nataka niishukuru sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kukubali kunyumburika kuwa *flexible* kwa kukubali kuambiwa, tunajua tunatoka mbali na serikali hii ni serikali ambayo imekuja kukumbana na mageuzi makubwa ya kisiasa hapa Zanzibar, mageuzi ambayo yameleta uwazi na ukweli na uadilifu ndani ya chombo hiki cha kutunga sheria. Lakini ninashukuru kwa kujitahidi kwenda na kasi ya mabadiliko ya demokrasia Zanzibar lakini, vile vile, na

kasi ya matakwa ya utekelezaji wa sheria ambayo wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanavyotaka.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niishukuru na Ofisi yako kwa kutukubalia tunapotaka kuihoji na kui- *search* na kuipekua serikali kiti chako kuturuhusu kuweza kufanya kazi hiyo, kwa kweli hiyo ni demokrasia kubwa na kwa kweli wananchi wote wa Zanzibar wanaridhika sana na utendaji wa chombo hicho cha Baraza la Wawakilishi lakini, vile vile, na kukubali japo kwa mwendo wa pole kwa serikali yetu kukubali na kuweza kutekeleza baadhi ya yale matakwa ambayo tunayoyahitaji.

Mhe. Mwenyekiti, katika hoja ambazo Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, alilitaka Baraza lako kupitia hoja hii kwamba tuangalie upya kanuni zetu alitaka tuangalie upya kanuni zetu kwa sababu kanuni zetu zinataka kama italetwa hoja binafsi basi yule mjumbe aliyetoa hoja alitakiwa na yeye awemo katika hiyo kamati. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti hoja hiyo ya Mhe. Waziri siikubali kwa sababu kama mjumbe aliyetoa hoja yeye ndie mwenye taarifa za kutosha yeye akiwemo katika ile kamati yeye ndie atatakiwa afatane na ile kamati kwa ajili ya kuisaidia taarifa mbali mbali alizonazo na kwa sababu kwa kuwa utaratibu wetu kama Baraza la Wawakilishi hatuzungumzi siri, kama kuna tuhuma za mtu anaitwa kwenye kamati anahojiwa, anajieleza na yale maelezo yake baada ya kuthibitika ule ukweli aliloueleza ndio ripoti ambayo iliyokuja hapa.

Sasa leo Mhe. Waziri kutaka turekebishe kanuni zetu hizi mimi nadhani serikali inataka kuingilia muhimili huu wa Baraza jambo ambalo sio sahihi. Lakini kupitia ushauri wa Mhe. Waziri na mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti ninawashauri wenzangu tangu juzi tulikuwa tuna semina ya kupitia kanuni zetu, bado kanuni yetu ina mapungufu. Na katika maeneo ambayo yana mapungufu, moja tunakuwa tunalalamikiwa sana hapa kwamba tunawasema watu au tunasema taasisi wao

wenyewe hawapati nafasi ya kujieleza. Sasa hivi Mhe. Mwenyekiti naomba Katibu mezani achukue hoja yangu kwamba tufanye marekebisho ya Kanuni mtu yeyote anayetajwa, kwa sababu yeye hapati nafasi ya kuja kujitetea kwenye Baraza la Wawakilishi basi apewe nafasi kwa mujibu wa kanuni ya kuleta maandishi ya kujitetea na sisi ili tuweze kuzungumza au kujadili ule utetezi wake.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika kurekebisha kanuni zetu, Mhe. Mwenyekiti juzi baada ya kumaliza hoja hii wenzetu waheshimiwa mawaziri walipata nafasi ya kuitana kwa sababu wao wana Kiongozi wa Shughuli za Serikali Barazani na serikali yetu kama tunavyoijua ni serikali yenye mfumo wa umoja wa kitaifa, haiongozwi kisiasa inaongozwa katika masuala mazima ya utawala bora, Mawaziri wa pande zote mbili wamekutana wakajadili ili kujenga hoja na ndio maana leo mawaziri watasimama karibu wanane kwa ajili ya kujibu hoja zetu.

Mhe. Mwenyekiti kanuni yetu ina mapungufu naomba na hili tulifanyie marekebisho, kwa kuwa sisi tuna wanadhimu wa vyama, sisi tumebaguliwa kwenye kanuni yetu au tumejibagua wenyewe kwa sisi ndio tunaoweka kanuni. Sisi tumejibagua, Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi atawaita watu wa Chama chake, na Mnadhimu wa Chama cha CUF atawaita wanachama wake. Kwa hivyo, wanakwenda kupeana misimamo ya kivyama sio misimamo ya kutetea nchi moja kwa moja. Unajua katika vyama kuna *whip* hapa Barazani unatetea masuala ya jimbo lako, unatetea masuala ya wazanzibari wote halafu, vile vile, bila kukiuka misingi ya chama chako.

Sasa wanadhimu wao wanatuita kwa mujibu wa misingi ya vyama vyetu, sasa na sisi tufanye marekebisho ya kanuni ili sasa tuwe na mnadhimu kwa upande wa *backbenchers* ambayo yeye hatoangalia chama hiki wala chama hiki, isipokuwa kwa mambo ambayo yanayohusu sera, yanayohusu misimamo ya vyama, wanadhimu wataendelea na majukumu yao vile vile.

Sasa Mhe. Waziri yeye kataka tuondoe au tutengue kifungu cha kanuni kilichomtaka mjumbe aliyetoa hoja aingie kwenye kamati sasa sisi tunaongeza na vifungu vyengine viwili ili kanuni yetu izidi kuwa imara zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika hoja zangu, katika hoja ambazo zilizozungumzwa na Mhe. Waziri, Mhe. Waziri ukiangalia *paper* yake yaani amejiweka kati kati hakutaka kuikaidi kamati wala hawakutaka na wao serikali kukiuka yale maamuzi ya kamati. Sasa kwanza wameisifu kamati, wamemsifu na mtoa hoja na kakiri mapungufu yaliyotokea katika Shirika la Umeme. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho nilichokiona mapungufu ambayo tuliyoyafanya tulipokuwa tukipitisha yale maazimio, kwa kweli hatukuweza kutoa mapendekezo ya moja kwa moja, isipokuwa tu mapendekezo yetu mengi tulisema watendaji wote wanaohusika wachukuliwe hatua za kinidham na kisheria, ndio maana serikali ikaji-*defend* kwamba kuna watu wengine taarifa zao zimeshashapelekwa Polisi wengine wamepewa maonyo, wengine wamesimamishwa kazi. Sasa utakuta tumetoa *loop hole* kwa serikali ili sasa kufanya vile wanavyotaka wao.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho ninachotaka kukisema kwamba katika maamuzi haya matatu yaliyofanywa na serikali, kuna baadhi ya maamuzi yapo kisheria, mfano kama kutoa onyo, yapo kwenye kanuni na sheria lakini kuna baadhi ya mambo mengine ya kuwahamisha watu kuwaondoa sehemu moja, kuwapeleka sehemu nyengine wakati moja kwa moja ushahidi wa kutosha upo kwamba wameiibia serikali, wameliibia Shirika, maamuzi haya mimi sitoyakubali na hili nitaliomba sana ili ripoti yetu hii isije ikawa na mvutano mkubwa wa kupitisha. Lazima serikali watukubalie baadhi ya mambo ambayo kwa kweli hatukuridhika nayo katika maamuzi hayo.

Mhe. Mwenyekiti, mfano katika hoja ya mwanzo wateja kupewa risiti zenye kiwango kidogo kuliko malipo halisi waliolipa. Mhe. Mwenyekiti, huu ni wizi, huu ni wizi kabisa tena wa

mchana. Kwa sababu haiwezekani mtu kalipa pesa nyingi halafu umpe risiti ya pesa kidogo. Kwa hivyo, ina maana zile pesa kidogo zilizokuwemo kwenye risiti ndio zilizoingia kwenye Shirika, zile pesa nyingi ndio zimeingia kwenye account yake, Mheshimiwa huu ni wizi. Na kwa bahati nzuri Kamati imeleta *document,* kwa bahati *document* yangu nimeisahau hapa lakini wameleta ripoti, kuna ripoti nzima ya vielelezo kuna tabu zima la vielelezo lakini ripoti ya Mhe. Waziri imekuja nyepesi imetoa maelezo tu hawana document. Sasa ndio maana hapa haya maamuzi katika hili suala la mwanzo kwa kweli maamuzi ya serikali kwamba serikali inakubaliana na mapendekezo yaliyoletwa na Baraza lako tukufu tayari imeshakuwa hatua za Shirika la Umeme kuliarifu Jeshi la Polisi kuchukua hatua za kufanya uchunguzi wa malalamiko ya wateja na kuweza kulipa fidia.

Sasa hapa Waziri ametwambia tu kwamba serikali au Shirika la Umeme wameshachukulia hatua ya kuwaandikia Jeshi la Polisi kuna kielelezo gani kilicholetwa hapa kikatuthibitishia kwamba Shirika la Umeme tayari wameshaandikia Jeshi la Polisi. Sasa kama sisi tulivyopata tabu ya kutafuta *document* tunaomba serikali kabla ya hoja hii kupitishwa tuletewe hivi vielelezo ili tuvipitie ili tuzithibitishe, kwa sababu sisi kama tulivyosema, mimi ni Mwakilishi wa wananchi inawezekana miongoni mwa hao waliofanya hayo masuala au ukosefu pengine wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura.

Kwa hivyo, bado na mimi nitatetea hatua zozote za kisheria na kinidhamu zitakazochukuliwa na serikali. Sasa hapa tutaiomba serikali watuletee hizi *document* ambazo zilionesha kwamba hawa watu tayari taarifa zao zimeshapelekwa Polisi na Polisi wanatakiwa wafanye uchunguzi.

Lakini vile vile hapa serikali ingelitwambia. Je, vile vielelezo vilivyoletwa na Kamati ya Baraza la Wawakilishi Kamati ya PAC? Je,vilikuwa sio halali? Kwa sababu kama vilikuwa ni halali ina maana hapa tayari huo ni wizi ambao uliokwisha kufanyika. Kwa hivyo, watu hawa moja kwa moja na utaratibu hapa unavyotakiwa alikuwa moja kwa moja asimamishwe kazi ili na huo uchunguzi uweze kufanyika.

Kwa hivyo, katika hoja ya mwanzo Mhe. Mwenyekiti, sikubaliani lakini vile vile hapa tukaambiwa kwamba Shirika la umeme serikali imemuagiza Mhe. Waziri anayeshughulikia sekta ya nishati kuunda kamati ya rufaa ili kushughulikia malalamiko ya wateja. Mheshimiwa sisi hatukuzungumza malalamiko ya wateja, sisi baada ya kamati kwenda ndio ikagundua sio kama tulileteWa malalamiko. Kama wananchi wana malalamiko wao ndio wangelipeleka kwa Waziri au angelipeleka kwa Meneja, sisi baada ya Kamati kwenda kufanya uchunguzi ndio wakagundua kwamba kuna watu wameungiwa umeme katika gharama iliyokuwa kubwa lakini risiti wakapewa kidogo.

Kwa hivyo, ina maana hilo suala kama Waziri ataunda Kamati, Kanuni zinamruhusu huko wache waendelee kufanya sisi hatuna matatizo. Lakini hii Mheshimiwa hii ni hoja kibinafsi, hii ni kesi lazima serikali ichukulie hatua za kinidham au hatua za kisheria kama nilivyosema. Lakini kwa hatua hizi bado mimi sijaridhika na hatua zilizochukuliwa na serikali. Kwa sababu hapa ni upotevu wa fedha za umma.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, katika hoja hii hii huku mbele imeeleza, napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza lako Tukufu ukurasa wa pili katika viambatanisho kwa tayari barua ya onyo imetolewa kwa Meneja Mkuu, hii mimi sina pingamizi nayo kwa sababu hizi ni kanuni ambazo au taratibu za kisheria hazina matatizo. Halafu chini yake hapo inafuata pia serikali imetoa onyo la mwisho kwa maandishi kwa ndugu Ahmed S. Yussuf

kwa vitendo vyake vya kujifanya wakala wa wateja wanaotaka kuungiwa umeme wakati yeye ni mfanyakazi wa Shirika, aidha serikali haitomvumulia mtendaji yeyote wa Shirika atakaekwenda kinyume na taratibu. Mheshimiwa hata hili mimi pia sina pingamizi nalo kwa sababu kwa kuwa ni mtendaji wa serikali ambaye yeye amegeuka sasa akawa ni dalali kwa hilo onyo walilopewa mimi pia sina matatizo nayo.

Lakini jengine hoja namba mbili fedha za malipo kuungiwa umeme katika *account* ya mtendaji wa Shirika Ndugu Zakia Juma Azan hapa ndio kabisa sikubali. Serikali inasema vipi, serikali inakubaliana na pendekezo hilo la kamati, sasa hapa tatizo ndio kama vile nilivyosema, kwamba kamati ilileta mapendekezo ambayo yalikuwa mepesi hatua za kisheria na kinidhamu zichukuliwe dhidi ya muhusika.

Mimi ninafikiri kamati mara nyengine tunapokwenda kufanya kazi tutafute hasa zile kanuni za adhabu na tutaje kifungu ili serikali tuiagize itumie kifungu namba ngapi kwa ajili ya kumwadhibu, lakini hapa sisi tulisema tu serikali wachukuwe hatua za kinidham dhidi ya muhusika. Lakini je tuangalie hii hatua mtumishi huyu fedha za malipo za uungaji wa umeme tena fedha sio kidogo zaidi ya karibu milioni thalathini na saba fedha zimeingia kwenye *account* yake na yeye mwenyewe kahojiwa na kamati amekiri, fedha baada ya kwenda katika *account* ya Shirika zimekwenda kwenye *account* yake.

Mhe. Mwenyekiti huu ni wizi. Leo mtu huyu tumeambiwa amehamishwa kutoka Shirika la Umeme amepelekwa Wizarani. Jamani mwizi anataka aondolewe pahala pamoja apelekwe sehemu nyengine. Kwa kweli huu si uadilifu na hapa mimi ndio maana nikasema nitasimama kwa kofia yangu nikiwa kama mjumbe wa Halmashauri ya Taifa, Mhe. Mwenyekiti Chama chetu hakikubaliani na masuala yoyote ya ubadhirifu, mimi sizungumzi ufisadi maana yake ukizungumza neno ufisadi ufisadi limekwenda mbali zaidi. Chama chetu hakikubaliani na

masuala ya ubadhirifu wa mali za umma, huu ni ubadhirifu wa mali ya umma.

Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana na ninampongeza sana Katibu wetu mwenezi wa CCM Taifa Ndugu Nape Mnauye, amepita katika majukwaa mikoa mbali mbali ya kuzungungumza kwamba Chama cha Mapinduzi kitapambana na mafisadi wote, sasa huku kwetu hakuna mafisadi lakini kuna wabadhirifu wa mali ya umma. Sasa na mimi nikiwa mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ninasimama katika msimamo huo wa kutetea hoja hiyo ya chama changu kwamba pahala popote penye kutokea ubadhirifu lazima nitasimama kwa upande wa chama changu cha Mapinduzi kupiga vita masuala yote yanayohusu ubadhirifu wa mali ya umma.

Sasa hapa vile vile Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe onyo, leo nimesikiliza katika vichwa vya magazeti nadhani kama sikosei mtaniomba radhi vyombo vya habari kwenye magazeti sijui kama Zanzibar Leo au chombo gani kimeeleza kuna Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Kusini Unguja, amesema eti analani anawaasa Wawakilishi wa Chama cha Mapinduzi kuacha mara moja kuisokota serikali ya Chama cha Mapinduzi, yeye katumwa na nani kuingilia mamlaka ya Baraza la Wawakilishi. Mimi naomba sana tena naona aibu sana kwa kiongozi wa Chama cha Mapinduzi tena wa Mkoa tena Mwenyekiti wa Wazazi leo anashindwa kujua hata kanuni za Baraza la Wawakilishi na kanuni zinasemaje. Baraza la Wawakilishi hapa kuna sheria za kinga na fursa huwezi tu ukakaa huko nyumbani kwako
ukaanza kuhoji na kuingilia mamlaka ya huku ndani, huku kuna taratibu maalum za kisheria. Kwa hivyo, naomba sana tena naona aibu sana kwamba Mwenyekiti wangu amepotoka na amepotosha umma.

Sasa na yeye ninamuonya aache mara moja kuingilia masuala ya chombo hiki cha kutunga sheria. Mhe. Mwenyekiti, chombo hiki

kina kinga zake huku tuna Kamati zetu kuna Kamati ya Wawakilishi ya Chama cha Mapinduzi, Mwenyekiti wake ni Makamu wa Pili wa Rais ambaye yeye ni mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi mkubwa kuliko yeye, sasa yeye kwani hasikii tunavyosema. Kama tumekosea tuna *cocus* zetu hapa tunaitana tunaelekezana. Tunaomba sana asutumie kofia kwa kupotosha umma na asikitie aibu Chama cha Mapinduzi, kama na yeye anahusika katika ubadhirifu basi hata na yeye tutamshughulikia.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana hapa ninasema kwamba katika hoja hii namba mbili ya Ndugu huyu aliyetajwa kwa jina katika ukurasa wa 17 kifungu namba 2 hoja namba 2 maamuzi ya serikali kumhamisha kutoka Shirika la Umeme kumpeleka Wizarani sitokubaliana nayo na inaweza ikasababisha nikaja nikaipinga ripoti hii *otherwise* serikali itukubalie kwamba na yeye huyu asimamishwe kazi, Jeshi la Polisi lipewe kazi ya kufanya uchunguzi. Na ninaahidi Kamati ya PAC Wajumbe wapo, *document* tunazo, *account* yake fedha zilizoingia ipo, Jeshi la Polisi tutawapa moja kwa moja wamburuze Mahkamani kwa ajili ya kwenda kujibu hoja na hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna viongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi kuna mzee mmoja anaitwa Peter Kisumu, hivi karibuni nilisoma kwenye mtandao katika vyombo vya habari akatoa onyo kwa Chama cha Mapinduzi na anazungumza kwa upande wa Bara, akasema Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaweza ikaja ikaadhibiwa na wananchi kwa kuvumilia na kufumbia macho mambo ya ubadhirifu wa mali za umma. Sasa yule alikuwa ni miongoni kama sijakosea waliokuwa wadhamini wa chama chetu, mimi naheshimu sana maelezo yake.

Hivyo, mimi naiomba sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiongozwa na Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi tujitahidi sana

tusiwavumilie wabadhirifu wa mali ya umma ili wananchi wasije wakatuadhibu kutuweka tena madarakani. Sasa sisi tukiwa Wawakilishi makini wa Chama cha Mapinduzi kauli zetu ndio hizi tunaendelea kupiga vita ubadhirifu. Kwa hivyo, wananchi muendelee kutupa imani kuturejesha tena Wawakilishi wa Chama cha Mapinduzi ili kuja kulinda serikali yetu isifanyiwe mambo ya ubadhirifu. Kwa hiyo, hoja nambari mbili Mhe. Mwenyekiti, maamuzi ya serikali sikubaliani nayo hata kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja hoja nambari tatu, hoja nambari tatu kuwepo kwa makisio ya aina mbili, huu ndio ule ule wizi. Kwa hivyo, hoja yangu hii naikusanya na hoja nambari moja hao watu lazima kama wako waliofanya mambo kama hayo na kamati imewathibitisha kwanza wasimamishwe kazi halafu baadae uchunguzi ufanyike wapandishwe Mahkamani.

Mhe. Mwenyekiti, ushiriki wa Mohamed Bashir kwa niaba ya *Sana Express,* haya ni mambo ya wafanyabiashara na Shirika la Umeme lina sheria vile vile, kwamba hakuna duka lolote litakaloruhusiwa kuuza vitu vya umeme kama halina kibali. Kwa hivyo, hapa tunawataka Shirika la Umeme wamchukulie hatua mara moja huyu mfanyabiashara anayeuza vifaa ambaye hana leseni ya kuuzia vifaa hivyo au kibali kutoka Shirika la Umeme.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nambari saba inasema Fundi Abeid maarufu Punda, si mfanyakazi wa shirika lakini anafanya kazi za shirika kinyume na taratibu kamati haikupendekeza chochote. Kwa hivyo, Mhe. Waziri kakubaliana na hoja na serikali imelitaka shirika kuwa makini. Kwa hivyo, shirika mimi nafikiri Meneja Mkuu ameshasikia azidi kuwa makini vyenginevyo basi kama wameshapewa maonyo, nafikiri kama hawajachukulia hatua mambo kama haya madogo madogo yanaweza yakawaharibia mambo yao.

Lakini jengine katika hoja nambari nane kuhusu suala la Kampuni ya *GECCO*. Mhe. Mwenyekiti, Kampuni ya *GECCO*

hii kwamba kukiukwa kwa agizo la Bodi ya Wakurugenzi kuhusu mgongano wa maslahi wa Ndugu Hamidu Saidani Ali na Ndugu Ali Abeid Haji wa *ZECO* na *GECCO* ukurasa wa 29 katika ripoti. Kamati imependekeza kutumiwa muda wa kazi kwa kufanya shughuli za kampuni binafsi za *GECCO*. Sasa hapa Mhe. Mwenyekiti, ndio ule ukiukaji wa maadili ya kazi kwamba wewe ni mfanyakazi wa shirika kazi ambazo zilikuwa zifanywe na shirika unazipeleka katika kampuni yako huku Mkurugenzi na huku Mtendaji wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hili si suala zuri, lakini nashukuru nimefurahishwa na maamuzi yaliyofanywa na serikali kwamba, wale moja kwa moja serikali wanasema suala la kuwepo mgongano wa maslahi *conflict of interest* kuhusu baadhi ya wafanyakazi wa *ZECO* na pia kwa wafanyakazi wa kampuni binafsi ya *GECCO* ni jambo ambalo halikubaliki hata kidogo ili kuondoa mgongano wa maslahi, serikali imeshachukua hatua za kuwahamisha wafanyakazi hao na kuwapeleka sehemu nyengine.

Mimi naipongeza sana hatua hiyo ya serikali, lakini serikali isionee wanyonge tu, inapochukua hatua ichukue kwa pande zote. Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti yetu ya mwanzo hapa ya kamati teule ambapo ilipoletwa hapa Barazani, majibu ya serikali hatukukubaliana nayo, wako watendaji wengine wana *conflict of interest*, wamo ndani ya serikali lakini huku wana makampuni yao ndani ya serikali hiyo hiyo tena katika taasisi wanazoziongoza. Sasa leo inakuwaje hawa wanyonge wa Mwenyezi Mungu wameweza kuondoshwa Kampuni ya *ZECO* wakapelekwa sehemu nyengine wale wengine ma-*giant* wanaendelea kubakia.

Mheshimiwa, hili sitokubaliana nalo kwa sababu serikali hapa haitendi haki. Kuna wengine inawatendea haki kuna wengine haiwatendei haki, hapa nasimama kwa miguu miwili nikiwa Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura hapa inaonesha kama itakuwa hatua wamechukuliwa hawa yule mwengine

hakuchukuliwa hatua, nitasema hapa kuna uonevu na hili mimi sitokubali kwa serikali yangu kufanya mambo ya uonevu.

Kwa hivyo, hoja hii nambari nane siikubali na siikubali sio kwa hoja hii, nakubaliana na maamuzi yaliyofanywa na serikali lakini vile vile nataka uetekelezaji huu uendelee katika ile taasisi nyengine tuliyozunguzma katika ripoti iliyopita ambapo Mhe. Mwanasheria Mkuu tumeshamlalamikia sana analijua hilo na Makamu wa Pili wa Rais analijua vile vile. Naamini hatua kama hizi serikali ikichukua na maeneo mengine nafikiri ndio tutakuwa tunakwenda zaidi katika ule utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, watu walioungiwa umeme kinyume na utaratibu huu bado narejea tena ni ule ule wizi. Kwa hivyo, mwizi kwanza kama kahusika katika shirika lazima kwanza asimamishwe kazi, aburuzwe na polisi, apelekwe kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, aburuzwe Mahakamani ikatafutwe sheria inasemaje.

Kwa kumalizia Mhe. Mwenyekiti, ili na wenzangu wapate kuzungumza hizi nyengine ninazoziacha sina matatizo nazo sana, lakini hoja nambari 13 inayosema tofauti na malipo ya kazi yanayofanana kwa wengine na kazi kubwa na malipo madogo katika uungaji wa umeme.

Mhe. Mwenyekiti, hili suala ndio yale yale ninayozungumza, kwa sababu kama shirika mimi najua kuna vigezo vya kuweza kutoza, malipo mbali mbali. Kwa hivyo, ina maana kama hawaingii wamefanyiwa *favour* labda liwe suala la jamii, kama suala la jamii hakuna tatizo, laini kama amefanyiwa mtu binafsi hapa inaonesha itakuwa kuna ujanja ujanja umefanyika. Kwa hiyo, hatua za kisheria na kinidhamu lazima zichukuliwe. Na waliohusika na masuala hayo mimi bado napendekeza wasimamiswe kazi kama *GO* zinavyosema ufanyike uchunguzi walipwe nusu mshahara mpaka utakapothibitika aidha

warudishwe kazini au waondolewe kabisa ili kujenga nidhamu katika shirika letu.

Mhe. Mwenyekiti, hapa malipo yaliyolipwa kwa baadhi ya wateja bila ya kupewa risiti kabisa. Hapa Mhe. Mwenyekiti, ndio kabisa sikubaliani napo. Hoja nambari 15 inasema malipo yaliyolipwa na baadhi ya wateja bila hata kupewa risiti Mheshimiwa, huu ndio wizi, huu ndio wizi wa mchana. Serikali malipo yake yote lazima upewe stakabadhi.Kwa hivyo, ina maana hawa malipo wamefanya na kwenye kamati wameeleza malipo yale fedha wamepeleka kwa nani, mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, hatua za kisheria hapa ni moja tu ni kufuata *GO*, kusimamishwa kazi, hawa wapelekewe polisi majalada kuwafikisha Mahakamani.

Lakini huku serikali jawabu yake iliyotoa eti inasema serikali imetaka Shirika la Umeme litoe elimu kwa wananchi kwamba kamwe wasikubali kulipa pesa mkononi kwa mtu yeyote kwa ajili ya kupata huduma ya umeme. Ah! Suala la kutoa elimu ni kazi yao, Shirika la Umeme ni kazi yao, tena mimi nawaona katika vipindi mbali mbali vya redio, televisheni tunawasikia wanatoa elimu lakini hapa kuna wafanyakazi ambao si waadilifu wametumia utumishi wao wa umma vibaya na hawa maarufu kule Bara wanaitwa vishoka. Kwa sababu wako wengi hawa hata kule Bara wapo wanawaungia watu umeme ambapo huku malipo hayendi serikalini. Kwa hiyo, hapa sikubaliani na hoja ya serikali. Hivyo, tunataka moja kwa moja hawa waliohusika na kadhia hii ambapo ripoti ya kamati imewataja.

Mhe. Mwenyekiti (Mgeni Hassan Juma): Mhe. Mjumbe umebakiwa na dakika nne malizia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sawa naheshimu sana dakika zangu nitajitahidi nimalizie. Kwa hivyo, hapa vile vile sikubaliani na maamuzi ya serikali ya kusema kwamba Shirika la

Umeme litoe elimu wakati kuna pesa zimeshaingia mfukoni mwa watu.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ambayo nataka niizungumze ni hoja nambari 19 inayosema, shirika kuendelea kuiruhusu *GECCO* kufanya biashara ya *transformer* wakati kuna agizo la Bodi ya Wakurugenzi bila ya kibali. Mimi nafikiri hili tayari kwa kuwa kuna onyo limeshatoka na maamuzi ya Bodi yanatakiwa lazima yaheshimiwe.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nambari 20 ukurasa wa tisa inasema, upotevu wa kumbukumbu za wateja Ras Kichanga ukurasa wa 35 na 36, kuroa kwa mafaili 147, Mheshimiwa huu ndio wizi, huu ndio wizi dhahiri. Leo mafaili yameroa jamani Shirika la Umeme linavuja lile, mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, hawa waliofanya kadhia hii wasimamishwe mara moja wapelekewe Kamishna wa Polisi ili kuwachukulia hatua za kisheria. Kwa hivyo, ndio maana
nikasema kuna baadhi ya mambo ya serikali waliyoyafanya nimeyapongeza lakini mengi yao sikuyapongeza kwa sababu maamuzi waliyoyafanya kwa kweli hayaendani hata na hizo *GO* zinavyosema.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, hoja nambari 21 kutochukuliwa hatua za kisheria zidi ya *Residence Hotel* ambayo ilivuta umeme huku serikali ilibaini kuwa kazi ya uungaji wa umeme katika hoteli hiyo imefanywa na *ZECO* na kamapuni ya *CRJE,* imelipa *ZECO* gharama za kazi ya uungaji wa *labour charge* na Kampuni ya *GECCO* imeiuzia Kampuni ya *CRJE* vifaa vya umeme vilivyotumika katika kazi hiyo.

Sasa Mheshimiwa, kama sisi tumejenga hoja hapa kumekiukwa taratibu na *document* zipo, serikali na wao wangelituletea *document* zinazohalalisha kile kilichofanyika, lakini serikali imetuletea maneno tu hakuna *document* yoyote. Sasa leo hata Mahakamani mwenye *document* na aliyekuwa hana *document*

nani ataaminiwa, nani atapata haki. Sisi itabidi leo tupate haki mpaka serikali itakapoleta *document* zake za kufuta zile hoja zilizoletwa na kamati.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kuungwa umeme Kendwa na *Leisure Hotel* bila ya kufuata utaratibu, serikali imelitaka Shirika la Umeme kuhakikisha kwamba linahakiki wateja wake wote. Mimi nafikiri hapa kuna uchunguzi uliofanywa na kamati, mimi nafikiri bado na huo pia apelekewe Kamishna wa Jeshi la Polisi ili kuweza kuyafanyia kazi masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, kushindwa kuthibitishwa zimenunuliwa nguzo za *transformer* zilizotumika katika nyumba ya kupumzikia binti aliyetajwa. Hapa serikali wamesema ilifanya ukaguzi wa eneo linalohusika na hoja hii na kubaini kwamba nguzo zilizotumika na kupelekwa umeme huo zilikuwa ni 20 na Shirika la Umeme ndio lililopeleka nguzo hizo. Aidha serikali ilipeleka umeme kwa kuelewa kwamba eneo hilo ni la uwekezaji kwani tayari kuna hoteli mbili. Wakati ripoti ya kamati inasema kuna nyumba tu ya mtu ya kupumzikia, serikali inatwambia kuna hoteli mbili. Sasa mimi Mhe. Mwenyekiti, naweza sasa nikaja nikatumia kanuni ya kuahirisha hoja hii mpaka twende tukakague Baraza zima. Kwa sababu kamati inatwambia vyengine na serikali inatwambia vyengine, kamati inasema kuna nyumba ya mtu mmoja tu, serikali inatwambia kuna hoteli mbili tukathibitishe. Mheshimiwa, ziko kesi zinakwenda mpaka kuhukumiwa hospitali ili kuthibitisha. Sasa na hili Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti (Mgeni Hassan Juma): Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sawa naomba dakika mbili nimalizie Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu baadae nataka aidha niseme naunga mkono hoja au siikubali hoja. Mhe. Mwenyekiti,

kwa kumalizia mimi naomba sana hasa katika suala la fedha kuingia katika mtu binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili kwa serikalini ni suala la kawaida, katika ripoti iliyopita ya Baraza la Manispaa kuna mtu sitaki kumtaja jina katika ripoti itakuja kuelezwa, fedha ziliingizwa kwenye *account* yake mara mbili za mtu binafsi tukaambiwa imekosewa, imekosewa mara ya kwanza, ikakosewa na mara ya pili. Bado narejea tena kusema *account* lazima iwe na nambari ya *account* na jina la mtu hapa pamefanywa kwa makusudi, huu ni ubadhirifu wa mali ya umma, hawa watu lazima wafikishwe polisi.

Vile vile, sio kufikishwa polisi tu, naomba fedha zote zilizoingia mifukoni kwa watu, naomba tuamue Baraza hili zirejeshwe serikalini hatua nyengine za kisheria zichukuliwe na hili alilifanya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika fedha za *EPA* alijua wezi wakienda Mahakamani hawafungwi kwa sababu wajanja wanajua namna ya kubabaisha kesi ya *EPA* mpaka leo hakufungwa mtu. Lakini Mhe. Rais aliwaambia vipi, aa mimi nataka hizo pesa zilizoibiwa zirudishwe mbona pesa zilirudishwa. Kwa hivyo, serikali imerejeshewa pesa zake sheria huko tena watachukua mkondo wao wamewachukulia hatua, hawakuwachukulia hatua lakini fedha za umma zirejeshwe. Kwa hivyo, hapa naomba fedha zote zilizoingia mifukoni kwa watu zirudi ndio tutakubali kupitisha sheria.

Mhe. Mwenyekiti, nasubiri maelezo ya serikali nikikubaliana nayo nitaunga mkono hoja, lakini kama sijakubaliana nayo sitoweza kuunga mkono hoja hii. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuamka wazima na salama na hatimaye tukaweza

kuwa pamoja hapa kuendelea na harakati zetu na mipango yetu ya kimaendeleo ambayo tumejipangia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nachukua fursa hii vile vile kuishukuru serikali pamoja na wajumbe wenzangu wote wa Baraza hili kwa kuletewa hoja hii na tukaweza kuichangia kwa kadiri ambavyo kila mmoja amehisi anapaswa kufanya hivyo. Kwa upande wangu Mhe. Mwenyekiti, mimi nimejaribu kuipitia hii hoja ambayo imewasilishwa hapa ikiwa ni majibu baada ya ile ripoti ya *PAC* ambayo iliwasilishwa hapa na kamati inayohusika.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ambayo imeletwa mbele yetu ina vifungu 38 nimejaribu kwenda ndani na nimejaribu kusikiliza kwa kina michango ya Wajumbe mbali mbali ambao walipata fursa ya kuchangia katika taarifa hii ambayo imewasilishwa kwetu hapa. Mimi kwa upande wangu nahisi kuna mvutano mdogo tu ambao unaendelea kujitokeza baina ya *back benchers* na wale watu wa Serikali Kuu ambao wako mbele. Lakini inaonekana sote tuna mwelekeo mmoja tukiwa na malengo ya kujenga nchi yetu na kupata maendeleo kwa maslahi ya nchi yetu na watu wetu kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mtazamo wangu baada ya kwishakusikiliza hoja za Wajumbe wenzangu pamoja na kuisoma hii ripoti, ninachokiona ni kwamba namna ya uchukuaji wa hatua ambazo zimechukuliwa baada ya ripoti hii kwishakupatikana hadi kurejeshewa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ndipo pahala ambapo panagonga. Sasa jambo la msingi ninaloliomba mimi ni serikali kuichukua tena hoja hii kwenda kuhakikisha kwamba yale mambo ambayo yanataka hatua za kiutawala na za kisera zifanywe kwa utaratibu ambao sheria na taratibu ambazo tumeziweka zinatutaka tufanye hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimejaribu kwenda sana katika haya mambo ambayo yalizungumzwa humu kwa mfano niliangalia

katika ukurasa wa nne katika eneo ambalo linahusu naomba kunukukuu.

Kifungu 44 cha Sheria ya Shirika la Umeme Nam. 3 ya mwaka 2006 kinasema kwamba:

> "Serikali imemuagiza Waziri anayehusika na Sekta ya Nishati kuunda kamati ya rufaa".

Haya ni mambo ambayo yanahusu utawala ndani ya ofisi inayohusika. Ni suala la msingi sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tumpe nafasi waziri anayehusika kwa sababu waziri ni mpya katika wizara hii aende akafanye hii kazi kwa ufanisi unaostahiki ili tuweze kuona sasa mwelekeo wa kazi hii nzuri ambayo tumeitoa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hatma yake na matokeo yake ni nini.

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli ripoti hii nilipokwisha kuipata, mimi ilinipa kazi kubwa sana, pamoja na majukumu yote tuliyonayo lakini nilipata fursa yakukaa na baadhi ya Wajumbe, baadhi ya wananchi ndani ya jimbo langu kwa kupata maoni yao kila namna. Kwa bahati nzuri asilimia 55 ya wananchi katika jimbo langu ambapo kundi hili linaongozwa na wazee, wao walikuwa na mwelekeo wa kukubaliana na ripoti hii lakini hatua zizidi kuchukuliwa zaidi. Lakini asilimia 45 ya watu ambao nilikaa nao wao wanasema kwamba ripoti hii ina matatizo na watu wachukuliwe hatua na haya maelekezo ambayo yalitolewa hawajakubaliana nayo. Hawa watu kwa upande wangu wana haki zao za msingi na mimi ni kiongozi ambaye nawasimamia wao na niko humu kwa ajili ya kuwatetea na kuendeleza mambo kwa ajili ya kufuata maslahi ya nchi yetu.

Sasa mimi kwa upande wangu naona kwamba tujitahidi tuhakikishe kwamba haya masuala yaliyozungumzwa humu ni masuala mazito na masuala ambayo yamekuja yakiwa na vielelezo, yakiwa na mwelekeo ambao wananchi pamoja na

viongozi ambao wako humu wanataka kuona kwamba serikali yao inafuata taratibu za kulinda misingi ya sheria na kanuni kuhakikisha kwamba hatua za kinidhamu kila panapojiri zinachukuliwa na watu wanawajibika kwa kadiri haki na wajibu unavyotuelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikiwa naendelea mbele zaidi katika hoja hizi kuna mambo ambayo vile vile nataka kupata ufafanuzi zaidi hususan hapa pahala tunapokuta kuwa tunakubaliana na hoja ya Baraza lako tukufu kuwa Fundi Ali Abeid Mohamed si mfanyakazi wa Shirika la Umeme. Sasa mtu keshajulikana kuwa si mfanyakazi wa Shirika lakini hapo hapo wanatakiwa polisi wakafanye uchunguzi wa kina zaidi ya vielelezo ambavyo vimekwishakutolewa ni uchunguzi gani tena wa kina unatakiwa kwenda kufanyika hapa. Mimi ningeliomba katika hatua kama hivi na vielelezo vilivyothibitishwa na kuwasilishwa wale watu ambao wanahusika wakachukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu ambazo zinapaswa.

Lakini vile vile kuna maelezo katika eneo la namna ya utoaji wa *tender* kwa kampuni ambayo ilikuwa imeshinda na kampuni ambayo ilikuwa imeshindwa, ningeliomba serikali iweze kutimiza yale mambo ambayo taratibu halisi zinatakiwa tuzifuate. Mtu ambaye ameshinda akubalike kupewa na aweze kuendelea na taratibu zinazohusika.

Mhe. Mwenyekiti, wengi wamekwishakuchangia hii ripoti na sipendi na mimi kuwa nazungumza kwa kurejea rejea mle kwa mle wakati watu wameshazungumza na wamekwishaelekeza nini cha kufanywa. Kwa upande wangu naiomba serikali ikubali kuchukua maoni ya Wajumbe ambayo tayari yamekwishawasilishwa na wakazidi kwenda kutafakari zaidi na kulifanyia kazi suala hili na tuhakikishe kwamba maamuzi na utaratibu mzuri unatengenezwa kuona kwamba haya mambo yanayohusu sheria yanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria, yanayohusu utawala yanashughulikiwa kwa mujibu wa utawala

na yale ambayo yanahusu kuwawajibisha watu basi wawajibishwe ili amani na maendeleo ya nchi yetu yaweze kupatikana kwa mujibu wa taratibu tunazojiwekea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda nifikie hapo katika maelezo yangu hususan ukitilia maanani kwamba mimi ni mmoja kati ya walezi na wachunga katika taasisi hii. Waswahili wana msemo wanasema kwamba, "Hakuna ng'ombe anayeelemewa na nundu yake". Nikiwa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, ninachoweza kuahidi hapa tutahakikisha haya mambo yote ambayo yamezungumzwa humu mimi pamoja na Wajumbe wenzangu wa Kamati nitakwenda kuyasimamia tuhakikishe kwamba yanafanyiwa utaratibu na yanatekelezwa kwa mujibu wa taratibu na sheria tulizojiwekea.

Baada ya maelekezo hayo, naomba kusita hapo nasema nashukuru sana kwa kunioa fursa hii ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia kidogo katika taarifa hii ambayo imeletwa na serikali. Mhe. Mwenyekiti, napenda kwanza nizungumzie suala zima la wajibu wetu sisi kama ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, wajibu wetu uko katika kifungu nambari 5(a) cha Katiba ya Zanzibar na kinasema kwamba:

> "…Wajibu wetu ni kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma……."

Huo ndio wajibu mkubwa wa shughuli zetu. Lakini katika kifungu hicho hicho kinaelezea suala la mgawanyo wa madaraka baina ya vyombo vitatu hivi vikubwa vya serikali; kwanza Baraza la Wawakilishi, pili Serikali na tatu Mahakama. Sasa katika mgawanyo huo wa madaraka Mhe. Mwenyekiti, naomba sana nimshukuru Mhe. Salmin Awadh Salmin wakati alipokuwa

akichangia bajeti yangu katika hotuba yake Mhe. Salmin Awadh Salmin alisema kwamba anahofia na asingelipenda chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi kikawa kama ni Mahakama, akasema kwamba nilizungumzia juu ya Baraza hili watu kulinasibisha na Mahakama na kwa hiyo chombo hiki kisionekane kwamba ni Mahakama. Haya ni maneno ya Mhe. Salmin Awadh Salmin wakati wa kuchangia hotuba yangu ya bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, huu ni usemi ambao ni wa ukweli na wa uhakika kabisa, kwamba chombo hiki hakitakiwi kiwe kama Mahakama, chombo hiki kinavyotakiwa ni kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Kwa maana hiyo, Mhe. Mwenyekiti, katika shughuli hizi kuna mambo ambayo lazima Baraza la Wawakilishi yaelekeze kwa serikali na kuna mambo serikali lazima iyachukue na iyafanyie kazi. Lakini katika hayo mambo ambayo serikali inayafanyia kazi sote tunajua kwamba kuna mambo ambayo lazima tuyatizame na hayo ni kutokana na ule utaratibu wa ahadi zetu na viapo vyetu ambavyo tulikula, ni kwamba tutailinda katiba na sheria zilizopo, na maamuzi yetu yote yatafuata katiba na sheria.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili, mimi nafikiri kuna mambo manne lazima tuyatizame. Kwanza tutizame katiba inasema nini halafu tutizame sheria nyengine zilizopo ambazo zinatawala mambo haya na sheria hizi kwa mfano sheria nambari 2 ya mwaka 2011 Sheria ya Utumishi. Halafu kuna sheria ya Afisi ya Mwendesha Mashtaka (*DPP*) Sheria nambari 2 ya mwaka 2010.Vile vile, kuna sheria nambari 4 ya mwaka 2007, Sheria inayohusiana na *privileges* na *immunities* za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Sasa hizi zote Mhe. Mwenyekiti, ndizo sheria ambazo zinatuongoza katika kutoa maamuzi ya mambo yote ambayo yanaletwa katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 19(3) cha Sheria ya *privileges and immunities* za Baraza la Wawakilishi inasema hivi naomba ninukuu.

Kifungu cha 19(3) kinasema kwamba:

"An answer by a person to a question put by the House or Committee shall not except in the case of criminal proceedings under section 91,95,97 and 98 of the Penal Act or of an offence against this Act, be in any proceedings civil or criminal admissible in evidence against him".

Hii inaonesha kwamba mambo yote yale ambayo yanakusanywa na kamati yako au kamati zako katika uchunguzi fulani, basi mambo yale yanayokusanywa hayatokubaliwa katika uendeshaji wa kesi Mahakamani. Kwa maana hiyo, chochote ambacho Baraza litapendekeza, lazima kuwe kuna nafasi ya serikali kufanya uchunguzi mpya kwa mujibu wa sheria nyengine ambazo zimewekwa, na hapa Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba katika kifungu cha Sheria ya Muendesha mashtaka yaani *DPP* sheria namba 2 ya mwaka 2010. Kifungu cha 9 kinasema hivi naomba ninukuu:-

> "Kifungu hichi kinampa uwezo muendesha mashtaka yaani *DPP* kutoa *directive* kwa polisi kwamba kitu falani kilichopelekwa mbele yake kifanyiwe uchunguzi na pale polisi ambapo unafanya uchunguzi basi baadae anatakiwa akirejeshe tena kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ili aweze kutizama na kutoa uamuzi kama kweli uchunguzi ule umefanywa kwa mujibu wa utaratibu au laa na anaweza tena akarejesha"

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ninavyotaka kusema kwa kusema hayo ni kwamba mambo yote ambayo yanaelekezwa hapa haiwezi tu serikali kwa mfano kama mtu ameonekana na kosa fulani tukasema huyu apelekwe Mahakamani na akapelekwa Mahakamni lazima tufate utaratibu. Vyenginevyo tukienda kinyume na utaatibu ambao umewekwa kisheria basi

tunatoa mwanya kwa yule ambae amepelekwa Mahamakani atashinda kesi na baadae kulipwa mapesa chungu nzima na hilo litakuja suala jengine la kuja kulaumiana hapa Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hayo ndio tukasema kwamba hayo yote ambayo yameelekezwa na kamati yako basi tunafanyakazi kwa misingi hiyo. Yaani kwanza yanakuja halafu yanapelekwa polisi kwa kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu yachunguzwe tena hasa ukitilia maanani kwamba yale ambayo yalitoka huku hayakubaliwi Mahakamani. Na hii ni sheria mbayo sisi wenyewe tuliipitisha hapa. Kwa hivyo, lazima kuwe na uchunguzi na kama kweli unataka kupeleka kesi yako Mahakamani.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hilo ni la kwanza ambalo lingelipenda Waheshimiwa Wajumbe wakalifahamu na wakalizingatia. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ukitizama sheria ya *Public service Act nom 2* ya mwaka 2011. Sheria ile inaeleza katika sehemu ya 7 kuanzia kifungu cha 81 mpaka kifungu cha 92. Hichi kinasema:-

> "Ule utaratibu wa kuzishughulikia zile adhabu ambazo zinatolewa, kuna utaratibu wake ambao umewekwa na utaratibu huo inatupasa sisi serikali kuufuata"

Kwa sababu kama mfanyakazi anashitakiwa au ameshitakiwa kwa kitu fulani na unapopata jukumu lile huwezi moja kwa moja ukachukua hatua kinyume na ule utaratibu ambao uliowekwa chini ya sheria hiyo. Kwa hiyo, ndio kazi moja kubwa ya serikali kutizama kwamba mfanyakazi yule hata kama tunamchukia kiasi gani lakini tunakwenda kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria. Sheria ambazo sisi katika Baraza la Wawakilishi sote tuliipitisha na tukasema kwamba wafanyakazi katika utoaji wa adhabu basi lazima wapitie katika misingi hiyo.
Kwa hivyo, ndio maana Mhe. Mwenyekiti, katika baadi ya maelezo ambayo yametolewa na serikali tumesema kwamba

haya yanachukuliwa hatua hii kwa mujibu wa sheria hii. Ile ni ku- *conform* na sheria ambazo nimezitaja hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa maana hiyo kwanza tujue kwamba hatuwezi Baraza la Wawakilishi baada ya uchunguzi tukasema moja kwa moja watu wapelekwe Mahakamani lazima lipitie kwa *DPP* na *DPP* ataagiza kwa polisi na polisi watachunguza watakuja tena kwa *DPP* halafu *DPP* ndie ataidhinisha kwamba huyu kweli kwa mujibu wa ushahidi huu anaweza kupelekwa Mahakamani au hawezi kupelekwa Mahamani. Huo ndio utaratibu wa kufuatwa na hivyo ndivyo tulivyofanya katika ripoti hii.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 56 (a) cha Katiba lazima *DPP* atoe maamuzi yake kutokana na uchunguzi ambao umefanywa na polisi na yeye kwa sheria ile ya *DPP* niliyoitaja ya mwaka 2010 chini ya kifungu cha 9 lazima atoe ripoti hizo kwa polisi. Hayo ndio yatatufanya sisi mfanyakazi yule kumpeleka Mahakamani na hata tukimpeleka Mahakani kwa utaratibu huo yeye hawezi tena kuja kushtaki serikali kwamba utaratibu ule umekiukwa. Vyengine tukienda kinyume na hayo atakuwa na mwanya wa kuja kuishitaki serikali kwamba kwa utaratibu wote kwa mujibu wa sheria imekiukwa na atadai fedha na fedha hizo atalipwa halafu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunaweza tukasema kwamba labda uchunguzi haujafanywa au kuna makosa kama haya. Kwa hivyo, ninachoomba ni lazima tufate utaratibu kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, baada ya kupata ripoti kutoka kwa Kamati Teule kuna watu ambao wametajwa na watu hao walitajwa kwa mujibu wa taratibu vile vile lazima watu hawa waitwe kwa sababu kisheria kuna zile *principle* za *natural justice* na hizi ni tatu.

Kwanza ni *Right of being part* lazima yule mtu kabla hujampa adhabu au hujachukua hatua yoyote aitwe ili atoe maelezo yake na hilo ndilo lililofanywa. Sasa katika kumwita kuna mambo mengi ambao yanajitokeza na yakijitokeza basi hapo ndio wewe utapata nafasi nzuri ya kuamua kama hili ni kosa au hili si kosa au kosa hili limekwenda wapi na wapi. Na hayo ndio serikali yaliyafanya.

Kwa hivyo, hata huyu mshitakiwa hawezi kwenda Mahakamani kusema kwamba hakupata nafasi ya kusikilizwa au hakupata nafasi ya kutoa maoni yake. Hayo yote tumeyazingatia na ndio maana tukafika katika *stage* hii.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, ni suala limezungumzwa hapa kwamba mfanyakazi mmoja ambae alitoa maelezo kwa kamati aliondolewa pale akapelekwa sehemu nyengine. Hii Mhe. Waziri wa Maji anaweza akaelezea vizuri. Lakini mimi nataka kusema *experience* moja ambayo tumeipata Mhe. Mwenyekiti, huko nyuma tulijiwa sisi na mfanyakazi mmoja akatoa ripoti kwamba wasafirishaji wa karafuu wako katika maeneo fulani.

Tukaona kuwa yule mtu mzuri sana, mfanyakazi huyu akasema wasafirishaji karafuu wako maeneo fulani, kwa hivyo sisi tupeleke nguvu zetu katika maeneo yale. Bahati mbaya Mhe. Mwenyekiti, mfanyakazi huyu alifanya vile ili na yeye kupata nafasi kufanya mambo mengine. Kumbe alitaka nguvu zile zilipelekwe kule na huku yeye kumbe anafanya mambo kama hayo.

Sasa ndio hawa kina kaduara, Kaduara alikuja kwa kamati akasema lakini kumbe yeye ana mambo mengine hayo ambao yanafanywa. Kwa hivyo, wasione kwamba amechukuliwa hatua Kaduara kwa sababu yeye tu kawa ni mtoaji habari nzuri wa kamati na kwamba hana kosa, Kaduara ana makosa mengi kwanza ni mwizi aliiba milioni mbili. Pili hizo gari ambazo ziliuzwa bila ya idhini yeye wakati ni Afisa wa Utumishi ndie

aliezinunua kwa nguvu zake. Sasa haya yote aliyafanya yeye kutaka kujificha na ndio baada ya kumwita hapa kupata hiyo *Right of being part* kwa watu wengine tutapata ushahidi kama huo.

Kwa hivyo, kutokana na hayo ndio akapewa adhabu hiyo ndio tukasema kwamba kuna mambo mengine hayo yamepelekwa polisi hayo hayo ya Kaduara katika huo wizi uuzaji wa magari na mambo kama hayo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, si kwamba serikali imemuonea Kaduara, serikali imefanya jukumu lake na imefanya haki katika kuwatizama wachunguzi hawa au wafanyabiashara hawa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo lilizungumzwa ambalo nahisi kisheria nilizungumze ni kwamba Mhe. Waziri Mohammed Aboud Mohammed alitoa pendekezo la kusema kwamba yule mtoa hoja katika mambo kama haya sasa anapendekeza kwamba asiwemo katika kamati na baadhi ya Wajumbe wakasema haiwezekani. Lakini kitu ambacho kimetufanya sisi tuseme hivyo serikali ni kwamba kwa misingi hiyo hiyo ya *natural justice*.

Natural justice kuna mambo ambayo inatakiwa. Kwanza usiwe *biased* na ukiwa wewe ndio uliotoa hoja kwamba kuna matatizo katika chombo fulani kwa hivyo hata ukifanywa kwamba wewe ni Mjumbe wa Kamati ile kwa hivyo wewe utakuwa uko *biased*. Sasa kwa nini wewe usikae nje wakaachiwa watu wengine kwenda kutizama na kuchunguza yale mambo ambayo wewe mwenyewe umesema kwamba yapo. Kwa hivyo, ndio ile *Princeple* ya *natural justice* inavyo *apply*.

Kwa hivyo, mimi nashauri sana kwamba suala hili ambalo limependekezwa kwamba mtu ambae anatoa hoja katika jambo fulani yule hawezi kuwa Mjumbe au hata Mwenyekiti katika kamati ile kwa sababu bado atakuwa ni *biased*. Kwa sababu yeye atataka ku- *prove* tu kwamba hoja ile aliyoitoa ni ya uhakika. Na

hiyo haitokwenda vizuri. Kwa hivyo, vizuri kwamba mtu kama huyo abakie nje.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachotaka kusema katika misingi hiyo ya sheria tuitizameni. Tutizameni sheria ya *Public Service Act* tutizameni sheria ya *DPP* na tuzizameni sheria ya *immunity* ambazo zote hizi zinatufanya kwamba huu utaratibu ambao serikali imeufanya kwa kupitia ndio utaratibu mzuri na ndio utaratibu wa Utawala Bora.Vyenginevyo tukikurupuka tu basi tunaweza yule mfanyakazi akaja baadae akashitaki kwamba misingi ya sheria hizi haikufatwa na baadae serikali hiyo hiyo mlipe kwa kutokufata misingi ile.

Mhe. Mwenyekiti, hivi ndio tulivyofanya na nafikiri huu ndio utaratibu mzuri na naomba kuunga mkono hoja. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi kuchangia katika waraka huu muhimu.

Baada ya kukushurukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, saa naomba kutoa nafasi hii kuwafahamisha Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi kwa jumla. Kwamba serikali imepokea waraka huu kwa mikono miwili na uliufanyiakazi kiasi cha kutosha kwa kuusoma waraka huu kwa uzuri kabasi na kuufanyia kazi kwa muda wote huo ambao tuliokuwa tukiufanyia kazi.
Shirika la Umeme *ZECO* ni Shirika muhimu sana kiuchumi Zanzibar. Shirika hili linafanya kazi nyingi sana na kwa kweli kazi zake ni muhimu kwa maendeleo ya nchi hii kiuchumi na kibiashara. Na ndio maana serikali ilichukuwa muda mrefu sana kutafakari kuangalia hoja moja moja ambapo kwa kweli tumekuwa na thamani kubwa sana. Kamati hii tunaipongeza sana imefanya kazi nzuri na sisi tunasema kwamba hatuna la kuwalipa wamefanyaka kazi nzuri sana.

Lakini inaonesha kwamba katika michango yao Waheshimiwa Wawakilishi wanahisi kwamba sisi ile ripoti leo tumeiangalia kwa uhafifu hafifu.

Lakini ningetaka kusema kwamba si Baraza la Wawakilishi wala si serikali ambapo kwamba itaweza kutoa hukumu ya wale washutumiwa isipokuwa Mahakama. Serikali haimlindi mtu katika suala hili, serikali haimpendelei mtu. Lakini serikali haitaki kumuonea mtu katika suala hili. Serikali haimuonei haya mtu wala serikali haina utashi wowote kwa chochote na kwa yeyote yule.

Serikali inataka haki itendeke kwa kufata Katiba, Sheria na kila mtu apewe haki yake bila ya kumpendelea yeyote wala kumuonea yeyote. Kama tulivyoambiwa kwenye semina iliyofanyika kule Diamond kwamba ushahidi wa *PAC* au ushahidi utakaotoka popote pale katika Baraza la Wawakilishi hauwezi kutumika kama ni ushahidi Mahakamani.

Ushahidi wa *PAC* na ushahidi uliotoka hapa ni viashirio tu vya ile shutuma ilioko katika *ZECO*. Lakini ushahidi ule hauwezi kuingia vyombo vya Mahakama na kumtia mtu hatiani. Kwa hivyo, lazima sheria ifuatwe watuhumiwa wote wafikishwe katika vyombo vinavyohusika wafike polisi kwa *DPP* na Mahakamani na Mahakama ndio itakayotoa hukumu ya suala hili.

Sasa baadhi ya Wawakilishi hapa michango yao imeonesha dhahiri kwamba wanataka sisi hapa Barazani tuwe mahakimu wa kuhukumu wale washukiwa. Ningeomba dhana hii tuiondoshe kabisa kwamba sisi hatuna jukumu hilo la kutoa hukumu juu ya wale walioshutumiwa. Washutumiwa tuwapeleke katika vyombo vya sheria wachukuliwe hatua za kisheria kama inavyohitajia.

Kwa upande wa serikali, sisi tunatumia Sheria ya Kazi namba 2 ya mwaka 2011 na mapendekezo mengi sana kwa sababu ndugu

zetu katika Kamati ya *PAC* walituletea hoja 13 tuzijibu. Baada ya kusoma waraka ule tumetoa hoja 36 takribani tumezijibu kwa kuona umuhimu wa suala hili.

Kwa hivyo, mimi nataka kuwaambia kwamba ndugu zangu Wawakilishi tusifanye jazba kwenye suala hili. Mimi nawaelewa mnavyoumia na mimi nilikuwa mfanyabiashara hivyo hivyo na katika biashara zangu hivyo hivyo naibiwa na nahujumiwa tena sana tu na nikakamata wezi wangu na nikawapeleka mpaka Mahakamani tena nikawa mkali sana na kesi nikazisimamia kuona kwamba haki itendeke.

Lakini usifikiri vile ninavyotaka mimi ndio watakavyohukumiwa wale. Lazima upelelezi ufanyike, ushahidi upatikane atiwe mtu hatiani halafu ahukumiwe. Kuna kesi moja Mhe. Mwenyekiti, mimi niliibiwa karibu milioni 36. Sasa ile kesi ilikwenda na baada yake mimi nikaambiwa nilipe milioni kumi na mbili, mimi nilieibiwa nilipe milioni kumi na mbili. Hizo ndio kesi jamani unatumia jazba na ushahidi wa kutosha huna unatumia nguvu mwisho,inafika kesi Mahakamani hakuna vielelezo vya kumtia hatiani yule ulie mshutumu. Baada yake unaonekana wewe uliepeleka kesi ile ndio mkosa unaambiwa wewe ndie ulipe na nilizilipa.

Hiyo kesi si mtu fulani bwana ni yangu mwenyewe na kesi nyingi nyenginezo. Wala usione ajabu leo kwamba Kaduara yeye ndio shahidi wetu mbona katiwa kwenye kundi la uhalifu mambo haya vipi. Mambo haya hayakuanza leo tangu enzi za jadi. Iko nyimbo moja ya Siti Bint Saad. Siti Bint Saad ana nyimbo yake ya Kijiti kinasema hivi:

Mambo haya ni ajabu kila tukiyatizama
Kijiti kaua mtu na Tumboni mna mwana
Kijiti kavuka Mto Mashahidi wamezama
Jaji amekasirika kitini alipoketi
Kasema blali fuli mashahidi wa Kijiti

Kwa hivyo, usione ajabu leo Kaduara kaingia ndani ya kesi, hayo ndio masuala ya kesi na haya ndio masuala ya kutafuta *justice*. Kwa hivyo, ningewaomba ndugu zangu Wawakilishi mawazo yenu mazuri sana na naelewa kwamba mna uchungu mkubwa sana mna uchungu wa nchi yenu mna uchungu wa mali ya serikali.

Lakini jazba haitotufikisha pahali pazuri kwa kuweza kutatua tatizo hilo na *ZECO* ni shirika muhimu kwa uchumi wa Zanzibar na shirika muhimu kwa wawekezaji wa Zanzibar. Kwa hivyo, lazima tutumie njia sahihi za kuweza kuwachukulia hatua wale wote waliohusika kwa njia moja au nyengine katika suala hili.

Katika mwaka 2010 Mhe. Mwenyekiti, palitokea *crash* kubwa umeme haukupatikana katika nchi yetu. Nchi yetu ilihangaika kweli kweli watalii walikuwa wengi hawakuja nchini mahoteli yakapata hasara kubwa sana hivi viwanda vichache vilipata tabu sana na serikali ilijitahidi sana kutafuta njia ya kuweza ku-*risque* ile hali halisi ilivyo.

Katika ku- *risque* hali ile wafadhili walijitokeza wakaleta majenereta yale yaliokuja. Imo hoja hapa ya majenereta mwenyewe ataeleza Mhe. Waziri. Lakini ninavyojua majenereta sio majenereta tunayoyakusudia hapa tunayozungumza sisi hapa.

Kuna jenereta za aina mbili kuna genereta za *emergence* na kuna genereta za *stand by. Stand by generators* zinakuwa ni *emergence and ecomonic*. Hayo yalioko kituoni 32 ni genereta za *emergence*, sio genefreta za *stand by*. Na ndio maana wafadhili wale walipoleta pesa zile hawakutia serikalini walitia *consultant* wao wenyewe wakaja watu wakatathmini na wakatangaza tenda wenyewe wakanunua majenereta wenyewe wakayaacha pale na sisi tukasaidia kuya-*fix* majenereta yale.

Baada ya kufanyika kazi hiyo katika mkataba wao ule baada ya kupata umeme wa kutosha Zanzibar kutoka katika ile *MCC* Dar es Salam ilibidi serikali ikae na wafadhili wale kutafuta mustakbali wa majenereta yale kwa sababu yale ni *emergence*, just cut for crises ikitokezea sio *stand by generators*.

Mimi nilitaka kuelezea hayo kwamba tusije tukaji- *confuse* na ushahidi upo kwamba mambo yalifanyika na wenyewe wale wafadhili katika ripoti zao za fedha hazikuonesha kwamba kuna ubadhirifu wowote. Sasa sisi tusijiingize katika matatizo makubwa sana tukadhani kwamba kuna pesa zililiwa. Pale wafadhili wenyewe waliingia wenyewe na wakafanyakazi wenyewe na wakatia watu wao wa kushughulikia shughuli ile na majenereta yale ni majenereta ya *emergence not stand by uneconomical*.

Kwa hivyo, Waheshimiwa tusaidiane suala hili serikali haikufanya hatua mnazotaka nyie zifanywe kwa sababu mngekosea sana na hii ni serikali jamani. Inaiambia serikali ichukuwe *document* kutoka wizarani na *file* zake zote ziletwe Baraza la Wawakilishi huu kweli ndio utaratibu tuliojipangia humu ndani?

Document serikali kuja Baraza la Wawakilishi si kuna taratibu zake tulizokubaliana. Kwa hivyo, wewe una shaka na suala nenda kalifanyie utafiti hawa serikali wametwambia kuwa wametoa *document* kadha na kadha kaiangalie *document* ile haipo? Utaratibu gani utumike *document* hiyo ifike kwenye Baraza iangalie kwanza.

Lakini nakuombeni jazba tuziekeni upande, tuiangalie *reality*, hapa hapendwi mtu. Hapa inatakiwa upatikane audilifu. Mfanyakazi wa *ZECO* lazima apewe haki yake ya kusilizwa kama kafanya kosa ahukumiwe kwa mujibu wa sheria, sio ahukumiwe kwa mujibu wa matakwa yetu sisi Wawakilishi au serikali.

Baada ya kusema hayo nasema kwamba ningeomba tushirikiane vyombo hivi viwili Serikali na Baraza la Wawakilishi kuona kwamba suala la *ZECO* tunalifikisha kwenye vyombo vinavyohusika kwa taratibu zinazostahiki ili haki ipatikane tena iwe haki ya kweli sio ya kusukuma sukuma.

Tukianza kuzozana zozana hawa hawatapata haki zao kwa mujibu wa sheria. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kidogo kuna mabadiliko baada ya kuzungumza Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, atakaefuata Mhe. Ramadhani Abdalla Shaaban, Waziri wa Nchi, Makaazi, Maji na Nishati na baadae atazungumza Mhe. Haroun Ali Suleiman Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi na Umma, kisha ndio Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi napenda kuchukuwa nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa kupata nafasi hii ya kukuzungumza juu ya hoja hii ya serikali inayozungumzia ripoti muhimu kabisa ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachotaka kusema kwenye mchango wangu ni kwamba niliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi ya Baraza la Wawakilishi. Wakati ule nikiwa mwenyekiti tukiwa tukifanyakazi ya kuhoji wizara mbali mbali katika bajeti na pia tukipata kazi maalum kama hii ambayo iliofanywa na Wajumbe hawa.

Na tulikuwa tukimaliza ripoti zetu tunaweka mapendekezo na mapendekezo haya tunawasilisha serikalini. Serikali inapokea mapendekezo yetu inakwenda kuyafanyiakazi. Katika baadhi ya maeneo katika ripoti yetu tunafanikiwa kwa mujibu wa mapendekezo yetu na katika baadhi ya maeneo tulikuwa hatupati

jibu lolote kwa sababu tunaelewa kwamba pengine serikali katika kichunguza imeona kwamba maeneo yale hayana nguvu sana.

Sasa katika hali hiyo mimi ninachotaka kusema tulikuwa tukifanya hivyo tulikuwa tukijua kwamba ilikuwa kazi yetu kubwa ni kuishauri serikali kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakati ule. Tulikuwa tunaishauri serikali kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa hivyo, tulikuwa tukifanya kazi hiyo. Nimefanya kazi hiyo si muda mrefu sana kwenye mwaka 1981 na nimekuwa mwenyekiti pale kwa kamati mbali mbali na tukizipeleka na zikijadiliwa.

Kwa hivyo, naomba kuwaomba wenzangu kwamba kuleta ripoti katika serikali na ikaangaliwa ni jambo la kawaida na ina wajibu ifanywe hivyo na halafu taarifa ya serikali huwa inaletwa serikalini kueleweshwa utekelezaji wa ripoti ile.

Mhe. Mwenyekiti, katika wizara aliebahatika katika Baraza hili kipindi hiki ni mimi. Maana nimechanguliwa kuwa Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati katika kipindi hicho hicho kifupi baada ya kufika tu hata sijaanza kazi imeundwa kamati hii imekuja kuchunguza Shirika la Umeme *ZECO,* mie nimebahatika, kuna siku yalioandikwa kwenye ripoti ile yatanisaidia sana kazi yangu pengine nisingepata nafasi hii nisingejua mengi ambayo yamo katika ripoti ile sasa hivi.

Lakini yamo na nimeshayajua kwamba katika ripoti ile mna nini na nini na *ZECO* imefatiliwa kifungu kwa kifungu. sasa mimi ninachotakiwa sasa hivi kufanyakazi kwa ajili ya ripoti hii. Kwa hiyo, mimi nimebahatika na sio hapo tu. Baada ya kufika vile vile kumeundwa tume ya kuchungua ardhi huko nako nasema nimebahatika kweli kweli na nangojea hiyo ripoti ya ardhi nayo nijue namna ya kufanya kazi vizuri.

Kwa hivyo, mimi nimepata kazi katika kipindi ambacho Wajumbe hawa wameshafanya kazi nzuri kabisa wameshanipa nafasi mimi ya kufanyakazi yangu vizuri katika Baraza hili kuvishughulikia vyombo hivi ambavyo sasa hivi vipo. Na nasema mwenyekiti kwamba katika kipindi hiki kama alivyosema Mhe. Nassor Ahmed Mazrui hapa tuone maendeleo yamepatikana katika *ZECO*, tuseme tu kwamba haifai, *ZECO* iko hivi, *ZECO* nayo inafanya kazi. Kuna mambo mengi ambayo yameshafanywa na ZECO ni mazuri katika kipindi hichi.

Labda niseme machache tulikuwa na matatizo ya makusanyo. Alhamdullah mwaka jana
tulikuwa tukikusanya shilingi bilioni 32, tumepiga hatua. Sasa hivi *ZECO* wanakusanya bilioni 46 na ushee. Hii ni hatua nzuri sana kwamba wanafanya kazi. *ZECO* imeendelea katika kufanya kazi nzuri katika kipindi hiki kutokana na maelezo yanayotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wetu wa Baraza la Wawakilishi katika kipindi mbali mbali.

Wameweza kuwaungia umeme watu elfu tisa mwaka huu, wakati mwaka jana waliowaungia umeme ni watu elfu tano tu. Kwa hivyo, ni *achievement* nzuri imefanywa na ZECO. ZECO wamejitahidi sana katika kipindi hichi mwaka mmoja uliopita, imeweza kupeleka umeme katika vijiji 22 kwamba ni hatua nzuri sana. Wamepeleka:-

1. Kilindi
2. Zimahongwe
3. Mahongweni
4. Fimbo
5. Chanjamjawiri
6. Sipekwe
7. Muazini
8. Ndegeni
8.Maweni
9.Mapape

10.Makangale
11.Mwane
12. Mwakibaba
13. Wivumtogwe
14.Kwajichovi
15.Mtwango
16.Mkanyageni
17.Koani Kibondemaji
18.Kianga Kiombangoma
19.Fuoni Michenzani
20.Kama
21Mwera Mtofani

Kwa mwaka mmoja wamefanya kazi hii. (*Makofi*).

Na karibu Ukunjwi anasema Mheshimiwa hapa wameshakwenda ku-*survery* na kila kitu, wanafanya kazi. Wajumbe mumesaidia *ZECO* katika kazi zenu. *ZECO* imeweza kusimamia mradi huu wa *megawatt 100* katika mwaka huu. Alhamdullah si haba , umeme wa megawatt 100 umeshafika Zanzibar hivi sasa na unatumika na ili kuondoa matatizo kwa wananchi *ZECO* waliomba kwamba hata kama mradi hatujakabidhiwa lakini turuhusiwe kuutumia. Na ndio maana tukaruhusiwa kuutumia tukaufungua mradi ule na tukaanza kuutumia ili kuondoa tatizo la umeme.

Na ndio maana juzi ikatokezea hapa dharura ya kwamba kuna nguzo hazikusimama vizuri. Maana mradi ilikuwa haujakabidhiwa. Washauri wale ndio wakasema hizi kwamba hizi nguzo hazijasimama vizuri. Kwa hivyo, tunaomba hawa waliozijenga wakazifanyie matengenezo wakati sisi tunafaidika. Tukafunga kwa kipindi hichi kifupi tu, watu wakaanza kulalamika ooh! wameanza wamefunga, majenereta yapo hawatumii kwa nini.

Hawakufanya makosa, wanahitaji kuelimishwa tu kwamba kuyatumia majenereta yale ni hasara. Sasa yale majenereta ni ya nini kama anavyouliza mtu huko nyuma yangu, ni ya *emergency*. Lakini tunayo njia yetu ya zamani ya umeme tunaweza kuitumia njia yetu ya zamani ya umeme na tukaweza kuzima kwa muda wa saa moja moja angalau tukaweza kufanya matengenezo.

Mhe. Mwenyekiti, matengenezo yamekamilika na hivi sasa hakuna suala tena la kuzimwa umeme. Mambo yanaendelea vizuri tu. (*Makofi*).

ZECO wamejitahidi kupunguza uzimikaji wa umeme na ndio hivi vituo vitatu hivi sasa vya umeme vilivyopo; hichi kilichokuwepo hapa Mpendae, Mwanyanya, Welezo kwa kupunguza hii *tension* ya umeme. Kwa hivyo, tusiwasakame kiasi ambacho wakaonekana hawana maana kabisa. Lakini katika kufanya kazi utelezi unatokea. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hayo nimeona niyazungumze katika suala la kadhia ya *ZECO*.

Sasa ninataka kuzungumza mambo yaliyochomoza katika michango ya Wajumbe mbali mbali. Mhe. Waziri wa Sheria ameshazungumza juu ya suala la wafanyakazi wetu ambao wamesimamishwa kazi na wengine wamehamishwa katika maeneo. Unaweza ukahisi kwamba kuhamishwa katika eneo lako unalofanya kazi, unaweza ukaona kama si adhabu, ni kweli utaratibu wa kazi lakini wakati mwengine hutegemea pale unapofanya kazi kuhamishwa ni adhabu, maana umeshakuwa na mkono mkono, unachota chota, leo unahamishwa hupati tena kuchota ,si adhabu hiyo, maana una mkono mkono, mara kunyakua hichi, mara kuteka hapa. Sasa unahamishwa hufiki tena pale kwenda kuchota, peke yake ni adhabu hiyo. Kwa hivyo, hiyo ni adhabu.

Lakini kuna la pili umeshabainika kwamba wewe ni fundi wa kuchota lakini pia ni fundi wa kuficha, mambo mawili yote

unayo. Pale pakija kufanyiwa uchunguzi wewe ukiwepo hapapatikani kitu, uondoshwe pale ili uchunguzi unapoendelea pale wewe uwe hupo usiharibu ushahidi wa mwahala pale. Haina maana kwamba kesi yako ndio imekwisha. (*Makofi*).

Mimi nilivutiwa sana na mchango wa Mhe. Hamza Hassaan Juma, aliposema kwamba huyu aliyechukua pesa apelekwe Polisi ashtakiwe, ndio kwani kuna tatizo gani? Si mchango mbaya, ni mchango mzuri kwamba hili suala sio dogo lazima ashughulikiwe. Lakini sasa ukiendelea kumuweka pale, huo ushahidi pia utapotea pale. Na wengine akina Kaduwara na nani; hawa unajua kuna mambo Mhe. Mwenyekiti, ukiyatizama hayaingii kwenye ukweli kabisa kutokana na ile kesi.

Huyu Kaduwara wakati Mhe. Makame Mshimba Mbarouk katika Kamati yake ya Miundombinu na Mawasiliano alipokwenda kutembelea kule, alipokuta ile kamati inafanya kazi kweli kweli, alituma *message* akawaletea Waheshimiwa wengine, jamani imekuja kamati inapewa pesa, inafanya mambo ya ajabu ajabu. Maana anaona anakaribiwa karibiwa pale.

Hiyo *message* ipo lakini Mhe. Makame Mshimba Mbarouk akamuhoji, wewe bwana umekwenda kusema kule sisi tunapewa pesa. Akakataa mwisho akakubali. Akaambiwa omba radhi. Akaandika barua ya kuomba radhi huyu kwa sababu alione anakaribiwa katika mambo yake. Watu wameshakuwa karibia akaona eeh! sasa hivi wataniona ndani nilivyo.

Sasa hiyo ndio hali halisi ilivyo, pana mambo mengi tu. Sio kama pale ndio kahamishwa kwamba kaisaidia kamati, kuisaidia kamati ndio kheri, si itanisaidia mimi kufanya kazi zangu vizuri. Lakini ana mambo pale kayafanya. Sasa yale mambo huwezi uyaache uyaangalie tu hivi hivi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna hili suala la majenereta 32. Mheshimiwa amelizungumzia hapa. Majenereta 32 ni kweli kama alivyosema

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui ni ya dharura na kuna mkataba ya majenereta yale 32. Majenereta yale 32 washirika wa maendeleo walitaka kuhakikisha kuwa fedha wanazozitoa zinatumika ipasavyo na waliwateuwa mameneja wa mradi wa umeme vijijini wakati huo, yupo bwana mmoja anaitwa Mr. Notrize kutoka Norway na mshauri mwelekezi wa manununzi kutoka No Plan ya Norway ni *sustain* waliochagua hawa kama ndio wasimamie masuala majenereta yale 32 katika unununzi wake. Ndio waliotayarisha zabuni ya unununzi majenereta haya na ndio waliofanya tathmini ya zabuni hizo.

Tathmini ya mshauri kuwasilishwa katika kikao cha pamoja cha kamati ya mradi ambayo ilikubaliana na mapendekezo ya ushauri ya kuteuwa Kampuni ya Matrica kuyaleta majanereta na kuyafunga pale. Hawa ndio waliofanya kazi katika majenereta haya ambayo ni majenereta ya *emergency* wakati ule tuna kiza cha miezi mitatu.

Sasa hawa tulipata taabu hapa, kulikuwa maji kuyapata mjini ilikuwa taabu hapa na wakati ule ilikuwa lazima tupate majenereta ya *emergency*, yakapatikana haya. Lakini walikuwa na mkataba. Wanasema washirika wa maendeleo walishauri kuwa mara tu waya wa pili wa umeme utakapokamilika kuwepo na majadiliano baina ya SMZ na washirika hao ili kujadili hatma ya majenereta hayo kama inavyoelezwa kwenye mkataba, (*Article 111* na *Article VII*
ya *agreement* ya majenereta yale). Tangu mwanzo yalikuwa ikifika wakati fulani majenereta yale wakae kitako wazungumzie hatma yake, kwa sababu suala la umeme litakuwa limeshatulia.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo ninapenda kulizungumza katika nafasi hii ya ripoti hii, ni ripoti nzuri ambayo itanisaidia sana inahusu bei za umeme. Baadhi ya Wajumbe walisema hapa kwamba bei za umeme zinapanda tu ovyo, watu taaban wanaumia na nini.

Mhe. Mwenyekiti, na sisi ni miongoni mwa wananchi na tunahakika hatukai maisha katika uongozi, tuna hakika tutaondoka katika uongozi na tutakuwa nje ya uongozi wakati fulani, tuna hakika hiyo. Kwa sababu hii ni nchi ya kidemokrasia hakuna mfalme hapa kwamba atakaa kwenye kiti cha mfalme mpaka afe halafu akazikwe kwa sherehe tu, haiwezekani hiyo. (*Makofi*).

Sasa kwa nini tuweke mambo ambayo tukija kuondoka katika uongozi yake yatuumize. Lakini lisilobudi hutendwa. Mhe. Mwenyekiti, ukiomba msaada kwa wahisani, wafadhili au washirika wa maendeleo wanakupa mashirika. Jambo moja wanalopigia kelele ni *tariff* za umeme. Wanasema sisi tutakusaidieni kuleta *megawatt 100* lakini muzirekebishe *current* zenu mpate faida. Maana yake hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, wastani wa makusanyo kwa mwezi ni shilingi bilioni tatu milioni mia mbili, ndio makusanyo kwa mwezi.

Lakini gharama za ununuzi wa umeme kutoka *TANESCO* ni shilingi bilioni tatu milioni mia saba na sitini. Ni kubwa kuliko makusanyo yetu. Washirika wa maendeleo wakasema hapana badilisheni *tariff* ili muweze kuliendesha shirika kwa faida. Sasa hiyo ndio inayotulazimisha kupeleka umeme. Umeme utakuwa rahisi Zanzibar wakati tutakapopata gesi yetu na kuzalisha umeme basi. Hapo ndipo umeme utakuwa rahisi Zanzibar.(*Makofi*).

Lakini kwa sasa hivi tuseme umeme tupate rahisi hatupati wananchi tuwaambieni kweli kwa bei rahisi hivi sasa, kwa sababu tunanunua kutoka kwa wenzetu. Lakini wakati huo tumeshapata gesi yetu hapa, aah! *unit* moja ya umeme itakuwa senti saba tu au senti kumi tu za dola basi, kutakuwa hakuna tena matatizo haya. (*Makofi*).

Sasa hii ndio hali halisi ya sasa hivi na sio kwamba sisi tunataka wananchi wale wapate taabu, waumie, tunawapandishia umeme

ovyo ovyo, hapana tusiwadanganye, tuwaeleze ukweli wetu juu ya masuala haya kwamba hali hii ngumu katika nchi yetu lazima twende hivi. *Otherwise* tuamue tusitumie umeme. Sasa hilo litakuwa ni suala jengine. Hapa tutapopata umeme wetu matatizo yatakuwa yameondoka.

Juzi Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa taaban kweli na nilikuwa taaban kwa sababu tuliambiwa kwamba kuna mahala kumeungwa umeme kwa nguzo 40 bure. Mimi nimeshakwenda mara mbili kule, kwenda kuhesabu zile nguzo, nimefanya kazi nzito kweli. Sasa nikajiuliza hizi nguzo 40 zimeanzia wapi mpaka kufika pale hata zikatimia 40. Nikaona aah! bora niende mara ya tatu.

Jana nikawaambia maafisa wangu wa umeme hebu twendeni tena kule Matemwe mukanioneshe hasa umeme mumeanza kuuchukua wapi nyinyi, mumeuchukua skuli? Mkwajuni? mjini? hebu twendeni mukanioneshe pale. Nimekwenda jana mimi pale, wakaniambia tumechukua hapa kwenye Hoteli ya Zi-Villa; hii hapa Zi-Villa hapa ndio tulipouchukua, tukaushusha kwa mara ya kwanza katika Hoteli inayoitwa Kasha, hii hapa
Hoteli ya pili. Zi-Villa ndipo ilipoanza na Kasha ndipo ulipofika kwa mara ya kwanza na tukauchukua hapa mpaka kwenye hiyo nyumba inayoitwa kandili. Ndio hiyo nyumba inayozungumzwa.

Kutoka Zi-Villa mpaka Kasha nimezihesabu nguzo ni nguzo saba. Nimehesabu vipi? Kule pahala ni maweni, nguzo huwezi kuiweka peke yake kwa sababu huwezi kuchimba shimo la kutosha kama utakavyochimba Bambi; Bambi unaweza kwenda chini sana shimo lake. Nikahesabu zile nguzo ni saba; nyengine zimekaa tatu na nyengine zinakaa mbili; nguzo saba umeshafika kwenye hoteli ya Kasha.

Kutoka kwenye Hoteli ya Kasha mpaka hii Kandili, nimezihesabu zipo tatu pamoja, zipo mbili pamoja, zipo nne pamoja, nikazihesabu zipo nguzo kumi na mbili. Kumi na mbili na saba ni nguzo kumi na tisa. Tena sio nguzo kumi na tisa

zimenyooka moja, mbili, tatu, nne, tano hapana, kwa sababu ile ni ardhi ya maweni zimeekwa nyengine mbili, nyengine tatu nimekwenda. Zi-Villa ipo nimeziona.

Kwa hivyo, hiyo nilikuwa ninajua kwamba nguzo zipo hivyo lakini juzi nilipoambiwa kuna nguzo arobaini, nilisema hapana bora niende nikaone tena, maana yake pengine sijui umeanza wapi ule umeme kuchukuliwa pale. Zi-Villa upo zamani pale na ndio ukachukue pale ukapeleka katika maeneo yale. Ndani kuna nguzo mbili ambazo kachomeka mwenyewe kwa ajili ya kutia kama tunavyochukua wewe umeme pale ukapeleka nyumbani.

Ninataka niseme Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili linawaomba *ZECO* wapeleke miundombinu ya umeme pahali ambapo panataka kuendelezwa baadae. Hilo ninaombwa. Kwetu kule umechukuliwa umeme kutoka Mgenihaji uwandani mpaka Ubago hakuna nyumba hata moja njiani, kwa sababu unapelekwa kwenye huduma unakwenda ukatumike wanapotaka wananchi, uwanda kwa uwanda umepita.

Kuna umeme umetoka Mkwajungoma Ndijani umekuja mpaka Binguni hapa panapotaka kujengwa hospitali nguzo zinafika kumi na tano au ishirini, hapana nguzo iliyotozwa pesa pale kwa mtu. Ni kazi yetu kupeleka umeme katika maeneo ya wananchi. Na hivi sasa *ZECO* wana nia ya kuuchukua umeme kutoka Kandili, tayari wameshaandaa hiyo *project* kuupeleka Kijini kule Kaskazi kutoka pale, lazima wapeleke kabla hakujajengwa. Uwezo tu Mhe. Mwenyekiti, unakuwa mdogo lakini kupeleka miundombinu kabisa ni vizuri. (*Makofi*).

Sasa ikiwa umeme umepita pale Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kajenga nyumba yake ukasema kapelekewa makusudi yeye. Tunapeleka umeme katika maeneo ambayo umeme haujafika. Mhe. Mwenyekiti, hiyo kazi inafanywa na *ZECO*. (Makofi).

Sasa tukipata uwezo wa kupeleka umeme maeneo mengine, sisi tunamtoza *service line* lakini hizi *line* za *high tension* tunapeleka wenyewe.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, ninataka kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wetu hawa walisaidie Shirika la *ZECO* liweze kufanya faida zaidi. Wanapotuletea maombi watuletee maombi, watusaidie kupiga kampeni mule tunapopeleka umeme wetu, wale tunawapelekea umeme ule wawe wanautumia ili kupata mapato zaidi katika hili shirika.

Nawaomba hawa kwa sababu hawa Mhe. Mwenyekiti, ndio Wawakilishi wanaoomba kusambaziwa umeme katika maeneo mbali mbali. Huwa tuna taabu kweli mtu anapokuja akatwambia tuleteeni umeme kwangu, tukahangaika tukapeleka umeme mpaka ukafika lakini hakuna mtu anayeutumia, inakuwa ni hasara, umeme upo kwenye nguzo tu hivi basi unachungulia chini hakuna anayetumia hata mmoja.

Watusaidie na mifano hii ninayo, sitaki kuitaja hapa aah! Ninanyamaza kimya, sina sababu ya kuitaja hapa lakini ipo tumepeleka umeme katika maeneo hivi sasa hautumiki, umekaa tu pale shirika limeshapoteza nguzo zake chungu nzima lakini hakuna mtu anayeutumia, ni hasara kwetu. Kwa hivyo, watusaidie Waheshimiwa, mimi ninawaomba sana ili *ZECO* iweze kupata faida.

Mimi naomba kwamba hii ripoti nipewe nafasi kwenda kuifanyia kazi. Itakapokelewa hapa nitapata nguvu ya kuifanyia kazi hii ripoti. Ikikataliwa nitaifanyia kazi lakini nitakuwa ninaifanyia kazi tu, lakini nitajua sina *support*, maana yake ni ripoti yetu hii lazima niifanyie kazi mimi, itanisaidia hii na ile ripoti ya ardhi ile naomba iletwe alau nipate kuifanyia kazi. (*Makofi*).

Naunga mkono hoja.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Sasa ninamkaribisha Mhe. Haroun Ali Suleiman.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru Mwenyezi Mungu na mimi kupata nafasi hii.

Lakini kabla sijaendelea naomba kurekebisha jina langu. Mimi jina langu ni Haroun Ali Suleiman lakini kadhaa nimekuwa ninaitwa Haroun Suleiman. Suleiman ndio babu yangu.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman. Endelea.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza niwashukuru sana Waheshimiwa wote waliochangia taarifa yetu hii ya serikali iliyowasilishwa hapa. Lakini pia niwashukuru sana Mawaziri watatu walionitangulia, na mimi sitaki niongeze chumvi, niongeze mambo mengine isipokuwa na mimi madhali nimepata nafasi ya kusimama basi nitangulize kwanza kuunga mkono hoja hii ya serikali au taarifa hii ya serikali kwa asilimia mia moja.(Makofi).

Mhe. Mwenyekiti, taratibu za kiutumishi au sheria za utumishi. Mimi nimekabidhiwa jukumu hili si muda mrefu ninajifunza ninasoma na ninaamini baada ya miezi miwili mitatu taarifa hizi au sheria hizi za utumishi zitakuwa kwenye hali ambayo nitazifahamu vizuri na nitazielewa vizuri zaidi.

Kwa hivyo, nitazungumzia *experience* yangu tu katika masuala mbali mbali juu ya hatua ambazo zinachukuliwa kwa makosa ambayo yanatendeka kwa baadhi ya wafanyakazi. Nirudi nyuma kidogo Mhe. Mwenyekiti, tusifikirie kwamba adabu mtu akifanya kosa basi adabu ya kwanza pengine afunguliwe

mashtaka au atiwe ndani. Taratibu za kiutumishi hazipo hivyo, zinakuwepo na taratibu zake.

Kuna onyo la kwanza anapewa kwa kosa alilolifanya, tena kwa mdomo ingawa Mhe. Mwenyekiti, siku moja wakati nikiwa pale Wizara ya Elimu kuna Mrajis wetu mmoja alimwita mwalimu akamwambia sasa wewe ninakupa onyo ya domo kwanza. Sasa ili asije akasahau akamwandikia na barua akamwambia ninakupa onyo la domo kwa maandishi.
Sasa kampa warning kwanza ya mdomo. Sasa ili asisahau akamwambia ninakupa onyo la domo kwa maandishi. Sasa nini maana yake. Nikamuuliza kwa nini ukachukua hatua hii wewe, ukasema ndio binadamu wana shida sana hawa, atakuja kukataa mimi kwamba sijampa onyo la mdomo huyu, lakini ninampa na barua kabisa hii kwamba nilichukua hatua ya kumpa onyo hilo, *for the sake keeping record*, aliniambia maneno hayo.

Kwa hivyo na *discipline* hizi tunapochukua Mhe. Mwenyekiti, katika mambo haya ya sheria za utumishi, hata katika sekta zetu za elimu, afya na kwengine, kuna taratibu zake. Kafanya kosa kuna mkuu wa idara, kafanya kosa kuna Katibu Mkuu, mpaka makosa haya yanakwenda *industry court* yanafika huko.

Lakini adabu ni adabu kazungumza mheshimiwa mmoja hapa mwenzangu hapa Mhe. Ramadhani Abdalla Shaaban. Hata nilipokuwa mwalimu mkuu wa Skuli ya Haile Selassie mfano Mhe. Mgeni Hassan Juma ulikuwepo pale, mwalimu anapofanya kosa anakuudhi wewe mwalimu mkuu na anaudhi walimu wenzake basi unampelekea taarifa mkurugenzi anamuhamisha anampeleka skuli nyengine.

Sasa hapo pana kazi. Anaondoshwa Skuli ya Haile Selassie anaambiwa nenda kasomeshe Skuli ya Kidoti mfano au anaondoshwa Kidoti mfano anaambiwa kasomeshe Makunduchi. Wapo walimu waliondoshwa Makunduchi wakapelekwa Kisiwapaza.Sasa ile njia moja ya adhabu, zile fursa ambazo

ulizokuwa unazipata pale, sasa huzipati unapelekwa kwengine. Sasa Zakia huyu kuondoshwa pale ambapo alikuwa anafanya makosa yale au alikuwa anafanya tendo lile kupelekwa wizarani isionekane labda kapendelewa au si adhabu. Lakini serikali ilisema wazi wazi kwamba ataendelewa kufuatiliwa.

Na Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban kasema kitu kizuri sana Mhe. Waziri wetu wa Ardhi, kakabidhiwa wizara hii karibuni, kapata ripoti hii. PAC wamekwenda kukagua kule wamekuja na taarifa. Taarifa hizi muachieni ameshasema kuwa atazifanyia kazi na sisi kwenye utumishi tutashirikiana naye kuhakikisha kwamba mle mulimokuwa muna kasoro mbili tatu tutachukua hatua.

Lakini huyu Zakia alijua kwamba anafanya makoa yale, inawezekana ndio, inawezekana sio. Nikatoa mfano na nitamtaja Mhe. Hamza Hassan Juma, nisamehe eeh. Nitakutaja lakini kwa njia za kheri usije ukawa na wasi wasi, huyu ni mwanafunzi wangu, kwa hivyo nitamfanya lolote hana tatizo huyu.

Mhe. Hamza unaweza ukawa unafanya kosa unajua unafanya kosa lakini ukapewa kitu kikakuonesha kwamba hiki ndio *excuse* yako. Mhe. Hamza alipokuwa Skuli ya Haile Selassie huyu mwanafunzi, basi alikuwa na tabia ya kuchelewa sana ya kuja skuli pale. Ni kweli na mwenyewe atathibitisha kama kweli au uwongo. (*Kicheko*).

Mimi nilikuwa ni mwalimu mkuu, mimi nilikuwa hata simjui yule lakini ninamkumbuka na mtu akiwa na mambo fulani skuli utamkumbuka, akiwa mtoro sana, anachelewa sana, hodari sana, pocho sana. Wale wanafunzi wale ni rahisi kuwatambua na kwenye michezo kama unacheza vile vile unacheza vizuri sana utawatambua. (*Kicheko*).

Nikamwambia Mhe. Hamza njoo, mimi ninakuonea huruma, ninakupa kadi maalum au kitambulisho maalum unaweza kuja

mpaka saa moja na nusu hakuna matatizo. Lakini haina maana kwamba sasa atumie kadi ile sasa atumie kadi ile aje saa mbili, kwa sababu kaambiwa mwisho saa moja na nusu.
Sasa nimemuondosha kwenye wale wanafunzi ambao wanakuwa wanapiga mikwaju pale saa moja wanaochelewa, kwa sababu wanakaa maeneo ya pale, yeye nikampa upendeleo maalum. Ninashukuru imesaidia Barazani anakuja kwa wakati hakuna matatizo sasa hivi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ile peke yake kwamba anakuja saa moja na nusu basi ni kielelezo kwamba na yeye anapewa warning au punishment. Sasa huko anakotoka atahakikisha kwamba saa moja na nusu anafika. Lakini jee ali-*meet* hiyo *committment* hiyo ya kufika saa moja na nusu au alikuwa anaongeza mpaka saa mbili. Sasa hayo yalikuwa ni yetu sisi ya ndani.

Lakini ninachokusudia kusema Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba serikali hii ya awamu ya saba imeleta mabadiliko makubwa, *very serious* kweli ninasema. Ripoti zinajadiliwa za *CAG* zinakuja tunajadili hapa, ripoti za tume hizi zinakwenda zinajadiliwa serikalini, zinafika hapa tunazileta. Tunasema ni high class of committment ya serikali yetu.

ZECO hawa wanafanya kazi, sote tunawasifia kazi wanazozifanya na Mhe. Waziri kazungumza. Meneja huyu ukimpigia simu kama ana kazi atakuleta ujumbe mimi nina kazi au atakupigia simu baadae. Mapato yameongezeka kasema Mhe.waziri, kutoka 1718 imefika mpaka zaidi ya 30 au zaidi ya 40, kama si *committed* huyo mtu. Leo wengine tunasema kuwa na yeye angechukuliwa hatua. Hee! *haste haste* kidogo, twendeni kwa hatua, tulikotoka siko tulipofika sasa hivi, tumuombe Mwenyezi Mungu atujaalie tuendelee na *seriousness* hii ya kufanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, nasema huwezi kuonesha *indicator* unapinda kushoto halafu ukaelekea kulia. *Indicator* zinaonesha sasa

tunakwenda kwenye njia ndio kwa hivyo sote tushirikiane kwa pamoja. Imetushtua, sio Shirika la Umeme tu pengine na maeneo mengine na sisi tuna taasisi zetu kwenye mawizara yetu nayo pia yatatusaidia sisi kujua tuwaangalie kwa kiasi gani watendaji wetu hawa katika utekelezaji wao wa kazi. Tunapokea maoni na ushauri kwa wakati wowote.

Kwa hivyo, utoaji wa adhabu hizi isionekane labda serikali imefanya kosa, bado masuala haya sio kama yamemalizika moja kwa moja tunayafanyia kazi kwa jumla. Hatuwezi kusema kwamba basi yamekwisha. Miswada inapoletwa. Tizameni mfano inapitia kwenye ngazi mbali mbali mpaka inakuja kwenye serikali kwenye *cabinet* tunaijadili, inakuja hapa inafanya mabadiliko na serikali inakubali mabadiliko yale. Maana yake ni kwamba tunaji-*commit* na sisi kwamba yale maoni yanayotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunayachukua na kuyatilia maanani. Kwa hivyo, tusijenge yale mawazo ya kwamba kila kitu ambacho kimetoka huko basi kipingwe, hapana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru Waheshimiwa Wajumbe wengi wamesema kuna mengi mazuri yamefanyika ndani ya taarifa hii yamechukuliwa hatua. Sasa kama kuna mengine ambayo Waheshimiwa Wajumbe hawajaridhika, bado serikali ndio sisi na tunafanyakazi kama timu. Wamesimama hapa mawaziri wawili au watatu na mimi nimesimama sasa hivi na mwengine atasimama. Sio kwamba tunai-*defence* serikali lakini ni wajibu wetu kufanya hivyo na tunafanya hivyo sio kwa sababu tunaipendelea hapana. Tunaangalia wajibu na haki katika masuala yote mawili. Kwa upande wa *back bencher* tuwasikilize na huku kwengine tuwasikilize Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kanuni na sheria zinasema wazi wazi humu. Kosa la kwanza onyo, wapo waliopewa onyo na wapo ambao wamesimamishwa na wanafanyiwa uchunguzi. Lakini sheria inasema ikibainika kwamba kafanya kosa, basi sheria pia

inasema wazi kumfukuza kazi mara moja. Lakini huwezi tu kumchukulia mtu adhabu kafanya kosa la kwanza hajapewa onyo la kwanza, hajapewa onyo la pili. Hapana, kuna taratibu zake. Yule yule akienda kutushtaki sisi, kwamba mimi mnanifukuza kazi au mnanisimamisha kazi kwa kosa hilo, je mliwahi kunipa onyo kwa kosa hili. Hatujawahi kumpa sio mara moja sio mara mbili, serikali tutakuwa tunaji-*embrace* sisi wenyewe.

Kwa hivyo, serikali iko makini katika suala hili. Nawaombeni sana Waheshimiwa Wajumbe pamoja na yote haya ambayo tumezungumza kwa jumla, nia ya serikali ni kuhakikisha kwamba inapambana ubadhirifu, utovu wa adamu wa aina yoyote ndani ya kazi zetu pia na masuala ambayo yanahusiana na masuala ya rushwa. Huyu bi Zakiya katajwa sana, lakini bi Zakiya huyu pesa zimetiwa kwenye *account* yake. Tunasema kwamba adhabu aliyopewa kapelekwa kwenye wizara haikuwa sahihi. Mhe. Ramadhan Abdalla kasema ilikuwa sahihi na mimi nakubali kuwa ni sahihi. Lakini tutizame *understanding* yake huyu bi Zakiya. Tunasema kulikuwa na *conflict of interest,* pesa katiliwa kwenye *account* yake, sawa.

Mfano mimi ni Waziri wa kazi au Waziri wa afya au Waziri wa elimu au Waziri wa kilimo. Kuna kazi inakuja *tender* fulani na mimi nina kampuni yangu inafanyakazi kwenye wizara yangu inataka kupewa kazi, lakini kumbe kuna kampuni inahusiana na mimi, basi mimi nika *influence* nikasema ipeni kampuni fulani kazi hii, wapewa hata kama wana haki na uwezo wa kufanya vile kwa mujibu wa utaratibu wa kazi pale itakuwa kuna *conflict of interest.* Kwa hivyo, kibinadamu na kiungwana usifanye tendo kama lile.

Mimi hata kama nina ndugu yangu baba mmoja mama mmoja ana uwezo wa kuwa na cheo chochote kile, nikimteuwa kwenye mabodi nikimpa uwenyekiti kwa mfano itakuwa ni *conflict of interest* itaonekana pale pana kitu kama hicho. Kwa hivyo, hata

kama ana uwezo sio dhambi, kwa sababu mimi mwanangu au ndugu yangu au mtu yeyote kuwa na uwezo akateuliwa na mtu mwengine sio tatizo, kwa nini. Akiwa mfanyabiashara, akiwa mwalimu, akiwa mkurugenzi hakuna tatizo ni haki yake yule na yeye ni raia kama raia mwengine. Lakini tunaangalia mambo haya, hasa mambo ya kibiashara na mambo haya yanaleta athari zake kama hivyo.

Sasa huyu mama yeye katiliwa pesa kwenye *account* yake, mimi naona dhana yake aliona kwamba aa! ndio nimepewa kazi. Sasa kanunua vifaa vile, kama kanunua *ZECO* au nje ya *ZECO* ni *understanding* yake mwenyewe. Lakini kama yeye ni mtaalamu kapewa na yeye maskini ya Mungu pengine hakufahamu kwamba hili ninalolifanya ni kosa, inawezekana alikuwa analielewa na inawezekana halielewi. Ndio tukampa *benefit of dought* sasa. Akaondoshwa pale na kupelekwa wizarani na hili suala serikali imesema inaendelea kulifuatilia ili afuatiliwe zaidi.

Kwa hivyo, nadhani tuelewane na hapa *shadow* inasema wazi wazi nambari 2 *dishonest*
adhabu zake ziko vipi, yaani *thief of any nature*, wizi wa aina yoyote. Lakini je huu tuutafsiri kama ni wizi, tutafsiri kama ni kutokujua au tufanye vipi. Kwa sababu kama ingekuwa ni wizi katumia pesa za shirika kwa maslahi yake, lakini zile pesa zimetoka kwa mtu mwengine wa nje katiliwa kwenye *account* yake asimamie ile kazi, kafanya. Sasa kama kanunua *ZECO* kenda kununua kwengine ni *understanding* yake mwenyewe. Sasa naomba jambo hili kidogo tulipimeni kwa makini sana jamani, kwa sababu hii ndio kesi kubwa ambayo imezungumzwa na wengi na tusifike mahapa tuka- *draw early conclusion* halafu *baadae tuka-regret*,
naomba sana waheshimiwa mambo kama haya ambayo yanamgusa mwananchi, yanamgusa raia haki yake, yanagusa maslahi yake ya maisha. Mhe. Ramadhan Abdalla kasema hapa kwamba kuna siku sisi hatutokuwepo hapa, kuna siku tutajikuta tunarudi huko.

Mimi huwatania watu Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa Waziri wa Elimu nilianza Mambo Msige kule, baadae tukajenga jengo letu tukahamia Mazizini. Sasa niko Mwanakwerekwe, naona naelekea karibu ya Makunduchi. Lakini naona narudishwa tena mjini, sasa sijui mambo yatakuwa vipi. Mwisho wetu tutarudi katika maeneo yetu kwenye vijiji vyetu. Nawaomba sana Waheshimiwa tukae tutafakari sana mambo haya na tuipongezeni sana Serikali yetu ya Awamu ya Saba, haya mambo yanayofanyika miaka mingi huko hayajafanyika. Mengine mazuri yametendeka na sasa haya tunayaendeleza kuyafanya, tujengeni *spirit* tusiwe mipaka kati ya *back benchers* na Mawaziri, sote ni wamoja.

Kuna siku Mhe. Abdalla Juma Abdalla, utakuja huku na sisi tutakuja huko na tumeshayaona yameshatendeka humu. Kwa hivyo, tujitahidini sana. Mhe. Haji Omar Kheir miaka 15 iliyopita alikuwa huko, miaka miwili hii ndio kaja huku kwa Mawaziri. Mimi nashukuru Mwenyezi Mungu tokea mambo yameanza ndio niko huku huku. Inshaallah lenye heri na mimi niendelee kuwanalo nilipate *Inshaallah.* Lakini ninachosema nawaombeni sana Waheshimiwa Wajumbe tujengeni *spirit* ya umoja, hili jambo ni letu sote, palipokosewa hapa na pale kama pana hitilafu serikali imeshasikia italitafakari na kuona kiasi gani tulifanyie kazi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuunga mkono tena hoja. Ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, na mimi baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya tukaweza kushiriki katika shughuli yetu hii ya leo, naomba nikushukuru kwa kunipa na mimi fursa hii.

Pili, Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuzungumza waliotangulia kusema kweli mengi wameyazungumza tena kwa lugha ambayo,

maana nadhani wote waliozungumza walikuwa walimu. Kwa hivyo, wamezungumza kwa lugha ya kiualimu na mimi naomba nizungumze machache tu na naomba nizungumze katika maeneo mawili makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, eneo la kwanza nadhani kuna mambo humu ndani ya chombo chetu tunaweza tukakaa tukatofautiana, kwa sababu ya mtizamo na kwa sababu ya ufahamu. Lakini kuna mambo hatuwezi kutofautiana, ni lazima sote tuwe na uelewa unaofanana, kwa sababu haya ni mambo ya *principle*. Tukitofautiana humu ndani ya chombo chetu tutapata shida na tutawapatisha shida wale tunaowatumikia, kwa sababu hapa ndipo wanapoangalia kwamba muongozo unaotoka hapa na utaratibu unaotoka hapa na kwa sababu chombo hiki kinafanyakazi zake kwa uwazi, wananchi wengi hawajui kinachoendelea ndani ya serikali kwa maana ya *executive* na wananchi wengi kwa bahati mbaya hata kupita mbele ya mahakama wanaogopa.

Kwa hivyo, hawakijui hata kinachoendelea ndani ya mahakama. Lakini ndani ya chombo hiki wana fursa kubwa ya kuona kinachoendelea, kufahamu kinachoendelea na bahati nzuri wanawekewa kumbukumbu ya kila nukta inayozungumzwa katika chombo hiki. Kwa hivyo, ni muhimu sana kwa umuhimu wa chombo hiki kuna mambo tukiyazungumza yanaweza yakawababaisha wananchi.

Kwa hivyo, mimi nilitaka kuyazungumza hayo kwa uchache na ninawashukuru, ningekuwa nina kofia nyingi kama Mhe. Hamza Hassan Juma, labda ningeyazungumza hiyo, lakini bahati mbaya nadhani kwa sababu ya kichwa kimoja na kofia ndio hiyo hiyo moja.

Suala la kwanza ambalo tunalizungumza ni msingi wa hoja yetu, tumezungumza hapa zilitoka hoja kidogo kwamba hii ni taarifa au ni hoja. Mimi nasema kwa sababu tunalizungumza na ni

jambo muhimu na limeingia kwenye kumbukumbu kwamba tuna wasi wasi hii ni hoja au ni taarifa. Nadhani sio jambo la kulidharau, nikasema tu kwamba ni vizuri labda na mimi nitowe fikra ya kwamba kwa mujibu wa kanuni zetu, tukiisoma ile kanuni yenyewe ya 48 imeeleza kwamba mjadala unaweza kuanzishwa ama kwa hoja au kwa utaratibu mwengine ulioelekezwa ndani ya kanuni. Kwa sababu inasema isipokuwa kama kanuni itaelekeza vyenginevyo, kila mjadala utaanzishwa kwa hoja.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ukisoma kanuni ya 27 ukasoma na kanuni ya 44, hasa kanuni ya 44 fasili ya (4) ni kwamba mjadala ndani ya Baraza unaweza kuanzishwa ama kwa hoja ambayo itakuwa imetimiza masharti ya kanuni ya 48, 49 na 50 au kwa njia zilizoelezwa katika kanuni ya 27 na 44 kwamba taarifa nayo ya serikali ni moja ya jambo ambalo linaweza likaanzisha mjadala ndani ya Baraza. Kwa hivyo, tukubaliane kwamba taarifa ya serikali ni taarifa na kwa mujibu wa kanuni ya 44 fasili ya (4) inaweza nayo kuanzisha mjadala vile vile kwa kufuata masharti ya kanuni ya 48. Kwa hivyo, nilisema hilo niliweke sawa kidogo tu.

Suala la pili ni hili ambalo limezungumzwa sana kwamba ripoti kwa nini kamati imekaa imekusanya vielelezo 100, imekusanya maelezo halafu kwa nini tena ziende zikachunguzwe na polisi, kwa nini zisiende kwa *DPP*. Hili ni jambo la msingi kusema kwali ndio ninalosema kwamba hili hatuwezi kutofautiana ni vizuri ndani ya Baraza tukubaliane kwamba msingi wa mambo haya ni upi. Suala hili wengine wamelisema kwa uchungu na kwa masikitiko kidogo kwamba labda Baraza linadharauliwa. Mimi nasema serikali itakayodharau Baraza sijui, lakini katika hali ya kawaida haiwezekani, kwa sababu tunaitaja tu kama Baraza lakini serikali ndio msimamizi wa dola. Kazi ya Baraza ni kuichunga serikali na sio tu kuchunga serikali, lakini kuchunga mfumo wa uendeshaji mzima wa dola yenyewe.

Kwa hivyo, Baraza ni kama mtu kavaa suti basi ni lazima akivaa suruali na koti, sasa ikiwa kapiga pasi koti lakini suruali hakupiga pasi au haifui, huyo atakuwa mtu wa ajabu kweli kweli, maana yake ni lazima utimize vitu hivi ndio uvae na kuwa nadhifu. Sasa hayo mimi nasema ni lazima dhana hiyo tuiondowe. Ni kwa sababu ya utaratibu na wala tusione kuwa ni dharau. Kwa sababu katika uchunguzi, kuna uchunguzi tunaita *inquest* huu unasimamiwa na majaji. Lakini ripoti ya *inquest* haipelekwi moja kwa moja pamoja na kwamba imesimamiwa na jaji, ikapelekwa kuwa ni ushahidi mtu akatiwa hatiani, huu ni uchunguzi wa vifo vya ghafla ni lazima zipite tena taratibu zile zile za kiuchunguzi.

Lakini kuna *commission of inquires* ambazo hapa tunaziunda kwa mujibu wa sheria. Kama zile za meli zilizoundwa, zile mwenyekiti alikuwa jaji wa Mahakama Kuu, katibu wake alikuwa ni mwendesha mashtaka mzoefu, maana aliwahi kuwa mkuu wa kitengo cha mashtaka katika ngazi ya mahakama za mikoa ndugu Shaaban na wengine wataalamu wakubwa wakubwa. Lakini ripoti zao zilipokuja pamoja na kusema kwamba huyu ashtakiwe na huyu, hazikupelekwa moja kwa moja mahakamani, zilirudishwa tena polisi wakafanya uchunguzi halafu ndio zikapelekwa mahakamani. Sasa na ripoti ya kamati nayo hii ni *quasi judicial inquiry* kwa mujibu wa sheria yetu nambari 4 ya mwaka 2007, tunaita ni *quasi judiciary inquiry* sawa sawa na *commission of inquiry*. Kwa hivyo, huwezi kuichukua ile ripoti yake ukaipeleka mahakamani au ukampelekea *DPP* moja kwa moja. Haya mambo mimi nasema ni kiasi cha kujenga kuaminiana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe nimekuwa *DPP* kwa miaka 9. Kwa hivyo, siwezi nikaishauri serikali nikaipotosha katika jambo ambalo hiyo Ofisi ya *DPP* Baraza hili ilikuwa ndio mama maana ndio iliyoizaa ile ofisi, lakini mkanipa ulezi wa kuilea kwa miaka 9. Kama ni msichana aliyepata ulaji mzuri na mbegu nzuri basi miaka 9 anaolewa. Sasa ndio nasema kwamba sio kwa

kudharau Baraza, sio kwa kuona kwamba hizi ripoti sio, ni kwa sababu ya utaratibu na utaratibu wake naomba niueleze kidogo tu.

Utaratibu wa kwanza ni kwamba uchunguzi wa kijinai kuna mambo ambayo ni lazima uyazingatie kuthibitisha lile kosa. Inawezekana umefanya uchunguzi mzuri, umekusanya vielelezo vizuri, lakini ukichunguza jinai ni lazima ujiulize lile kosa unalochunguzia lina viini gani na katika vile viini ndio utafute ushahidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nitowe mfano ili utusaidie kufahamu tu. Huku Uswahilini ukimwambia mtu fumanizi, basi anajua ni kumkuta mke wa mtu pahala, hiyo inatosha kama wana nguo au hawana nguo. Sasa ukimwambia huyu nenda kachunguze, basi yeye atakuambia ni kweli mimi niliona na fulani alikuwepo tumewakuta ndani chumbani. Sasa leo ukijakumwambia ushahidi huo hautoshi atakuwa mkali, unataka ushahidi gani tena.

Kwenye kuchunguza kosa la jinai tunasema, ili lile liwe ni kosa la *adultery* ni lazima kwanza uthibitishe kwamba, kwanza yule alikuwa ni mke wa mtu na kwamba yule mume hakukubali jambo lile.

Waheshimiwa Wajumbe: *(Vicheko/Makofi).*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: ndio sheria inavyosema Mhe. Mwenyekiti, wako wanaume wanaokubali na ndio maana sheria ikasema hivyo, na jambo la tatu ni kwamba huyo aliyechukua huyo mke wa mtu awe alikuwa hajui kama huyo ni mke wa mtu.

Lakini jambo la nne ni lazima iwepo *dakhala*, hapo ndio itakuwa kosa la *adultery* limetimia. Ndio kuchunguza jinai, kwamba Baraza limechunguza lakini mwisho inasema ichukuliwe hatua za kisheria ni kwamba yale iliyochunguza haikuanza na viini vya

hayo makosa yenyewe itakaporudi polisi watapata pahala pazuri sana pa kuanzia na hata ukiwa jaji huchunguzi kijinai. Wakati mwengine kwenye vielelezo vile kuna maandishi mengi tumechukua ni kielelezo, lakini ili uthibitishe kosa kijinai ni lazima uende ukapate *handwriting expert*, athibitishe kweli hizi ni za fulani, lazima upate *forensic examination* baadhi ya mambo. Sasa haya ndio msingi wa kusema kwamba utaratibu wetu kuna uchunguzi wa *corona*, kuna uchunguzi wa *commission of inquire* na kuna uchunguzi wa kijinai una mambo yake na utaratibu wake.

Lakini jambo kubwa katika hili Mhe. Mwenyekiti, na nawaomba na Waheshimiwa Wajumbe wafahamu sana, kwamba hivyo vielelezo ulivyokusanya kwa mujibu wa sheria ya *female procedure*, atakayeviwasilisha vile vielelezo ni kama aliyevikusanya au aliyevitengeneza, mwenyekiti atakuwa tayari kuwa ndio yeye akavitowe hivyo vielelezo mahakamani. Maana tukitumia ripoti ya kamati akawa mwenyekiti ndio mpelelezi, ina maana yeye ndio akasimame pale mahakamani athibitishe, yeye ndio awe shahidi. Sio utaratibu wetu kwamba Baraza au Mjumbe wa Baraza baada ya yale aliyoyafanya humu ndani ahalafu yeye ndio akawe shahidi akahojiwe na pale watakuhoji mawakili kwa utetezi. Maana ukimkuta mpelelezi anavyohojiwa utamuonea huruma. Sasa na Mwenyekiti tukisema yeye ndio mpelelezi, ripoti yake tunaipeleka pale akienda kuhojiwa na kuna watu kule. Maana moja katika *skill* za uwanasheria ni kumuhoji mtu ukamuudhi. Kwa hivyo, hayo ndio msingi wa kusema kwamba hapana, haya utaratibu wake jamani uko hivyo, tusitiliane shaka, tusiwe na kinyongo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni kuhusu hizi sheria za kazi,

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu umebakiza kama dakika 4 au utamalizia jioni.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Nitamalizia jioni.

Mhe. Mwenyekiti: Haya, ahsante lakini endelea kidogo ili tumalize muda kama dakika 4 halafu utaendelea jioni.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Suala la pili ni kuhusu sheria za kazi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema haya maamuzi tunayoyafanya mbali ya kutumia sheria na kanuni, lakini pia tumetumia uzoefu na busara. Uzoefu ni kwamba Mhe. Mwenyekiti, humu ndani ya hili Baraza takriban kila Mwakilishi ana kesi yake ya mfanyakazi aliyefukuzwa, aliyeachishwa kazi na sasa anataka arejeshwe kazini. Akiwemo Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Salmin Awadh Salmin, ana orodha yake ya wafanyakazi wa Shirika la Meli walifukuzwa siku nyingi.

Sasa kwa mujibu wa utaratibu wa sasa hivi uliowekwa katika sheria yetu ya *public service*. Kwanza anayefukuza kazi sio Waziri kama zamani, anayefukuza kazi sasa sio Katibu Mkuu kama zamani na wala sio Kamati ya Uongozi. Sasa hivi kuna *disciplinary committee* ambayo inaundwa na *service commission*. Unapokwenda pale kumshtaki mtu ili afukuzwe kazi ni lazima uende kama unakwenda mahakani ukiwa na ushahidi uliotimia, vielelezo vilivyotimia, ukajieleza na yeye ajitetee vile vile.

Kwa hivyo, ndio maana tukasema haya mengine si vyema wakati mwengine kuyasema hadharani, lakini ili ufanye hivyo ni lazima huyu mtu ama umsimamishe kazi na sheria yetu iko *very clear*, haijasema lazima umsimamishe kazi.

Kifungu cha 84 kinasema wazi kwamba:

"Unaweza kumsimamisha kazi".

Lakini ukimsimamisha kazi miezi 6, ni lazima uwe umeshamaliza uchunguzi na pengine umlipe na nusu mshahara. Usipothibitisha umrudishe umlipe na ule nusu mshahara aliokuwa hakuifanyia kazi. Masuala hayo yako mengi na tuna

kesi nyingi, serikali hii inapata hasara kwa taratibu hizo. Sasa unaposema mtu kahamishwa haizuwii uchunguzi kufanyika na hilondio lililokusudiwa na wala haizuwii uchunguzi wa kijinai kufanyika vile vile.

Kwa hivyo, mimi nilitaka nitanabaishe hilo kwamba kama tutatumia utaratibu wa kisheria uliopo wa kuwa ni lazima tumsimamishe mtu kazi, maana yake tujitayarishe kwamba hiyo ni hasara, tuna uzoefu wa hasara hizo na tuna uzoefu wa matatizo hayo. Sasa mimi nahisi hii ni njia nzuri ya kuweza kufanya uchunguzi na sheria hailazimishi Waheshimiwa. Kama sheria hailazimishi na tumeipitisha wenyewe, sasa tusiirekebishe kwa michango humu ndani, labda tuulete mswada rasmi ili tuirekebishe, lakini sheria inaruhusu kwamba anaweza akasimamishwa kazi na ni miezi 6 jumlisha na miezi 6.

Kwa hivyo, huo ndio utaratibu ambao unatumika na kwamba utaratibu wa sasa kusema ukweli kuja kuthibitisha kuna utaratibu wake ambao ni mgumu. Mhe. Mwenyekiti, imebaki hoja ya mwisho labda kwa sababu ya muda uniruhusu nije nimalizie jioni, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kwa kuwa muda wetu hautoshi. Kwa hivyo, kama alivyosema mwenyewe Mhe. Mwanasheria Mkuu, atakuwa ni mchangiaji wa mwanzo na baada ya hapo atakuja mwenyewe Mhe. Waziri na yeye kumalizia hoja hii.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuahirisha kikao hiki naomba kutoa tangazo moja. Mnadhimu wa CUF anatangaza kwamba anawataka Wajumbe wote wa CUF kubakia hapa baada tu ya kumaliza shughuli yetu hii.

Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuruni sana kwa utulivu wenu na tutaonana jioni saa 11.00. Ahsanteni.

(Saa 7:00 za mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

XXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXX

(Saa 11:00 Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa): Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea na

sasa tunamkaribisha Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kumalizia mchango wake.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nitangulie kukushukuru pamoja na kwamba ruhusa hii ilianza mapema, lakini naona Kiti kimebadilika, kwa hiyo na wewe naomba nikushukuru kwa dhati kabisa kwa kuendelea kunipa fursa hii.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa asubuhi nilizungumza maeneo matatu na nilisema labda nimalizie hili eneo la mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani tatizo letu kubwa tulilonalo tukubali kwamba ni utaratibu wetu wa kuwasilisha ripoti.

UTARATIBU

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 72 kuhusu idadi ya Wajumbe kuanza kwa kikao naomba kunukuu.

Kanuni ya 72(1) ya Baraza la Wawakilishi inaeleza hivi:-

> “Kiwango cha vikao vyote vya Baraza kitakuwa ni nusu ya Wajumbe wote”.

Lakini nikiangalia Mhe. Mwenyekiti nahisi Wajumbe bado hawajakamilia. Sasa nashauri bora tuangalie

utaratibu mwengine kwa sababu Wajumbe hawajakamilika kwa ajili ya kuanza kikao.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, sawa hoja yako ambayo umezungumza, lakini wakati wa kufanya kazi kwa Kanuni hiyo ni pale ambapo tunataka kupitisha hoja ya serikali. Kwa hivyo, kwa sasa bado tunaendelea kusikiliza maoni ya Waheshimiwa Wajumbe ambao wanachangia katika hoja, na tutakapotaka kupitisha hoja basi tutatizama hiyo *quorum*, na baadaye tutafuata utaratibu kwa kadri unavyotuelekeza. *(Makofi)*

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia hii Kanuni ya 72 inasema uhalali wa shughuli za mikutano na vikao vya Baraza na wala haikusema wakati wa kupitisha vifungu au wakati wa kuhoji, isipokuwa inasema uhalali wa shughuli za mikutano na vikao vya Baraza.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba uisome.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naomba uwashauri Makatibu wakusomee.

Katibu Mezani: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 72 (1) cha Kanuni ya Baraza la Wawakilishi kinaeleza hivi:-

Kifungu cha 72(1) cha Kanuni ya Baraza la Wawakilishi kinaeleza hivi:-

"Kiwango cha vikao vyote vya Baraza kitakuwa ni nusu ya Wajumbe wote".

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani tunaposoma Kanuni hii ya 72(1) tunasema inasomeka pamoja na Kanuni ya 71(2) kwa madhumuni ya ile hoja ya Mhe. Mbarouk Wadi Mussa. Kwa hivyo, aliyoitumia Mhe. Mjumbe ni Kanuni ya 72(2) ndiyo aliyoitumia kunyanyuka na kutoa hoja aliyoitoa. Sasa hiyo ni kama ulivyosema Mhe. Mwenyekiti, kwamba hii nafasi aliyoitumia yeye inaweza kutumika pale kabla ya kupitisha uamuzi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu arejee tena sijamfahamu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba katika Kanuni zetu kuna Kanuni ambazo ni amri na nyengine za kueleza utaratibu. Kwa hivyo, Kanuni ya 72(1) ni kweli inataka hilo litimie, lakini kulitilia nguvu kwake ni wakati gani ndicho ninachozungumza mimi, kwamba kulitilia nguvu kwake maana unaweza kuwa na maelekezo lakini maelekezo yoyote yanapovunjwa ina wakati ndipo ambapo inakuja tunasema *sanction* au kama ni adhabu ama ni *remedy*.

Sasa Kanuni zetu zinavyotuelekeza wakati wa kuleta hoja hiyo basi ni pale palipoelekezwa na fasili ya pili kabla ya kupitisha uamuzi, yaani kama ulivyosema

wewe Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, hii maana yake nini? Ni kwamba imeanza tokea asubuhi na hichi ni muendelezo wa kikao ambacho kimeakhirishwa asubuhi na tulikuwa na *quorum* na hivi sasa tunaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kama mtu anataka ku-*object* kusipitishwe uamuzi ndipo hapo fasili ya pili inavyotuongoza ni wakati gani sasa wa kuhakikisha kwamba hili la kwanza limetimizwa, ni wakati huo na sio wakati huu bado haujafika na utafika, na kama Mhe. Mjumbe akiwa na subira nadhani hili analolisema litafika wakati wake atalieleza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu amejieleza vya kutosha nadhani tuendelee. Mhe. Mwanasheria Mkuu tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba nadhani tuna tatizo kidogo utaratibu wetu wa kuwasilisha ripoti. Kutokana na tatizo hili basi naamini linatufikisha pengine hapa tulipo hivi sasa kwamba upande mmoja unaona kuwa labda kazi haikufanywa, na upande mwengine unaona kwamba kazi imefanyika kwa ukamilifu wake.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba ripoti za kamati ni kitu muhimu sana sio kwa Baraza tu, lakini kama alivyotangulia kusema Mhe. Waziri wa Ardhi,

Makaazi, Maji na Nishati kwamba hata kwetu sisi serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nilihakikishie Baraza hili kwamba hii ripoti si ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, na wala hakuitayarisha Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais peke yake, isipokuwa imetayarishwa na serikali yote nzima pamoja na kuidhinishwa na serikali na wala sio kukaa muda wa nusu saa, ni kutwa nzima na usiku wake kwa ajili ya kujadili ripoti hii na mpaka ikafika hapa tulipofika. *(Makofi)*

Sasa tunapofika pahala tukaona kwamba tuna tatizo labda mpaka wengine tunasema kuwa ripoti hii ni ya ubabaishaji, na wengine tunasema ya kuondoa njiani. Kwa kweli ni vitu ambavyo havielekei kwa sababu havina msingi wa kuwa hivyo ilivyo, lazima kuna tatizo ambalo pengine hatujakubali kwamba hili ndio tatizo letu.

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine haya maneno peke yake yanaweza kuwagombanisha kweli kama hamuaminiani, na kama munaaminiana kwenye maneno unaweza ukateleza na bado mukawa musigombane, lakini kama hamuaminiani basi munaweza kugombana kwa kuteleza maneno tu. Kwa mfano; watu wamegombana mtu kamuita mpenzi wake *dear* kwa Kiingereza, lakini kakosea *spelling* akaandika ile ya paa *deer*. *(Makofi)*

Kwa hivyo, huo ni ugomvi mkubwa Mhe. Mwenyekiti, kutoka kwa mpenzi mpaka ukamuita swala au sijui paa, lakini ugomvi huu umekuja tu kwa sababu wenyewe tu hawaaminiani, na kama wanaaminiana basi angejua tu ah! Huyu kateleza tu. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, na sisi ninachoamini ni kwamba niungane na hoja ile aliyosema Mhe. Hamza Hassan Juma labda kuna pahala inabidi turekebishe. Kwa kweli mimi naamini kwamba ripoti hizi zitakuja labda zitapelekwa kwenye kamati na kujadiliwa kama tunavyojadili mswada, basi yale ambayo yanahitaji ufafanuzi kabla ya kuja hapa, maana yake hapa ni muda mdogo au hapa muda wa kuisoma hiyo ripoti yenyewe ni mdogo, muda wa kuitafakari mdogo na hata muda wa kuieleza pia ni mdogo.

Kwa hivyo, mimi fikira yangu ni kwamba tunalo tatizo la msingi na tatizo hili linafanya hizi ripoti za Kamati kweli zisiwe na tija, lakini hazina tija si kwa sababu serikali imedharau, isipokuwa tunafika pahala namna au imekuwa kama kuja kusema kwamba *ok* tulichofanya hichi tunakikataa, lakini unakikataa kwa sababu ya msingi wa kwamba namna kilivyowasilishwa,wakati uliotumika kwenye kuwasilishwa una mashaka kusema kweli.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wetu katika hili kusema kweli una mashaka, ndio maana tunafika pahala tunasema aa! Labda tubadilishe Kanuni zetu tuwe na Mnadhimu wa *Backbenchers*, Mhe. Mwenyekiti

nadhani huko tutakuwa tunapotea zaidi, maana vyama vina wanadhimu kwa sababu vina sera, lazima sera za vyama zisimamiwe na ndio maana Mnadhimu kazi yake ni kuhakikisha kwamba yale yaliomo katika Sera na kwenye Ilani ya vyama vyao yanasimamiwa.

Sasa leo ukiwa na Mnadhimu wa *Backbenchers* sijui itatumika sera gani, nadhani sera itakayotumika ni kujenga msimamo na wala nchi haziendeshwi kwa misimamo Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, nchi zinaendeshwa kwa *vision*, mtazamo sahihi, na mitazamo hii ikawa ni ya pamoja, yaani ni *shared visions,* na haya katika historia Mhe. Mwenyekiti yametokea. Waingereza walikuwa na *situation* hiyo hiyo, kwamba Wabunge wakajenga misimamo mpaka wakaiondoa serikali mwaka 1649.

Lakini baada ya kuiondoa wakakaa na kuchukua nchi wakaondoa Ufalme wakaweka Jamhuri chini Oliver Cromwell, lakini yule bwana akafa mwaka 1658. Sasa yeye ndiye aliyekuwa *vision* yake, yaani aliyekuwa akiwaburuza pamoja kuwa msimamo, maana sera ya muungano wao ule ulikuwa wa yule mtu mmoja, na ndio maana alipokufa baada ya miaka miwili wenyewe wakarudi wakaenda wakamtafuta mfalme akaja akawatawala tena. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, nasema kwamba lolote tunalofikiria tayari limeshatokea kwenye historia, kwa hiyo lazima katika mambo ya nchi tuamue kwa busara, kwa kufikiria mbele pamoja na kwamba sote mwisho

wa siku Baraza hili, serikali sote kazi yetu ni kuijenga nchi hii pamoja na kuwatumikia watu wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, lazima tutafute utaratibu Ripoti za Kamati ziwe na tija, na kwa kuanzia kuwa na tija, basi lazima tuwe na utaratibu unaoridhisha wa kuziwasilisha na tukaelewana wapi pamepungua na wapi hatujaridhika, maana tukisema hatujatosheka Mhe. Mwenyekiti, kwamba kutosheka kuna matatizo yake, ndio kila mtu atatizama kwa lile analoliona yeye. Kwa mfano, mwengine ripoti mpaka iwe kubwa na mwengine fupi ndio yeye anatosheka. Sasa haya ni mambo ambayo yanaweza yakatupeleka pahala tukakosea. *(Vicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, nadhani kitu cha msingi nashukuru Waheshimiwa Wajumbe wengi hapa wamesema kwamba yapo mambo yametekelezwa, na mengi ambayo yamelalamikiwa mimi ninaamini ni kwa sababu hatujapata *forum* ya kuelezana na kufahamisha busara pamoja na utaratibu uliotumika ndio tatizo kubwa.
Lakini la pili ni kwamba hii Ripoti ya Kamati utekelezaji wake ni endelevu; yaani kuna mambo mengine huwezi kusema kwamba leo tumeyatekeleza na tumeyakamilisha.

Mhe. Mwenyekiti, nasema pa kuanzia kwanza tupitishe ripoti tuipokee na tuseme yale ambayo kuna mambo haya serikali ilete taarifa kwa sababu imo ndani ya kanuni zetu kwamba tunaweza tukaleta taarifa ya hili

hili, kwamba hapa haya yalitekelezwa na hivi sasa hii ni taarifa kwa yale ambayo yalibakia au Wajumbe walionekana kutoridhika.

Lakini tukasema ah! Ripoti hii tunaikataa, mimi nasema tutakuwa tunatibu maradhi yetu kwa dawa za kienyeji na sisi hatuugui maradhi ya kienyeji, isipokuwa sisi tunaugua maradhi ya kisayansi, na lazima tupate dawa ya kisayansi ndipo tutapoweza kupata namna gani ya kuweza kuendelea, kwa sababu haya yatakuwepo tu na tukisema tunasusia hata Kamati Teule hatutaki tena ni kwa sababu hatujajua tatizo liko pahala gani.

Kwa hivyo, kusema kweli kwa dhati kabisa nadhani kwamba Ripoti za Kamati kwa umuhimu wake, kwa msaada wake kwa serikali basi lazima ziwe na tija, na vizuri tutafute utaratibu wa kuziwasilisha ndani ya Baraza kwa njia ambayo italeta tija, tutafahamiana pamoja na kuelekezana, na tukafika pahala ambapo tunaafikiana, lakini kusema tunakataa ripoti, hatuundi tena Kamati Teule hiyo si suluhu, isipokuwa hiyo itakuwa tunatumia miti shamba kutibu maradhi ambayo yanahitaji uchunguzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono taarifa hii na ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe waipokee hii ripoti, na mule ambamo munahitaji taarifa zaidi, basi serikali ilete taarifa zaidi hapo baadaye na tuweze kuendelea kuwatumikia wananchi wetu kwa tija kutokana na fedha hizi ambazo wamezitumia kwa ajili

ya hizi Kamati ambazo zimeundwa na kufanya kazi vizuri. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia na kutuwezesha kuendelea na mjadala wetu huu vizuri, naamini Waheshimiwa Wajumbe kwa njia moja ama nyengine wameanza kuelewa kwa undani hatua ambazo imechukua.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi ya kuja kufanya majumuisho ya Taarifa yetu tuliyoiwasilisha katika Baraza hili.

Aidha nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote wale waliochangia na wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia, lakini sote tunakuwa na mtazamo mmoja; kwa nia ile ile ya kujenga pamoja na kutafuta ufumbuzi wa matatizo yetu, ili tuweze kuendesha nchi yetu vizuri kwa manufaa ya watu wetu. Naamini yote yaliyosemwa nia yake ilikuwa ni hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba uniruhusu niwataje wale waliochangia taarifa hii.

1. Mhe. Fatma Mbarouk Said (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na

Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*)

2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Asha Bakari Makame
4. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
5. Mhe. Ali Salum Haji
6. Mhe. Hija Hassan Hija
7. Mhe. Abdalla Moh'd Ali
8. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
9. Mhe. Mohammed Haji Khalid
10. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
11. Mhe. Omar Ali Shehe
12. Mhe. Salmin Awadh Salmin
13. Mhe. Marina Joel Thomas
14. Mhe. Hamza Hassan Juma
15. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
16. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria
17. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
18. Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati
19. Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Kazi na Utumishi wa Umma na
20. Mhe. Mwanasheria Mkuu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kutoa ufafanuzi wa kina naamini kwa kiasi kikubwa kazi yetu wameifanya, hivyo mimi nije hapa niwaombe tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba tumalizie vyema suala letu hili ambalo tumelianza kwa nia ile ile na madhumuni ya kuwatumikia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imefanya wajibu wake. Wajibu ambao umetumwa na Baraza hili tukufu ndani ya serikali Mhe. Mwenyekiti hatuwezi hata siku moja kudharau maagizo ya Baraza, pia hatuwezi hata siku moja ndani ya serikali kufanya ubabaishaji wa maelekezo ya Baraza hili, na wala hatuwezi kufanya upendeleo ama jambo jengine lolote kinyume na Baraza hili. Kwa kweli sisi ndani ya serikali na Baraza hili tunazungumza lugha moja, tena lugha ya kuwatumikia wananchi. *(Makofi)*

Kwa kweli nataka nimuunge mkono sana ndugu yangu Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwamba inawezekana kabisa pengine kuna baadhi ya vipengele hatukuelewana tu kwa kutofahamu madhumuni halisi yaliyokusudiwa, lakini naamini baada ya maelezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Mawaziri basi tumekaa katika *position* nzuri ya kuelewa hasa nini kipo, undani wake pamoja na muelekeo wake.

Kwa hivyo, nia yetu ni moja, na hata siku moja serikali hii haitafikiria kufanya kazi peke yake, isipokuwa tunafanya kazi kwa pamoja kwa maslahi ya watu wetu, tukiamini kabisa kwamba waamuzi wa mambo yote ya nchi hii ni wananchi wenyewe. Kutokana na hali hiyo, wanatupima sote, yaani wanaipima serikali, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kila tunalolisema, tunalolifanya wanatuona na watu wanatujua. Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba wao ndio wanaoweza kutuhukumu siku ikifika ya kutuhukumu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe kuna ndugu zangu ambao walisema kwamba hii ni taarifa ya Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, lakini Mhe. Mwanasheria Mkuu amelieleza vizuri, kwamba taarifa hii Mhe. Mwenyekiti ni Taarifa ya Serikali, yaani ni uamuzi wa pamoja. Na kama alivyosema kwamba ulifanyiwa kazi sana na sio tu katika Baraza la Mapinduzi lakini serikali iliunda Kamati Maalum iliyowashirikisha wahusika wote, ili kila sekta kuona lile ambalo liliagizwa na Baraza hili kwa nia ya kulifanyia kazi pamoja na kulitekeleza na yale ambayo yalihitaji ufumbuzi wa awali basi hatua zimechukuliwa.

Ni nia ya serikali kuyatekeleza maagizo yote; kwa sababu ukitizama pale katika ripoti yetu tumesema kabisa kwamba tunakubaliana na hili na tukatoa namna ya utekelezaji, kwa sababu serikali ndio inayosimamia suala la utekelezaji na ndio Katiba yetu ndivyo inavyotuelekeza kwamba kila mamlaka ina majukumu yake pamoja na wajibu wake wa kufanya.

Kwa hiyo, kama serikali ina wajibu huo basi inatekeleza kwa kuhakikisha kwamba misingi ya sheria, taratibu zilizopo pamoja na haki za watu wetu zinaheshimiwa, ili uamuzi uwe haukuleta upendeleo wala haukumuathiri mwengine, isipokuwa uwe uamuzi wa haki, na kila mmoja auamini kwamba nia ni kutenda haki.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la msingi hapa tukubali tu kwamba sisi ni wamoja na nia yetu ni kufanya kazi kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Waheshimiwa Mawaziri waliyaeleza mengi katika mambo haya. Nia yetu ya kufanya shughuli hizi za kuunda Kamati Teule ama shughuli nyengine zozote za uchunguzi, madhumuni yake ni kurekebisha pale palipokosewa, na maamuzi yanayotoka ni yale maamuzi yanayolenga katika kuondoa tatizo na kuweka lililo sahihi kwa maslahi ya watu wetu.

Sasa tunaposema tusiletewe au hatuhitaji kufanya ripoti nyengine itakuwa kidogo tumetizama kwa mtazamo tofauti, kwa sababu yale ambayo yameoneshwa na Ripoti za Kamati yametekelezwa na matokeo yake nimemsikia leo asubuhi hapa Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati akieleza kwa kina mafanikio yaliyopatikana katika Shirika la *ZECO* mwaka mmoja nyuma hayakupewo mafanikio hayo, lakini kutokana na busara pamoja na hekima zenu Waheshimiwa Wajumbe basi mabadiliko yametokea. *(Makofi)*

Vile vile nataka niseme sio *ZECO*, isipokuwa taasisi zote za serikali zimejirekebisha sana, watendaji wa serikali wamejirekebisha na lazima tukubaliane tunatoka mbali na yalikuwepo matatizo mengi na wala hatuwezi kuyamaliza kwa pamoja, isipokuwa ni hatua kwa hatua, na huo ndio wajibu wa serikali.

Kwa kweli serikali ni endelevu na wenzetu wamefanya kwa kiwango fulani na wamemaliza yaliyokuwepo mwanzo na wakarekebisha matatizo yaliyokuwepo nyuma, na wakafikia hatua waliyofika, na sisi tumekuta matatizo yapo na tunachukua hatua, kwa yale ambayo tunayaweza kuyakamilisha sasa basi tunayakamilisha, na yale ya muda wa kati tutayafanya kwa muda wa kati, na kwa yale ya muda mrefu tutayafanya kwa muda mrefu.

Lakini nia ipo pale pale ya kuwatumikia wananchi na tayari hatua zimeanza. Kwa mfano, Waheshimiwa Wajumbe haya mambo yanayochukuliwa ya kisera, ya kisheria ya kuunda taasisi mbali mbali ikiwemo Taasisi ya Rushwa maana yake ni kupambana na maovu na ubadhirifu katika serikali. Kwa hivyo, serikali hata siku moja haiwezi kumlinda au kumpendelea anayetenda maovu, lakini tunaweka misingi ya kuondoa matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba tuelewane na nimshukuru sana mama yangu Mhe. Asha Bakari Makame alisema kuwa tuwe wakweli, pale kwenye kasoro basi tuseme kasoro zenyewe na pale ambapo pamefanikiwa tupongezeni na pale ambapo hapajakamilika basi unasema hapajakamilika.

Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti kwamba tukubaliane katika mambo haya ya msingi ambayo nia yetu ni

kuendeleza, kwa sababu kuna maneno mengine hapa tunapoyasema basi mujue kwamba tunaifitinisha serikali kwa wananchi wakati ina nia njema. Kwa mfano, ukisema serikali imebabaisha ripoti hii, maana inaonekana serikali hii haitekelezi wajibu wake, wakati tumefanya kazi na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ameeleza hapa na mimi ninazo takwimu hapa.

Kwa maana hiyo, si vyema hata kidogo kuifitinisha serikali kwa wananchi wake, kwa hiyo ni vyema tufanye kazi kwa pamoja kwa kuwa sote ni wamoja na mambo haya sisi leo tupo mbele haya, lakini kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Kazi na Utumishi wa Umma asubuhi hapa kwamba Mwenyezi Mungu atuweke mbele, lakini mambo haya yana mabadiliko, leo tupo sisi na kesho mutakuja wenzetu ndio utaratibu wenyewe huo. Mhe. Mwenyekiti, tuliopo leo sio waliokuwepo jana, na watakaokuwepo kesho ni wengine.

Hivyo, ni vyema tukubaliane kwamba mabadiliko yapo kila wakati na hii nchi yetu pamoja, sasa kwenda tukafika pahala tukavunjana moyo hata yale mambo mazuri tunayoyafanya si vizuri hata kidogo. Kwa maana hiyo, lazima tukubali kwamba tunapofanya kosa basi tuambiwe hili ni kosa, na pale tunapofanya jema, basi na jema nalo liwe *appreciated* tupongezwe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri pamoja na watendaji wa serikali, wanafanya kazi nzuri na wala sisemi kama hakuna makosa ndani ya serikali yapo, lakini nia yetu ni kurekebisha na hivi tunavyoshirikiana ndivyo tunarekebisha. Kwa hiyo, ninakuombeni wenzangu Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba tulielewe hili.

Hata hivyo, nisingependa kurudia ambayo wenzangu tayari wameshayazungumza sana, lakini hili suala la kwa nini Polisi wafanye uchunguzi ambalo limeelezwa sana na wala sina haja ya kulirudia, kwa sababu ni utaratibu uliopo kisheria kufanya vile.

Mhe. Mwenyekiti, juu ya hivyo bado na watendaji wenyewe wa *ZECO* wameleta malalamiko serikalini kwamba hawakupata fursa na wao kutoa maoni yao vya kutosha, licha ya kuundwa kwenye kamati mbali mbali. Sasa hapo watakapokwenda Polisi kufanya uchunguzi watapata nafasi ya kueleza kwa kina yale ambayo wao wanayaona hawakupata kutoa ushahidi wao ili kuisaidia Polisi.

Mhe. Mwenyekiti, hata na sisi wenyewe watu wa ZECO wametulalamikia pia. Wametwambia sisi tumewabana wao tu, lakini na sisi Waheshimiwa hatukujitaja, kuna wengine humu pia tumeunga umeme kinyume na utaratibu, tumeuziwa magari kinyume na utaratibu, na wengine wamekwenda mbali zaidi kuna mambo mengine yamefanyika ambayo na wao wanahitaji wayaseme.

Kwa hiyo uchunguzi ule ukiendelea utawawezesha na wao kutoa dukuduku lao, kutoa na maoni yao, *sheria ni msumeno*, sio wao

hata sisi kama tuna makosa itatukumba. Kwa hivyo tulioshiriki kuunga umeme kinyume na taratibu nayo itatukumba, tuliouziwa magari chini ya bei tukauza kwa bei ya juu itatukumba, tuliodai rushwa kwa kuwakaripia itatukumba. Kwa hiyo tusilaumu ndio tunataka kusafisha, kama hatukufanya kosa ndio itakayotusafisha kutuweka sawa sisi Waheshimiwa sote. Malalamiko hayo wanatulalamikia kwa nguvu zote.

Mimi napenda Waheshimiwa haya maamuzi ambayo serikali wamekuja nayo tuyaunge mkono kwa nia njema ili tusafishe pale penye makosa, turekebishe na sasa tujenge mstari mwengine wa kuhakikisha kwamba watendaji wetu wawe wasafi na kila mmoja awe msafi ili nchi ipige hatua zaidi.

Naamini hizi jitihada tunazozifanya tusivunjike moyo hata kidogo; ni jitihada kubwa zimeleta mafanikio, mmefanya kazi kubwa Wajumbe wa Baraza hili na matokeo yake mnaanza kuyaona ni kama yale aliyoyataja Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban; Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pale asubuhi. Kwa hivyo nawaomba sana jamani tushirikiane, tufanye kazi kwa pamoja ili matokeo yawe ni yetu sote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa humu inabidi yale yote ambayo yamesemwa nisipende kuyarudia rudia niseme yale ambayo kwa kiasi fulani hayakuzungumzwa.

Lipo suala ambalo lilizungumzwa hapa Mhe. Mwenyekiti, kuhusu risiti zilizolipwa malipo madogo kuliko ambavyo yangelipwa. Tatizo lazima na sisi hapa tujiambie wewe umekwenda kulipa fedha umelipa milioni moja ukapewa risiti ya laki mbili ukakaa nayo nyumbani ukaiweka, mkakaa wewe na mkeo mnaitizama tu mpaka siku inayokuja Kamati ndiyo unasema mimi nimelipishwa fedha nyingi, wakati ulikuwa na nafasi ya kuripoti, ukienda polisi au mahali pengine popote hata kwenye taasisi za serikali kueleza bwana mimi nimelipa milioni moja lakini nimepewa risiti ya milioni mbili, watendaji wenu

wezi, mbona mlinyamaza kimya muda wote huo, madhumuni yake yalikuwa nini? Hapa ni lazima tujue, hapa kuna mazingira ya rushwa, aliyetoa hizo pesa pia na yeye tumsaili, kwa nini na yeye hakusema.

Ndiyo maana tukataka polisi hawa watu tuwaulize watueleze, unakaa nayo nyumbani kwani *certificate* ile? Umelipa pesa nyingi wewe zaidi ya pesa ulizozitoa, risiti unapewa ndogo, jamani haya mambo mengine tujiulize. Kuna mambo ambayo ni lazima tufike mahali tujiulize kwamba hizi zinaleta mazingira ya rushwa.Ikishafika hali hii lazima wachunguzwe wote wawili, haiwezekani unatoa milioni kumi unapewa risiti ya milioni moja na wewe unakubali. Lazima haya mengine jamani tujiulize na sisi wenyewe, tusiwe kila tunaloambiwa tunalikubali tu.

Kwa hivyo hili naona upo umuhimu wa kulifuatilia zaidi na kuona tatizo liliopo. Kuhusu uhamisho umezungumzwa vizuri na nisingependa nirudie kwa sababu Mawaziri wametoa ufafanuzi mzuri kwa adhabu hiyo ya uhamisho na ilikuwa na nia mbili.

Moja ni kumkosesha kile alichokipata alipokuwa katika nafasi hii. Lakini la pili ni kutupa nafasi ya kuchunguza pale alipokuwepo yale ambayo yapo kama kuna madhambi zaidi tutaona, kama hakuna dhambi basi. Kwa hiyo utaratibu uliofanyika naomba Waheshimiwa tukubaliane uhamisho. Msingi wetu ni wa nia safi kwa nia kwamba kwanza unamkosesha kama hayo anayoonekana akiyapata.

Lakini la pili tunapata nafasi katika uchunguzi unaofanyika kujua nini cha kufanya na kama kuna makosa zaidi tuweze kuelewana.

Kwa sababu ndiyo hiyo inayoonesha wazi kwamba mteja anamuamini mfanyakazi kumpa fedha ili ampatie huduma katika Shirika la Umeme. Sasa huyu kumpa fedha pale hajafanya kosa kumuamini huyu, kosa huyu ni kwamba mfanyakazi wa Shirika

kwa vyovyote fikra itakayokuja na dhana itakayokuja kwamba huyu atazinunua huduma kwa bei sio sahihi, ndio dhana tutakayoipata. Ndio tunasema kule mgongano wa maslahi, kwamba tukimchunguza huyu tutapata ukweli ndani yake tujue liliopo ndani yake tujue liliopo ni lipi zaidi, na kama sasa baada ya uchunguzi huo kuonekana unatusaidia kuwa na ushahidi wa kupeleka mahakamani.

Kwa hivyo yote tuliyoyafanya ndani ya serikali Waheshimiwa hatukufanya vyengine vyovyote isipokuwa kwa nia njema ya kutafuta suluhu njema ya kuondoa matatizo yaliyopo na kujenga misingi mizuri kwa watendaji wasirudie kufanya makosa ambayo hayatakiwi kufanywa na wafanye mambo yao kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa za kisheria.

Kuhusu wafanyakazi wa GECCO wakawa wapo na ZECO ndio huo mgongano wa maslahi, na kwa sababu kulikuwa hakujawekwa utaratibu mzuri, ndio maana hawa wakapata nafasi ya kuwa wapo kwenye Shirika la Umma, na wakati huo huo wakawa wanafanya shughuli katika Shirika binafsi. Lakini sasa kutokana na hali hii licha ya kurekebisha sheria zetu, lakini pia tunakuja na utaratibu wa maadili ya viongozi ambao katika maadili hayo pia yatawakuta na wafanyakazi ili utaratibu wetu uwe mzuri, tusitumie fursa zetu katika nafasi zetu za kazi tukajifanyia mambo yetu binafsi. Sasa ni lazima tuvumiliane wakati tunafanya shughuli hii kwa nia ya kurekebisha.

Kuhusu suala la ajira ya watu 16 iliyokosa idhini ya Bodi. Mimi niseme tu kwamba uajiri wa watu 16 uliofanywa na uongozi wa Shirika mwaka 2008 bila ya idhini ya Bodi ya Wakurugenzi, haukufanywa chini ya Uongozi wa Meneja Mkuu huyu tuliyenaye sasa hivi. Huyu anabeba lawama kwa sababu ya makosa yaliyofanyika nyuma. Meneja Mkuu huyu tayari amepewa barua za maonyo na ameitwa na serikali na kuambiwa kwamba bwana kuna matatizo haya yametokea, kwa hivyo tunataka mambo kama haya yasitokee tena na urekebishe Shirika

liende vizuri. Matokeo yake tumeona hapa, tumeambiwa hapa tulivyopiga hatua katika Shirika.

Kwa hivyo kumuhukumu Meneja Mkuu huyu kwa sasa kwa sababu ya kuwaajiri watu 16 yeye siye aliyewaajiri, lakini kwenye uongozi umebeba dhamana ya uongozi. Kwa hivyo Waheshimiwa tuone naye umakini wake wa utendaji, amefanya kazi kubwa sana katika kuliimarisha Shirika hili. Adhabu aliyopewa nahisi inatosha lakini bado uchunguzi unaendelea, kama kuna makosa mengine ataonekana nayo basi hatua nyengine zitafuata na hivyo hivyo kwa wafanyakazi wengine, sio tu uhamisho lakini bado na hatua nyengine zinaendelea kwa wale watakaoonekana wana makosa haya na yale hatua zitachukua nafasi yake, na wakati huo huo kesi zinakwenda kwa DPP yeye sasa atatuonesha kwamba hii kesi ya jinai, hii ya madai, huyu ana kesi, ili utaratibu uchukue nafasi yake.

Mimi naamini kwa msimamo huu ambao Baraza letu linauonesha hatua hii mnayopiga katika kurekebisha mambo wala tusiwe na wasi wasi Waheshimiwa, marekebisho ndani ya serikali yanafanyika katika nchi yanafanyika na hatua zinafikia. Cha msingi tuelezane maneno ambayo yatasaidia katika kujenga, yatawasaidia wananchi wetu kuwaweka wamoja. Kuna baadhi ya maneno hapa yanaposemwa yanaleta vurugu huko chini kwa wananchi, tunapata simu nyingi toka jana. Kwa hivyo tujue kabisa itakayohukumiwa sio serikali tu na Wawakilishi pia tunahukumiwa kwa maneno yetu na kila kitu. Kwa hivyo ni vizuri sisi wanasiasa tunayoyafanya yote tuyafanye kwa nia na maslahi ya nchi kwa maslahi ya taifa. Pia na sisi wenyewe tuwe watu wamoja, tushirikiane, penye kosa tuambizane, penye kasoro turekebishe ili tujenge nchi yetu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa sina mengi zaidi ya kusema baada ya maelezo mbali mbali yaliyotolewa na Waheshimiwa wenzangu, isipokuwa niwambie tu kwamba serikali hii haijafeli na wala haitofeli, imejiandaa kufanya kazi kwa kuwatumikia

wananchi kwa uadilifu mkubwa sana ndio nia na dhamira yetu. Tutafanya kila namna kuhakikisha wananchi wanapata maendeleo makubwa katika nchi yetu. Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na hoja yako pamoja na hoja za Wajumbe wote zilizowasilishwa umeweza kuzitolea ufafanuzi kwa kushirikiana na Mawaziri wenzako. Sasa tuwahoji Wajumbe wanaokubaliana.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, Baraza letu linaendeshwa kwa mujibu wa taratibu na heshima kubwa ya Kiti ambacho umekikalia. Mhe. Mwenyekiti, utaratibu ninaoueleza unahusu Kanuni ya 77(1) naomba noisome, inasema

"Baada ya kumaliza majabadiliano juu ya suala fulani iwe katika hali yake ile ile ya mwanzo au imebadilishwa kama itakavyokuwa suala hilo litatolewa na Spika, kwa ajili ya uamuzi wa Baraza kwa Spika, kusema wale wanaokubali wanyooshe mikono yao juu na hapo Spika atahesabu idadi ya Wajumbe walioonesha mikono kukubali, halafu atasema wale wasiokubali waoneshe mikono yao juu. Spika, tena atahesabu idadi ya Wajumbe walionyosha mikono yao juu kukataa. Na baadaye fasili ya pili mpaka ya saba zinamalizia utaratibu mzima ambao utafuata."

Mhe. Mwenyekiti, nimeinuka kuzungumzia kuhusu utaratibu kwa sababu hapa amezungumzwa Spika, lakini kwa mujibu wa kanuni zetu hizi tafsiri ya Spika, kama ambavyo ipo katika Kanuni ya Pili ukurasa wa nne pale inaonesha kwamba Spika, ni pamoja na yule ambaye amekalia kiti chake.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona ninyanyuke kabla hujatuhoji kwa sababu siku ya Ijumaa wakati ripoti hii ilipowasilishwa

tumenyanyuka baadhi yetu kuomba muongozo wa Spika, na akautoa kuhusu namna ya kutuhoji na hapa Mhe. Spika, ninayo *hansard* ya muongozo au uamuzi ambao Spika aliutoa; naomba niusome kwa ufupi tu, kwanza alizungumzia namna ya kutuhoji juu ya utekelezaji wa taarifa ile ya PAC, ambapo alisema naomba ninukuu sehemu hii.

"Basi mimi nadhani isilete matatizo, tuendelee kujadili kama inavyoelekezwa na kanuni zetu na hatimaye tuone utekelezaji huu wa serikali unatosheleza au laa, ambapo mwisho nitawahoji Waheshimiwa Wajumbe namna mlivyopokea mafungu yote au sehemu Fulani, kama utekelezaji wake unatosheleza au hautoshelezi mtaielekeza serikali vyenginevyo"

Baadaye Mhe. Spika, nilipoomba muongozo zaidi maelezo yake ya kufungia ya mwisho Mhe. Spika, alisema hivi:-

"Nafikiri sina muongozo mwengine zaidi ya kwamba tuendelee kujadili na hatimaye Wajumbe mtaamua jambo gani ambalo utekelezaji uliowasilishwa hapa umetosheleza, na jambo lipi ambalo kwa maelekezo mtakayotoa linahitaji kufuatiliwa zaidi na hatua kuchukuliwa. Mimi nafikiri tuendelee kujadili kama ilivyo na hatimaye nitawahoji Waheshimiwa Wajumbe namna gani mnaridhika na taarifa hii iliyotolewa na serikali, Utekelezaji wa Maamuzi ya Baraza yaliyofanywa huko nyuma" Halafu akamtaka Mhe. Makame Mshimba Mbarouk aendelee.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nimeona niisome kwa kutumia Kanuni hiyo na kukumbusha utaratibu kwamba Spika, ameshatuamulia siku ya Ijumaa kwamba tutahojiwa juu ya kifungu kwa kifungu cha utekelezaji wa ripoti ile, kwa sababu ilianza kuonesha wasi wasi kwamba yapo maeneo ambayo kuwa tumeridhika na yapo maeneo ambayo pengine hatukuridhika na tukawa tumeelekeza vyengine.

Kwa hivyo nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu umekalia kiti cha Spika, na yeye alishautoa muongozo huo, tuufuate muongozo huo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nilikuwa namsikiliza sana ndugu Mjumbe alipokuwa akitoa maelezo yale ambayo yalikuwa yamezungumzwa na Spika. Lakini Mhe. Spika, alipokuwa anatoa maelekezo yake na mimi pia nilikuwepo na nilimsikiliza kwa makini sana kwa sababu ni moja kati ya majukumu ambayo yanatupasa tuyafuate humu ndani.

Mhe. Spika, hakuelekeza kwamba tupitishe kifungu baada ya kifungu, katika hoja ambayo inaendelea, alichokisema Mhe. Spika, yale mambo ambayo tutahisi yanataka maelekezo au ufuatiliaji wa ziada basi tuangalie njia bora ya kuweza kuwatafutia muelekeo wake ili tuone namna gani serikali inakwenda kuyafanyia kazi kwa karibu zaidi. Lakini hatukuelekezwa utaratibu wa kupitisha kifungu baada ya kifungu, taratibu hizo zinahusu miswada au masuala yanayohusu bajeti.

Lakini katika taarifa za serikali tunalo jukumu kwa mujibu wa taratibu zetu kuwahoji Wajumbe wale ambao watakuwa wanakubaliana na hoja waunge mkono hoja, na wale ambao hawakubaliani na hoja na wao wanayo haki ya kusikilizwa. Lakini vile vile serikali kama serikali yale ambayo yatakuwa bado hayajaelekezwa vizuri au hayajafanyiwa kazi vizuri nahisi watakuwa na nafasi nzuri sana ya kuweza kwenda kuhakikisha kwamba yale ambayo yamezungumzwa na Wajumbe yanakwenda kufanyiwa kazi kwa maslahi ya nchi yetu na watu wetu kwa ujumla.

Kwa upande wangu Mhe. Mjumbe ninachoweza kuthubutu kufanya nitakwenda kwa mujibu wa taratibu za kanuni namna zinavyotuongoza, tuwaulize Wajumbe wanaokubaliana na hoja

wanyooshe mkono, na tutaangalia wingi wa kura zitakavyoelekeza. Naomba kuishia hapo, ahsanteni.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, si malengo yangu wala sikusudii wala sina mamlaka ya kubishana na kiti chako. Umesema kwamba na wewe ulimsikiliza Spika, lakini umetoa maneno kwa jinsi ulivyomfahamu, lakini mimi nimenukuu *hansard* na naomba niinukuu tena.

"Basi mimi nadhani isilete matatizo, tuendelee kujadili kama inavyoelekezwa na kanuni zetu na hatimaye tuone utekelezaji huu wa serikali unatosheleza au laa, ambapo mwisho nitawahoji Waheshimiwa Wajumbe namna mlivyopokea, mafungu yote au sehemu fulani kama utekelezaji wake unatosheleza au hautoshelezi mtaielekeza serikali vyenginevyo" Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nitoe ufafanuzi kidogo ili nimsaidie ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu, nataka nimuhakikishie kwamba serikali imekuwa ikisikiliza kwa makini kila mchango wa Mjumbe, na kila pale ambapo pameonesha pana malalamiko kwa Waheshimiwa Wajumbe tumepa-*note* vizuri, watendaji wetu wapo na wamesikia vizuri. Nia yetu ni kwamba pale pote penye kasoro tutakwenda kupafanyia kazi. Naomba akubali tu kwamba sisi tumeshafahamu yale yote yanayotakiwa kufanyiwa kazi na atuamini kwamba tutakwenda kuyafanyia kazi, tunaomba tukubaliane kwamba ripoti hii tuipokee kwa pamoja ili turahisishe shughuli zetu na tuweze kuendelea na shughuli nyengine Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sina matatizo, tatizo langu ni moja tu na hili nashukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu mara kwa mara amekuwa akituongoza kwamba chombo hiki tumekiwekea taratibu, na taratibu zake moja ni kuheshimu maelekezo ya Kiti. Sasa Kiti kiliamua wakati hoja hii inaanza,

iwe kwa jina lolote hoja au taarifa. Kama nilivyosema sitoi tu maneno kutoka kwenye kinywa changu lakini nanukuu *hansard* maelekezo ambayo Spika aliyatoa.

Hata ukisoma hii kanuni ya 77 Mhe. Mwenyekiti, inazungumzia namna ya kuhojiwa ni kwamba kuhusu suala fulani liwe katika hali yake ile ile ya mwanzo au limebadilishwa kama itakavyokuwa. Sasa huku kubadilishwa bahati sijui niseme nzuri au mbaya, lakini katika majumuisho yote serikali imejibu maelezo kwa ujumla wake haikutwambia katika michango ile ya Wajumbe kifungu kipi kimekubaliwa na Wajumbe, kifungu kipi kasema kwamba hiki tunakichukua na maelekezo ya Wajumbe.

Sasa tutakaposema kwamba tutaipokea kwa jumla hapa itakuwa maana yake kwamba tumepokea maelezo haya kwamba tumeyakubali yote. Lakini kama tungelikuwa serikali katika majumuisho yake imesema kutokana na majadiliano ya Wajumbe kwamba kifungu fulani tumeona Wajumbe wameridhika na sisi tumeafiki, na kuna kifungu fulani ambacho Wajumbe wameeleza hisia zao au mapungufu yao, hayo tumeyapokea. Lakini serikali haikufanya hivyo, majibu yake yalikuwa ya jumla, yapo maeneo machache mahsusi ambayo ndiyo waliamua kuyasema sana kwa mfano kama lile suala la ndugu Zakia aliyekuwa anatajwa.

Ndio maana najiuliza chini ya maelezo ya kanuni ya 77 na hasa baada ya muongozo wa Spika, ambao alitupa baada ya kuuomba katika Baraza hili siku ya Ijumaa, tutakaposema tuipokee tu ripoti kwa ujumla wake tutakuwa tumeitendea haki? Je, kwa mfano Wajumbe wakitokea kuikataa itakuwa tumeitendea haki vile vile serikali? Kwa sababu itakuwa kuna maeneo ambayo mengine tumeridhika nayo lakini sasa inatupa uamuzi mmoja tu kwamba ama tuikubali yote kwa ujumla au tuikatae yote kwa jumla. Naomba sana maelekezo yako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kama nilivyokwisha kusema mwanzo, Mhe. Spika hakukosea katika kutoa maelekezo yake. Tulipokuwa tunamsikiliza Mwanasheria Mkuu hapa amezungumza kwamba yapo mambo yatakwenda kufanyiwa kazi zaidi. Lakini na Waziri ambaye anahusika na sekta hii ya umeme naye vile vile amesifia na amewashukuru Wajumbe kutokana na kumzindua na kumuonesha namna gani taasisi anayoiongoza ilivyo. Haya yote tumesema kwamba yatasaidia katika kuleta ufanisi na kuona kwamba utekelezaji na haki na wajibu vinatimizwa kwa mujibu wa sheria. Haya yote tumeyasikia Waheshimiwa Mawaziri walipokuwa wakizungumza.

Sasa kwa sababu hoja yako Mjumbe ina msingi vile vile, lakini na sisi tunaongozwa na taratibu hizo hizo katika kuendeleza hizi Kanuni pamoja na Katiba na Sheria zilizomo humu ndani. Ninachokiomba kwenu kwa kukisaidia kiti, naomba niwahoji Wajumbe wanaokubaliana na hoja wanyooshe mkono na tuweze kuwahesabu wepi ambao wanakubali na wepi ambao wanakataa. Lakini baada ya hapo sio mwisho wa utekelezaji wa ripoti hii. Bado ripoti hii inatakiwa ikaendelee kufanyiwa kazi, pahala ambapo pana mapungufu pakafanyiwe kazi na baadaye tupate taarifa itakayoweza kututosheleza sote. *(Makofi)*
Baada ya maelekezo hayo sasa naomba niwahoji Wajumbe wale wanaokubaliana na ripoti hii wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa na kuamuliwa)

TAARIFA YA SERIKALI
KUHUSIANA NA BARAZA LA MANISPAA

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa niwashukuru sana sana Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa namna ambavyo wamepevuka katika eneo hili la siasa katika uvumilivu; katika kuangalia maslahi ya kuona wananchi wetu wanapewa kipaumbele. Mheshimiwa Baraza hili na Wajumbe wake ni la kupigiwa mfano mkubwa sana. Ni watu ambao wanasema hoja zao na wao vile vile wanakuwa na uvumilivu kusikiliza hoja za wengine na kufanya maamuzi sahihi, nataka niwapongeze sana na niwatakie kheri ya mafanikio makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Serikali kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa jinsi ulivyoliongoza Baraza letu hili hasa kwa kutumia busara na hekma kubwa ulizozionesha hivi sasa. Jambo ambalo limewezesha Baraza kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba kwa ufanisi mkubwa. Aidha nalishukuru Baraza lako tukufu kwa kuridhia kuundwa kwa Kamati Teule ya kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa.

Mhe. Spika, tulishukuru sana Baraza letu hili kwa kazi kubwa inayofanya. Vile vile nachukua fursa hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati Teule Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mwakilishi wa kuchaguliwa na wananchi wa jimbo la Magomeni pamoja na Wajumbe wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuibua hoja mbali mbali na kutoa mapendekezo juu ya hatua za kuchukuliwa na kuimarisha utendaji wa Baraza la Manispaa, na ambao Baraza hili tukufu limekubali ripoti hiyo na ikawa ripoti ya Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yalikuwa sahihi na yaliangaliwa kwa kina na serikali. Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Serikali tayari imeanza kuchukua hatua katika kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Baraza hili tukufu.

Mheshimiwa baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba uniruhusu kutoa maelezo kuhusiana na hoja mbali mbali zilizotolewa na Baraza lako kama ilivyoelekeza katika taarifa iliyowasilishwa katika Baraza hili. Mheshimiwa naomba kueleza.

Kuhusu hoja Namba 1. Mhe. Mwenyekiti, hoja hii ina maeneo sita yanahitaji kupatiwa maelezo kama ifuatavyo:-

1. Mikataba ya Baraza la Manispaa kusainiwa bila ya kufuata matakwa ya kifungu cha 20(2) ya Sheria Nam. 3 ya mwaka 1993.

2. Watendaji wa Baraza la Manispaa wakiongozwa na Mkurugenzi hawakufuata maadili ya kazi, Sheria na Kanuni za Baraza katika kuingia na kufunga mikataba.

3. Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa amekuwa akitumia madaraka yake vibaya kwa kuamua vile anavyoona inafaa.

4. Mwanasheria wa Baraza hakushirikishwa ipasavyo katika uundwaji na uandaaji wa mikataba mbali mbali.

5. Kifungu cha 20(2) cha Sheria Nam 3 ya mwaka 1995 kinachoeleza kwamba mikataba yote itakayoingiwa na Baraza itatiwa muhuri wa Baraza mbele ya Meya au Naibu Meya na Mkurugenzi wa Afisa mwengine wa Baraza atakayeidhinishwa kwa niaba ya Mkurugenzi kwa kibali au azimio la Baraza.

6. Vile vile Kanuni ya 55(b) ya kanuni za Baraza la Manispaa inaeleza kwamba mikataba itakayofungwa na Baraza ambayo thamani yake itazidi shilingi milioni tano ni lazima ipate kibali cha Baraza zima.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hoja hizo Kamati yako Teule ilitoa mapendekezo mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuchukuliwa

kwa hatua za kinidhamu na kisheria kwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa ndugu Rashid Ali Juma na kulitaka Baraza la Manispaa kutekeleza majukumu yake kwa misingi ya sheria na Kanuni za nchi, na mikataba yote ya Baraza inafungwa kwa kuzingatia sheria.

Aidha Kamati Teule imeishauri serikali hatua za makusudi kuhakikisha Madiwani na watendaji wa Baraza wanashirikiana ili kuleta tija inayokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hoja ya kusaini mikataba bila ya kufuata matakwa ya kisheria. Serikali imelitaka Baraza la Manispaa kurekebisha hali hiyo na kuipeleka mikataba yote iliyofungwa na itakayofungwa kuanzia sasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata ushauri na maelekezo, jambo ambalo tayari limeshatekelezwa. Aidha hivi sasa kila mkataba unaofungwa na Baraza la Manispaa utashuhudiwa na Meya ama Naibu Meya kwa kuweka saini yake katika mkataba huo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hoja ya watendaji wa Baraza wakiongozwa na Mkurugenzi kutofuata sheria na kanuni za Baraza katika kuingia na kufunga mikataba. Serikali inakubaliana na mapendekezo ya Kamati kwamba ingawa Baraza la Manispaa ni taasisi inayojitegemea, bado taasisi hii inatakiwa kutekeleza majukumu waliyopewa kwa kufuata misingi ya sheria na kanuni za nchi. Tayari serikali imeshaiagiza Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kuimarisha mazingira ya utendaji kazi wa Baraza hilo ili litekeleze majukumu kwa mujibu wa sheria na kanuni ziliopo. Aidha serikali tayari imempa maelekezo Mkurugenzi mpya wa Manispaa kuhakikisha kuwepo kwa ushirikiano wa kutosha baina ya Madiwani na Watendaji wa Baraza la Manispaa kwa lengo la kuleta ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti hoja namba 2 ya Baraza la Manispaa limefuta mikataba ya walioshindwa kutekeleza masharti ya mikataba bila ya kuwapa nafasi ya kujitetea. Mhe. Mwenyekiti Baraza katika maelezo yake juu ya hoja hii iliainisha kuwa masharti ya mikataba hayatekelezwi ipasavyo, kwa mfano kipengele cha 1(1) katika mikataba yote ya uwekaji mabango ambacho kinazungumzia kuhusu suala la muda kimekuwa kikitumika vibaya kwa upande mmoja kutoa maamuzi bila ya kuhusishwa upande wa pili, hali ambayo imepelekea kutokezea kwa maingiliano ya mikataba na kupelekea migogoro baina ya Kampuni za Matangazo na Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti mapendekezo ya Baraza kuhusu hoja hii ni kwamba hatua za kinidhamu na kisheria zichukuliwe dhidi ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa Ndugu Rashid Ali Juma na kulitaka Baraza la Manispaa kuzingatia sheria zinazoongoza mikataba. Mhe. Mwenyekiti sheria za mikataba zinataka kila upande ulioingia mikataba utekeleze majukumu yake. Endapo upande mmoja wa mkataba utashindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa masharti ya mikataba, ni wajibu wa upande huo ulioshindwa kuupa taarifa ya kushindwa kutekeleza majukumu ya upande mwengine. Kwa kuwa Kampuni zilizoingia mikataba ya kuweka mabango ya matangazo barabarani zilipewa muda maalumu wa utekelezaji zilipaswa kufuata muda, huona endapo Kampuni yoyote ilishindwa kutekeleza masharti ya mkataba ndani ya muda waliokubaliana ingepaswa Kampuni hiyo kutoa taarifa kwa Baraza la Manispaa na kuelezea sababu za kushindwa kutekeleza makubaliano hayo.

Hata hivyo serikali inakubaliana na pendekezo la Kamati kwamba Baraza la Manispaa lilipaswa kutoa *notice* kwa Kampuni iliyoshindwa kutekeleza makubaliano kabla ya kuchukuliwa maamuzi kwa Kampuni nyengine. Serikali tayari imeshaanza kuchukua hatua za kisheria kwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa kutokana na vitendo vyake vya kushindwa kufuata sheria na kanuni zilizopo nchini. Mhe.

Mwenyekiti serikali imekubaliana na mapendekezo ya Baraza ya kufuata sheria na kanuni katika uundaji na utekelezaji wa mikataba, tayari imetoa maelekezo kwa Baraza la Manispaa kuipeleka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mikataba yote kabla ya kusainiwa kwa ushauri na maelekezo zaidi.

Hoja namba 3: Suala la mabango, uendeshaji wake na mapato yake yanaamuliwa kibinafsi zaidi kutokana na kutowekwa chini ya Kamati yoyote kati ya kamati za Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti kamati yako katika hoja hii ilipendekeza kuimarishwa usimamizi wa fedha katika kazi za uwekaji wa mabango ya matangazo.

Mhe. Mwenyekiti serikali inakubaliana na pendekezo la Baraza na tayari imelitaka Baraza la Manispaa kuandaa na kutekeleza mpango bora wa usimamizi wa miradi ya Baraza ikiwemo uwekaji wa mabango ya matangazo ili kuimarisha mapato ya Baraza la Manispaa. Aidha serikali imelitaka Baraza kuhakikisha kwamba biashara ya uwekaji wa mabango ya matangazo yanafanyika kwa uwazi na kwa mujibu wa sheria wa ununuzi na uuzaji wa mali za serikali ya mwaka 2005, ikiwa ni pamoja na kutangaza zabuni.

Hoja namba 4. Mhe. Mwenyekiti hoja hii ilikuwa na vipengele viwili ambavyo ni kama ifuatavyo. Gharama zilizotumia Kampuni ya SYSCORP haziendani na gharama halisi ya kazi za ushushaji wa mabango, mbali ya kwamba Kamati hujiridhisha kwamba hakukuwa na mabango yaliyokuwa yanahitaji kushushwa kwa wakati ule.

Mbili, mkataba wa Baraza na Kampuni ya SYSCORP ulifungwa wakati wa Baraza la Manispaa lililopita limemaliza muda wake na Baraza jipya halikuzinduliwa na hivyo kushindwa kupata azimio la Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, katika hoja hii Baraza la Wawakilishi pia lilipendekeza kuimarishwa kwa usimamizi na uwekaji wa mabango ya matangazo. Mhe. Mwenyekiti serikali imeona kuwa haikuwa sahihi kwa Baraza la Manispaa kuitoza Kampuni ya SYSCORP gharama kwa kazi ya ushushaji wa mabango kwa sababu kimsingi kampuni hiyo ilipaswa ikabidhiwe eneo safi ambalo halina mabango ya matangazo. Hata hivyo kwa kuwa Kampuni ya SYSCORP walikubali kulipa gharama hizo kama sharti la kupatiwa eneo hilo, ni dhahiri kwamba yalikuwepo makubaliano ya pande mbili, na hivyo serikali inaona hili halikuwa tatizo.

Mhe. Mwenyekiti pamoja na maelezo hayo, serikali imelitaka Baraza la Manispaa kurekebisha mikataba yake na kampuni mbali mbali ili kuweka bayana kwamba kampuni yoyote itakayoweka mabango itakuwa na wajibu wa kuyashusha mara baada ya mkataba utakapomalizika, au endapo utakatishwa kwa sababu yoyote ile. Vile vile Baraza limetakiwa kufuata kikamilifu sheria ya ununuzi na uuzaji wa mali za umma namba 9 ya mwaka 2005.

Mhe. Mwenyekiti hoja namba 5. Baraza la Manispaa kujenga Bwawa la Michenzani kwa shilingi milioni 19 bila ya kuwa na bajeti ya ujenzi wa bwawa hilo.

Mhe. Mwenyekiti maoni ya Baraza la Wawakilishi kuhusu hoja hii ni kwamba Baraza la Manispaa lilipaswa kuwasilisha nyongeza ya makisio kama kanuni ya 68 ya Baraza la Manispaa inavyoeleza.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hoja hii serikali imeona kwamba matumizi yaliyofanyika ya shilingi milioni 19 kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Michenzani yalikuwa ndani ya bajeti ya mwaka ulioidhinishwa na Baraza hili. Na hivyo hapakuwa na haja ya kuombwa bajeti ya ziada (*supplementary budget)*, hata hivyo kutokana na hoja ya Kamati yako serikali imelitaka Baraza la

Manispaa kufuata sheria na kanuni zilizopo kuhusu matumizi ya fedha ikiwemo kufuata taratibu za uhaulishaji wa fedha kwa matumizi mengine ya vifungu vilivyoombewa bajeti hiyo.

Hoja namba 6. Mhe. Mwenyekiti hoja ilikuwa na vipengele 4 kama ifuatavyo:-

Moja, utaratibu wa Baraza la Manispaa kuwa ni lazima maombi ya matumizi yapitie kwa Afisa Utawala au Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ambaye naye baada ya kuyaidhinisha lazima ampe nakala Afisa Utawala. Hali hii inaonesha kwamba Afisa Utawala ndio mwenye uwezo kuliko mtu yoyote katika kuidhinisha matumizi ya Baraza la Manispaa.

Katika Baraza la Manispaa hakuna utaratibu maalumu unaotumika wakati wa kuidhinisha matumizi jambo ambalo ni kinyume na taratibu za fedha.

Kutoundwa kwa Kamati ya Kudumu ya Kuratibu na kuthibitisha masuala ya fedha ndani ya Baraza la Manispaa jambo ambalo ni matakwa ya sheria namba 3 ya 1995 imekuwa ni jambo la kawaida kwa miaka mingi, hivyo hupelekea kutumika fedha za wananchi kinyume na masharti ya sheria.

Nne; maamuzi ya matumizi ya fedha na maamuzi mengine yanayotolewa na Kamati za Kudumu za Baraza la Manispaa hayawasilishwi mbele ya Baraza zima.

Mhe. Mwenyekiti katika kuzipatia ufumbuzi hoja hizi Baraza la Wawakilishi lilipendekeza kuwa Afisa Utawala awe na hadhi sawa na Wakuu wengine wa Idara na kuwe na utaratibu maalumu unaofuatwa wakati wa kuomba na kuidhinisha matumizi ya fedha za Baraza. Aidha Kamati ilipendekeza kuwa shughuli ya Utawala na Utumishi ziendelee kuwa chini ya Mkurugenzi isipokuwa ateuliwe Afisa Maalumu wa kumsaidia

Mkurugenzi katika masuala hayo ambaye hatokuwa na mamlaka sawa au zaidi ya wakuu wa Idara waliotajwa ndani ya sheria.

Mhe. Mwenyekiti Baraza la Wawakilishi pia lilipendekeza kwa kuwa Kamati ya Kudumu ya kushughulikia zaidi masuala ya kisekta, ni vyema maamuzi yanayotolewa na kamati hizi yawasilishwe mbele ya Baraza zima, ili kutekeleza dhana ya uwajibikaji wa pamoja na utawala bora. Aidha kamati ilipendekeza kuwepo na kanuni inayokidhi matakwa ya kifungu 23 cha sheria namba 3 ya 1995 kuhusu kuundwa kwa Kamati ya Kudumu ya Kuratibu na Kudhibiti Masuala ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti serikali inakubaliana na hoja na mapendekezo yaliyotolewa na Baraza lako Tukufu na tayari imeliagiza Baraza la Manispaa kufuata matakwa ya sheria katika kutekeleza majukumu yake, ikiwemo kuundwa kwa kamati ya kudumu ya mipango na fedha ya Baraza. Aidha tayari Baraza la Manispaa limesharekebisha mapungufu yaliyokuwepo na sasa Idara zote za Baraza zina hadhi sawa, na umeandaliwa utaratibu wa kila Mkuu wa Idara kuwasilisha maombi ya Idara yake moja kwa moja kwa Mkurugenzi, na baada ya maombi hayo kuidhinishwa hupelekwa kwa Mhasibu kwa ajili ya malipo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu pendekezo la kamati ya kuteuliwa kwa Afisa Maalumu wa kumsaidia Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa katika shughuli za utawala na utumishi suala hili limezingatiwa na kuchukuliwa hatua ipasavyo.

Hoja namba 7. Hakuna utaratibu maalumu unaotumiwa na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa kuwasilisha ripoti ya fedha na ripoti ya watendaji kwa Waheshimiwa Madiwani wa Baraza hilo.

Mhe. Mwenyeikiti kuhusu hoja ya kuwepo kwa utaratibu maalumu wakati wa kuomba na kuidhinisha matumizi, serikali inakubaliana na uamuzi wa Baraza la Wawakilishi kwamba huko

nyuma haukuwepo utaratibu mzuri wa Mkurugenzi wa Manispaa kuwasilisha ripoti za fedha na ripoti za utendaji. Naomba kuchukua fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba kasoro hiyo hivi sasa haipo tena na Baraza la Manispaa linafuata utaratibu wa kuwasilisha ripoti za fedha na utendaji kwa waheshimiwa madiwani kikamilifu.

Hoja namba 8. Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati Teule kuhusu kuainisha vifungu 49(1) (c) na 51 ya sheria ya Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti upungufu ulioonekana na Baraza la Wawakilishi katika hoja hii hauzuii utendaji kazi wa Baraza la Manispaa. Hata hivyo serikali imepokea ushauri wa Baraza na ushauri huu utazingatiwa wakati wa kufanya mapitio ya sheria ya serikali za mitaa.

Hoja namba 9. Mhe. Mwenyekiti hoja hii inahusisha maeneo 3 yafuatayo:-

Watendaji wa Baraza la Manispaa wakiongozwa na Mkurugenzi kufanya manunuzi kwa kutumia watu binafsi badala ya Kampuni jambo ambalo linaleta hisia kuwa na maslahi binafsi.

Pili, takriban shughuli nyingi za manunuzi katika Baraza la Manispaa hufanywa bila ya kutolewa zabuni kinyume na ilivyoelezwa na kanuni ya 55, 56, na 57. Sharti la kutangaza zabuni pia linamfunga Mkurugenzi kwa mujibu wa kifungu cha 11(2) cha sheria namba 3 ya mwaka 1995 kinachomtaka azingatie sheria nyengine zote za nchi ambapo akiwa Afisa Muwajibikaji Mkuu wa masuala ya fedha, anapaswa kuzingatia sheria za manunuzi na uuzaji wa mali za umma namba 9 ya mwaka 2005.

Tatu, Afisa Ununuzi hashirikishwi katika kufanya ununuzi mbali mbali kwa ajili ya Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi katika hoja hii linapendekeza kuwa Baraza la Manispaa lifuate sheria ya ununuzi na uuzaji wa mali za umma na kanuni zake wakati wa kununua na kuuza mali za Baraza la Manispaa. Vile vile Baraza lilipendekeza kuwa Afisa wa Ununuzi wa Baraza la Manispaa ashirikishwe wakati wa ununuzi na asitumike kuziba mianya ya ukiukwaji wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti kuhusiana na hoja hii, serikali imelifuatilia kwa kina suala hili na kuona kwamba Baraza la Manispaa tayari limeanza kutekeleza sheria ya ununuzi na uuzaji wa mali za umma namba 9 ya 2005 kwa kuanzisha kitengo cha ununuzi (*PMU*). Hata hivyo imeonekana kuwepo na utata wa kisheria juu ya suala zima la uundwaji wa Bodi ya Zabuni kwa sababu taasisi yenye hadhi ya Shirika la Umma (*body corporate*) kama ilivyo kwa Baraza la Manispaa kutakiwa na Bodi ya Wakurugenzi ambayo ndio inayoteua wajumbe wa Bodi ya Zabuni. Kwa sasa sheria ya Baraza la Manispaa haina kifungu kinachoruhusu kuwa na Bodi ya Wakurugenzi, na Baraza la Madiwani liliopo haliwezi kuchukua nafasi hiyo kwa vile ni la wanasiasa.

Mhe. Mwenyekiti, serikali itazingatia suala hili wakati wa kuifanyia marekebisho Sheria ya Ununuzi na Uuzaji wa Mali za Umma 2005 ili Sheria hiyo itakayofanyiwa marekebisho iweze kutumiwa na serikali za mitaa katika kufanya manunuzi na kuuza mali za Baraza la Manispaa. Kwa sasa Afisi ya Mwanasheria Mkuu tayari imeshalishauri Baraza la Manispaa kuunda bodi yake ya zabuni kwa kuwatumia wakuu wa Idara kuwa ndiyo wajumbe wa bodi hiyo kama utaratibu unavyotumika kwa Idara zinazojitegemea.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la ushiriki wa Afisa Ununuzi katika masuala ya ununuzi. Naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba hivi sasa Afisa huyo anashirikishwa kikamilifu katika kufanya kazi hiyo. Aidha katika jitihada za kuimarisha kitengo

cha manunuzi cha Baraza la Manispaa (*PMU*), Baraza limepeleka masomoni wafanyakazi wake wawili ambao wanasomea Diploma ya Ununuzi na Ugavi na watakapokamilisha mafunzo yao na kurudi kazini watasaidia sana katika kuimarisha huduma za usimamizi wa ununuzi katika Baraza la Manispaa.

Hoja namba 10. Mhe. Spika, hoja hii ilikuwa na vipengele 4 kama ifuatavyo:

Wafanyabiashara ambao wametoa pesa zao kujenga vibaraza kwenye Soko la Mwanakwerekwe; hawakufahamishwa kwa uwazi utaratibu wa jenga, endesha na haulisha (BOT) ambao ndio uliotumika kujenga vibaraza hivyo.

Pili, Kamati ina wasiwasi juu thamani halisi (*value for money*) ya ujenzi wa vibaraza na meza katika soko la Mwanakwerekwe.

Tatu. Ingawa wafanyabiashara walilipa asilimia 80 ya fedha zote walizotakiwa kulipa shilingi 400000 kati ya shilingi 500000 kwa Mkandarasi, jambo la kustaajaabisha ni kwamba walitakiwa kufunga mkataba na Baraza la Manispaa badala ya Mkandarasi huyo.

Nne. Ingawa Mkurugenzi na Mkandarasi walieleza kuwa wakodishwaji wa vibaraza na meza wamelipa baada vibaraza na meza kujengwa. Kamati imebaini kuwa kauli hizo sio sahihi na badala yake kauli za wakodishwaji ndio zenye ukweli. Kamati imetamka hivyo baada ya kuangalia tarehe zilizotolewa risiti na tarehe ya kufungwa kwa mikataba.

Tano. Kutokana na kasoro mbali mbali zilizojitokeza kwenye mikataba, inadhihirisha wazi kuwa Watendaji wa Baraza la Manispaa wakiongozwa na Mkurugenzi hawapo makini wakati wa kufunga mikataba.

Sita. Baraza la Wawakilishi limeona sio kweli kwamba Mkandarasi alipeleka barua ya kuomba kupewa vibaraza kwa wale wafanyabiashara walioshindwa kulipa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mkurugenzi amemruhusu Mjenzi kujenga bila ya kufuata taratibu za kisheria, Baraza linapendekeza aliyekuwa Mkurugenzi wa Baraza Ndugu Rashid Ali Juma achukuliwe hatua za kinidhamu. Pia Baraza limependekeza Mkurugenzi huyo pamoja na Ndugu Khamis Ali Khamis mjenzi wa vibaraza wachukuliwe hatua za kisheria kwa kutoa ushahidi wa uongo mbele ya kamati iliyoundwa kwa mujibu wa kifungu cha 22 cha Sheria namba 4 ya 2007.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza limependekeza Mkurugenzi na watumishi wa Baraza waliohusika katika makosa yaliyobainika katika mikataba wachukuliwe hatua za kisheria. Aidha, Baraza limetoa ushauri kwa viongozi wa Baraza kuwa makini wakati wa kufunga mikataba ili kulinda uhalali wa mikataba hiyo.

Mhe. Mwenyekiti kuhusu suala la kumchukulia hatua za kinidhamu aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa Ndugu Rashid Ali Juma hatua hizo hazitoweza kuchukuliwa kwa vile muhusika amelazimika kujiuzulu wadhifa wake huo kutokana na uamuzi wake wa kuchukua nafasi ya uongozi katika chama cha siasa. Aidha serikali imelishauri Baraza la Wawakilishi kuwasilisha shauri linalohusu wahusika kutoa ushahidi wa uongo mbele ya Kamati kwa Jeshi la Polisi, yaani hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi ya wahusika hao.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la wafanyabiashara kufunga mkataba na Baraza la Manispaa badala ya Mkandarasi. Serikali imeamua kulifikisha suala hili Polisi kwa uchunguzi zaidi, na endapo itabainika kuna sheria zilizokiukwa, wahusika watachukuliwa hatua zinazofaa kwa mujibu wa sheria. Vile vile Baraza la Manispaa limetakiwa kuwasilisha rasimu za mikataba

yote katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kupitiwa na kushauriwa ipasavyo.

Hoja namba 11. Mhe. Mwenyekiti hoja hii ilikuwa na vipengele viwili kama ifuatavyo:-

Moja. Kutofuatwa kwa utaratibu wa kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa vibaraza katika soko la Mwanakwerekwe na kutotangazwa kwa zabuni za ujenzi huo, jambo ambalo ni kinyume na kifungu 55(b) cha Kanuni za Baraza la Manispaa pamoja na sheria ya ununuzi na uuzaji wa mali za umma ya mwaka 2005.

Mbili. Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa amehusika na mgogoro baina ya Baraza la Manispaa na Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi kutokana na kitendo chake cha kukusanya ada ya leseni kwa wafanyabiashara wa ndani wa soko la Mwanakwerekwe; jambo lililopelekea Mhe. Waziri wa Wizara husika kutoa agizo la kumtaka Mkurugenzi huyo kurejesha fedha hizo ambazo ni shilingi milioni 10. Hadi taarifa hii inakamilika fedha hizo zilikuwa hazijarejeshwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hoja hii, Baraza la Wawakilishi limependekeza kuchukuliwa kwa hatua za kinidhamu kwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa Ndugu Rashid Ali Juma kwa kitendo chake cha kuruhusu ujenzi kufanyika bila ya kupata taratibu za kisheria. Serikali imeona umuhimu wa pendekezo hilo na tayari imeliandikia Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi juu ya tuhuma mbali mbali zinazomkabili aliyekuwa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa Ndugu Rashid Ali Juma. Aidha serikali imelitaka Baraza la Manispaa kuilipa Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi fedha za leseni zilizokusanywa kutoka kwa wafanyabiashara walioko katika soko la Mwanakwerekwe ili kuondosha mzozo uliopo baina ya Baraza la Manispaa na Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi.

Aidha serikali imeelekeza kwamba wafanyabiashara wanaotumia masoko yaliyopo katika Wilaya ya Magharibi wakate leseni zao za biashara katika Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi, na Baraza la Manispaa liwatoze kodi za matumizi ya eneo tu.

Hoja namba 12. Mhe. Mwenyekiti katika hoja hii Baraza la Wawakilishi liliibua maeneo 5 yenye mapungufu kama ifuatavyo:-

Moja. Baadhi ya madiwani walijichukulia maeneo ya maduka katika Soko la Mwanakwerekwe kinyume cha utaratibu na kuwakodisha wafanyabiashara kwa maslahi yao binafsi.

Pili. Baadhi ya Madiwani hutumia Kamati za Kudumu za Baraza la Manispaa kuwa ni vitega uchumi vyao.

Tatu. Kitendo cha Madiwani kutafuta wateja wa kukodi maduka hayo kinaashiria kwamba Madiwani huchangia kwa asilimia kubwa ukiukwaji wa sheria kwa maslahi yao binafsi.

Nne. Kuna ukiukwaji mkubwa wa maadili ya kazi na utumiaji mbaya wa madaraka.

Tano. Kamati za Kudumu za Ujenzi na Mazingira za Baraza la Manispaa hutumiwa vibaya na Madiwani kama ni sehemu ya kujipatia maslahi yao.

Mhe. Mwenyekiti, katika kushughulikia suala hili Baraza la Wawakilishi limependekeza kwamba Madiwani hawa wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa makosa ya kujipatia fedha kinyume na sheria. Aidha kwa kuwa mikataba hiyo iliyowekwa imekiuka masharti ya kifungu cha 20(2) cha sheria namba 3 ya mwaka 1995, Baraza limependekeza kufungwa upya mikataba hiyo kama ilivyoelekezwa na kifungu hicho cha sheria. Vile vile Baraza la Wawakilishi limependekeza kuwa watendaji wa

Baraza la Manispaa waliohusika na ufungaji wa mikataba kinyume na sheria wachukuliwe hatua za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu pendekezo la kuwachukulia hatua za kisheria Madiwani wanaohusika na uchukuaji wa maduka na kukodisha kinyume na utaratibu, serikali haina mamlaka ya moja kwa moja kuwachukulia hatua za kinidhamu Madiwani hao. Ni vyema ikafahamika kwamba suala hili limechangiwa zaidi na kukosekana kwa sheria ya maadili ya viongozi. Hata hivyo serikali hivi sasa imo katika hatua za matayarisho ya sheria ya maadili ya viongozi ambayo itatumika kuwachukulia hatua za kisheria viongozi wanaokiuka maadili yao ya uongozi.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili vile vile litazingatiwa wakati wa utayarishaji wa sheria mpya ya serikali za mitaa. Aidha serikali imemuagiza Waziri mwenye mamlaka ya Tawala za Mikoa kukutana na Waheshimiwa Madiwani na kuwaelimisha juu ya njia sahihi za kutekeleza majukumu yao. Pia serikali itaviarifu vyama siasa na Madiwani hao kuvitaka kuzungumza na Madiwani hao juu ya haja ya kuheshimu sheria zilizopo nchini.

Mhe. Mwenyekiti kama ilivyoelezwa awali kwamba serikali imeliagiza Baraza la Manispaa kushirikiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kufanya mapitio ya mikataba yote na kasoro zozote zitakazobainika zirekebishwe kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Hoja namba 13. Baraza la Manispaa halikuwapatia risiti baadhi ya wakodishwaji baada ya kufanya malipo mbali mbali yakiwemo ya leseni. Kitendo hicho ni kinyume na kifungu namba 3 cha mkataba wa ukodishaji.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi limebaini kwamba wapo baadhi ya wafanyabiashara waliolipa fedha zao kwa ajili ya kukodishwa maduka ila hawakupatiwa risiti. Kutokana na kasoro hii Baraza limependekeza kuchukuliwa hatua kwa wale

wote waliobainika kutofuata sheria na kanuni za Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, ingawa suala hili halijawekwa wazi serikali inawataka wale wote ambao walilipa fedha zao na hawakupatiwa risiti wajitokeze ili hatua za kisheria na kinidhamu ziweze kuchukuliwa kwa wahusika.

Hoja namba 14. Mhe. Mwenyekiti, hoja hii ina vipengele viwili ambavyo ni kama ifuatavyo:-

Moja. Kitendo cha kuwatoza ada ya usafi wafanyabiashara wanaopanga biashara zao ndani na nje ya maduka ni cha dhulma. Hii ni kutokana kuwa ndani ya duka Baraza la Manispaa halitoi huduma za usafi.

Pili. Pamoja na kuwepo mikataba kwa wafanyabiashara waliokodishwa milango ya maduka, Baraza limebaini kuwa mikataba hiyo ina mapungufu kadhaa.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza katika hoja hii imelitaka Baraza la Manispaa liache kuwatoza mara mbili ada ya usafi wafanyabiashara wanaoweka biashara zao nje na ndani ya duka. Aidha Baraza la Wawakilishi limependekeza kuwa serikali ichukue hatua kwa wale wote waliobainika kutofuata sheria na kanuni za Baraza la Manispaa pamoja na sheria nyengine zinazohusiana na manunuzi. Baraza pia limependekeza Baraza la Manispaa lipitie upya mikataba yote iliyofungwa kipindi kilichopita ili ijiridhishe na utaratibu uliotumika.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hoja hii serikali tayari imeliagiza Baraza la Manispaa pamoja na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuipitia mikataba iliyoingia na Baraza la Manispaa na wafanyabishara mbali mbali na kuchukua hatua zinazofaa. Aidha serikali kupitia Wizara husika itaandaa utaratibu wa kuwahoji wakodishwaji na kuwatambua watendaji waliohusika na tatizo

hili, na ikithibitika kwamba wamefanya makosa hayo wahusika wote watachukuliwa hatua za kisheria. Nachukua fursa hii pia kueleza kwamba serikali inawashauri wafanyabiashara wanaohisi wamedhulumiwa kwa kutozwa ada za usafi bila ya kupata huduma hiyo, wafuate taratibu za kisheria kwa kuyapeleka malalamiko yao mahkamani kwani Baraza lina hadhi ya Shirika linaweza kushtaki na kushtakiwa.

Hoja namba 15. Kipengele cha 3 cha mkataba kimemtaka Mkodishwaji kulipia ada ya huduma ya usafi wa Shilingi 90,000 kwa mwezi wakati hali halisi analipia shilingi 40,000.

Mhe. Mwenyekiti, katika hoja hii Baraza la Wawakilishi linapendekeza kwamba watendaji wa Baraza waliohusika na suala hili wachukuliwe hatua za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imebaini kwamba mkataba wa Baraza la Manispaa una vifungu viwili tofauti; ambapo kimoja kinahusiana na ukodishwaji wa mlango na chengine kinahusu usafi. Hivyo serikali haikuridhika na maelezo yaliyotolewa na Baraza la Manispaa na inaendelea kulifanyia kazi suala hili ili kupata ukweli wake. Serikali itawachukulia hatua za kinidhamu na kisheria wale wote waliobainika kuwa na makosa katika hoja hii.

Hoja namba 16. Mhe. Mwenyekiti, hoja hii ilikuwa na vipengele vinne ambavyo ni:-

Moja. Rashid Khalfan Ali ameshindwa kulipa asilimia 20 ya kodi ya milango miwili kwa kipindi chote alichokodishwa na Baraza la Manispaa. Kwa upande mwengine Baraza la Manispaa limeshindwa kulipa gharama za ujenzi kwa mlango mmoja hadi sasa.

Pili, bwana Suleiman Msellem Nassor ameshindwa kulipa asilimia 20 ya kodi ya milango miwili kwa kipindi chote

alichokodishwa na Baraza la Manispaa. Kwa upande mwengine Baraza la Manispaa limeshindwa kulipa gharama za ujenzi wa milango minne.

Tatu. Wajenzi hawakulipwa gharama za fedha ambazo wamezitumia katika ujenzi.

Nne. Wajenzi wametumia gharama kubwa zaidi ya walichokubaliana na Baraza la Manispaa kinyume na makubaliano kutokana na maelekezo mabaya ya mshauri wa ujenzi wa Baraza la Manispaa Ndugu Abdulkadir.

Mhe. Mwenyekiti, katika hoja hii Baraza la Wawakilishi linapendekeza kuwa watendaji wa Baraza la Manispaa wachukuliwe hatua za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti kutokana na hoja hii, serikali imebaini kwamba Baraza la Manispaa limeshindwa kulipa gharama za maduka tisa na hivyo kuwashauri wajenzi wa maduka hayo Ndugu Rashid Khalfan Ali na Ndugu Suleiman Msellem Nassor kuyapeleka mashauri yao mahkamani kulishtaki Baraza la Manispaa, vyenginevyo Baraza hilo lifikirie kuwalipa wajenzi hao fedha wanazodai.

Mhe. Mwenyekiti hoja namba 17 ina vipengele kama ifuatavyo:-

Moja. Baraza la Manispaa limefunga mkataba wa ujenzi wa watu mbali mbali ambao ni Kampuni ya F&K Enterprises Limited ndugu Rashid Khalfan Ali na Ndugu Suleiman Msellem Nassor pamoja na waliokodishwa maduka. Hivyo Baraza lilishindwa kujua mjenzi halisi wa maduka hayo.

Pili. Kampuni ya F&K imesajiliwa kisheria isipokuwa kwa mujibu wa kipengele cha 3(a) na (r) cha *memorundum of association,* Kampuni hii haina jukumu la kufanya shughuli za usafi pamoja na shughuli za ujenzi.

Tatu. Baraza la Manispaa kutokuwa na mikataba ya kimaandishi na Bwana Suleiman Msellem Nassor kuhusu ujenzi wa maduka yote kumi.

Nne. Wakodishwaji wamejazishwa mikataba kama wao ni wajenzi wa maduka hayo na wanalipa asilimia sawa na waliojenga.

Tano. Baraza la Manispaa limeshindwa kutimiza ahadi ya kuwapatia milango wafanyabishara waliokuwa wanatumia eneo hilo maarufu wauza ndizi.

Sita. Ujenzi wa maduka haya umekosesha baadhi ya wananchi ajira, jambo ambalo limepelekea hali zao za maisha kuwa ngumu.

Mhe. Mwenyekiti, serikali katika kulifuatilia suala hili imeona kuna utata mkubwa katika suala zima la ujenzi wa maduka katika eneo la Darajani kama ilivyobainishwa na Baraza la Wawakilishi. Miongozi mwa ambayo yameleta utata ni kutowepo kwa mikataba halali baina ya Baraza la Manispaa na *F&K Enterprises Limited* serikali imeagiza Wizara husika ichukue hatua za kisheria dhidi ya Ndugu Ramadhan Abdalla Songa kwa kukodisha maduka na kuchukua fedha za wafanyabiashara wakati akijua fika kuwa sio yeye aliyejenga maduka hayo.

Kwa mujibu wa sheria namba 4 ya 2007, serikali inalishauri Baraza la Wawakilishi kuwasilisha Polisi na kwa Mkurugenzi wa Mashtaka suala la kumchukulia hatua za kisheria Ndugu Vuai Ame Vuai kwa kutoa maelezo yanayotofautiana mbele ya Kamati kwa lengo la kuipotosha Kamati. Kama ilivyoelezwa hapo awali serikali pia imeona haja ya kuchukuliwa hatua za kisheria kwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa Ndugu Rashid Ali Juma kutokana na sababu za kukiuka sheria ya ununuzi na

uuzaji wa mali za umma pamoja na kanuni zake. Aidha serikali itazingatia ushauri uliotolewa na Baraza la Wawakilishi juu ya kuwawezesha walioathirika hii itafanyika baada ya kujua idadi kamili na mahitaji ya waathirika hao. Baraza la Manispaa tayari limeagizwa kuanza kulifanyia kazi suala hili.

Hoja namba 19, 20, 21. Baraza la Manispaa halikuingia Mkataba na Kampuni ya F&K Enterprises Limited kuhusu ujenzi wa maduka 13 katika soko la Darajani na shughuli za ujenzi wa maduka 13 katika soko la Darajani ilifanywa bila ya kutangazwa zabuni jambo ambalo ni kinyume na Kanuni ya 55(b) ya Kanuni za Baraza la Manispaa na Sheria ya Ununuzi na Uuzaji wa Mali za Umma nambari 9 ya 2005.

Aidha, wakodishwaji wengine ambao si wajenzi mbali ya Ndugu Rashid na Ndugu Suleiman wamejazishwa mikataba sawa na wengine ya kujilipia asilimia 80 na kulilipa Baraza asilimia 20 wakati wao sio wajenzi.

Mhe. Mwenyekiti, katika hoja hizi serikali imeona upo utata mkubwa katika ujenzi wa maduka ya Soko la Darajani na tayari serikali imeanza kuchukua hatua kwa kuwasilisha suala hili katika Jeshi la Polisi dhidi ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa Ndugu Rashid Ali Juma kwa uchunguzi zaidi, na iwapo itathibitika kwamba Mkurugenzi huyo alifanya makosa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Hoja nambari 22: Ugawaji wa maduka na kufidia wajenzi haukuzingatia idadi ya ujenzi wa maduka, wajenzi wote wamepewa maduka mawili jambo ambalo ni kinyume na makubaliano yao. Mjenzi aliyejenga maduka matatu amepewa mawili na aliyejenga maduka kumi kapewa mawili.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inakubaliana na hoja ya Baraza la Wawakilishi na kuona kuwa hakukuwa na utaratibu mzuri katika

ugawaji maduka ya kufidia wajenzi wa maduka hayo. Baraza la Manispaa limetakiwa kuwa makini katika kufuata sheria na kanuni za utendaji wa shughuli zake.

Hoja nambari 23: Mhe. Mwenyekiti, hoja hii inahusisha vipengele vinane kama ifuatavyo:

i) Baraza la Manispaa kutotangaza zabuni ya ujenzi wa maduka 16 katika Soko la Mbogamboga Darajani.

ii) Mkurugenzi wa Manispaa alishindwa kutekeleza matakwa ya kifungu 29(2) cha Sheria Nambari 3 ya mwaka 1995 kinachomtaka aendeleze mikataba halali aliyoirithi.

iii) Maeneo yaliyokuwa na masoko kujengwa majengo ya kudumu (maduka) jambo ambalo huondosha dhamira ya kuwa na masoko.

iv) Baadhi ya vipengele vya mikataba havikujazwa.

v) Kipengele cha 14(c) cha mkataba kinachoeleza kwamba, mkodishwaji mjenzi akodishe maduka kwa watu wengine kwa makubaliano na mkodishaji wa Manispaa haikufuatwa. Hii ni kutokana na kuwa mkodishwaji amewakodisha watu bila ya kutoa taarifa kwa mkodishaji.

vi) Shughuli za ujenzi zimetolewa bila ya kufuata taratibu za zabuni jambo ambalo ni kinyume na kanuni ya 55(b) ya Baraza la Manispaa pamoja na Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Umma.

vii) Ujenzi wa maduka haya umewakosesha ajira wananchi na baadhi yao kubaki kutangatanga mitaani na

wengine kujibana kwa wenzao na kupelekea kushuka kwa shughuli za biashara.

viii) Baraza lilishindwa kutimiza ahadi iliyoitoa kwa wafanyabiashara waliokuwa wakitumia eneo lile.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na hoja hii, Baraza la Wawakilishi limependekeza kuwa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa achukuliwe hatua za kinidhamu kwa kutofuata sheria za nchi na amelitaka Baraza la Manispaa kulipa gharama alizotumia Ndugu Ussi Ame Pandu wa S.L.P 318 kwa mujibu wa thamani ya soko. Sambamba na hilo Baraza la Manispaa limlipe fidia Ndugu Ussi Ame kwa usumbufu alioupata.

Mhe. Mwenyekiti, tayari nimeshatoa maelezo juu ya serikali kwa suala hili, kimsingi serikali inakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na Baraza la Wawakilishi ikiwa ni pamoja na kulitaka Baraza la Manispaa kufuata Sheria ya Ununuzi na Uuzaji wa Mali za Umma katika masuala yote ya manunuzi hata kama inatumia utaratibu wa *BoT*. Aidha, serikali haioni haja ya kulipwa kwa Ndugu Ussi Ame Pandu kwa sababu taratibu za kisheria hazikufuatwa katika kufikia makubaliano.

Hoja nambari 24: Mhe. Mwenyekiti, hoja hii ina vipengele vinne kama ifuatavyo:

i) Mkodishwaji wa Bustani ya Jamhuri (Bi Asya Moh'd Bafadhil) anatumia gharama kubwa kinyume na anavyotarajiwa kwa kuwa kipato kinachopatikana ni kidogo.

ii) Kuna utata kuhusu tarehe ya kuanza kwa maduka kwa ukodishwaji wa Bustani ya Jamhuri ambapo risiti zinaonesha kwamba wameanza kulipa tokea tarehe 1 Aprili, 2010 wakati mkataba umeanza tarehe 1 Novemba, 2010.

iii) Shughuli za ujenzi katika Bustani ya Jamhuri imetolewa bila ya kufuata taratibu za zabuni jambo ambalo ni kinyume na kanuni ya 55(b) ya Baraza la Manispaa pamoja na Sheria ya Ununuzi na Uuzaji wa Mali za Umma.

iv) Kitendo cha Mkurugenzi kutamka kuwa mali za serikali hazikodishwi zaidi ya miaka kumi ni kinyume na kifungu cha 47 cha Sheria ya Ardhi Nambari 12 ya mwaka 1992 kama ilivyorekebishwa na kifungu cha 6 cha Sheria nambari 11 ya mwaka 2010. Hii ni kutokana na kuwa kifungu hicho kinaruhusu mali ya serikali ukodishwaji si zaidi ya miaka 99.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi katika hoja hii limependekeza kwamba watendaji wa Baraza la Manispaa wakiongozwa na Mkurugenzi wafuate sheria na kanuni mbali mbali za nchi pamoja na kumtaka Mkurugenzi huyo awe muangalifu na kauli zake anazozitoa. Aidha, kwa kuwa mkodishwaji alishindwa kutoa maelezo ya kina mbele ya Kamati ya Baraza kuhusiana na malipo yaliyofanywa tarehe 1 Aprili, 2010 Kamati ya Baraza inashauri kuwa mkataba huo uanze mwezi huo. Vile vile Kamati ya Baraza imependekeza kuwa Baraza la Manispaa kuwa makini wakati linapoingia na kufunga mikataba ili kuleta tija.

Mhe. Mwenyekiti, katika hoja hii serikali imeona kwamba, ingawa kwa mujibu wa Baraza la Wawakilishi mkodishwaji anatumia gharama kubwa na kipato anachokipata ni kidogo bado anasisitiza kuendelea na mkataba huo. Hii inaonesha wazi kwamba mkodishwaji huyo anapata faida, vyenginevyo asingesisitiza kuendelea na mkataba huo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mtazamo huo, serikali inakubaliana na pendekezo la Baraza la Wawakilishi kwamba Baraza la Manispaa kutakiwa kufuata sheria na kanuni na

imelitaka Baraza kufanya hivyo. Aidha, serikali inamtanabahisha Mkurugenzi aliyepo hivi sasa kuwa makini na kuzingatia ipasavyo sheria na kanuni zake, na kwamba wakati wote Baraza liwe makini na hasa wakati wa kuingia na kufunga mikataba ili kuweka tija kwa Baraza la Manispaa.

Kuhusu hoja ya mkodishwaji kutoa malipo kabla ya kuanza kwa mkataba, serikali haikuwa na tatizo kwa jambo hilo kwani mkataba uliotiwa saini ndio msingi mkuu unaopaswa kuheshimiwa.

Hoja nambari 25: Baraza limeona kwamba ukodishwaji wa Bustani ya Jamhuri hauna tija kwa Baraza la Manispaa. Baraza lako tukufu linapendekeza kwamba Baraza la Manispaa liwe makini wakati linapoingia na kufunga mikataba ili kuleta tija.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inakubaliana na hoja hii ya Baraza na imeona ni kweli mkataba wa ukodishwaji wa Bustani ya Jamhuri hauna maslahi kwa Baraza. Mkataba huo ni miongoni mwa mikataba itakayoangaliwa upya kwa msaada wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, Baraza la Manispaa kwa mara nyengine tena limetakiwa kuwa makini wakati linapoingia na kufunga mikataba.

Hoja nambari 26: Mhe. Mwenyekiti, katika hoja hii Baraza limebainisha kasoro sita kama ifuatavyo:-

1. Kampuni binafsi mbalimbali zilizopewa kazi na Baraza la Manispaa lakini bado mafundi wa Baraza hutumika kwenye kazi hizo walizopewa kampuni binafsi kinyume na utaratibu.
2. Shughuli za ujenzi katika maeneo mengine aliyojenga Ndugu Ali Abdalla Ali zimetolewa bila ya kufuatwa utaratibu wa zabuni kwa vile kazi zenye gharama zinahitaji hivyo.

3. Mjenzi alipewa fedha za kununulia miti kinyume na taratibu za manunuzi.
4. Baraza limenunua vifaa kama vile *"bollard", "paving stone"* kwa mtu binafsi wakati lina uwezo wa kutengeneza vifaa hivyo. Pia vifaa vinavyonunuliwa havina ubora ukilinganisha na vile vilivyotengenezwa na Baraza siku za nyuma.
5. Ingawa ziko barua tatu tofauti zinazoonesha ndugu Ali Abdalla Ali kulipa gharama alizotumia kwa awamu. Hata hivyo, Baraza limebaini kuwa kwa mujibu wa barua hizo malipo yaliyofanywa ndani ya mwezi mmoja kutokana na tarehe za barua hizo jambo ambalo liliitia mashaka Kamati ya Baraza. Sambamba na hilo hundi nambari 990385 inaonesha kwamba malipo hayo yalifanywa kwa pamoja. Kutokana na mashaka hayo, Kamati ya Baraza ilimtaka aeleze ukweli wa jambo hilo ambapo Ndugu Ali Abdalla alikiri kwamba alilipwa fedha zile kwa pamoja kimakosa, na katika kutatua hilo alitakiwa na Baraza kuandika barua zile.
6. Hakuna mkataba baina ya Baraza la Manispaa na Ndugu Ali Abdalla Ali wa ujenzi katika eneo la Darajani.

Mhe. Mwenyekiti, katika hoja hii Baraza la Wawakilishi limependekeza kuwa Baraza la Manispaa liache tabia ya kukwepa masharti ya sheria na kanuni zilizopo na lifuate matakwa ya sheria na kanuni hizo. Aidha, Kamati ya Baraza imependekeza kuwa wafanyakazi wa Baraza la Manispaa wasishirikishwe au wasitumike kwenye kazi walizopewa kampuni hata kama kazi hiyo inatakiwa haraka (kampuni iachiwe itafute mbinu za kumaliza kazi zake kwa wakati). Vile vile Baraza la Wawakilishi lilishauri Baraza la Manispaa kukabidhi kazi kwa wataalamu wake ili kuepuka kutumika vibaya fedha za walipa kodi wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi serikali inakubaliana na hoja na mapendekezo yaliyotolewa na Baraza la Wawakilishi na tayari

serikali imelitaka Baraza la Manispaa kuacha tabia ya kukwepa na kufuata masharti ya sheria na kanuni. Vile vile serikali imelitaka Baraza la Manispaa kutowashirikisha wafanyakazi wake katika kazi ilizopewa kampuni kwa namna yoyote ile. Baraza la Manispaa pia limeagizwa kutumia wataalamu wake wa fani mbali mbali kufanya kazi za Baraza ili kupunguza kutumika fedha za kulipa wataalamu wa nje kwa kazi zinazoweza kufanywa na wataalamu wa ndani ya Baraza la Manispaa.

Hoja nambari 27: Ndugu Ali Abdalla Ali alikuwa mfanyakazi wa Baraza la Manispaa wakati huo alipewa majukumu na kazi binafsi za Baraza la Manispaa kupitia kampuni yake.

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyokuwa kwa hoja nambari 26 Baraza la Wawakilishi imelishauri Baraza kukabidhi kazi kwa wataalamu wake hao ili kuepuka kutumika vibaya fedha za walipa kodi wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imeshangazwa sana na uamuzi wa Baraza la Manispaa kumpa mtu kazi ambaye Baraza hilo hilo limemfukuza kazi. Hivyo serikali inakubaliana na hoja ya Baraza la Wawakilishi na kukubali pendekezo lake. Baraza la Manispaa tayari limetakiwa kuachana kabisa na tabia ya kutumia wataalamu wa nje kwa kazi ambazo zinaweza kufanywa na wataalamu wake wa ndani katika Baraza la Manispaa.

Hoja nambari 28: Mhe. Mwenyekiti, katika hoja hii Baraza la Wawakilishi limeibua mambo makubwa matatu ambayo yameonekana kuwa ni kasoro katika utendaji wa Baraza la Manispaa ambayo ni kama ifuatavyo:

i) Baraza la Manispaa limenunua basi kwa ajili ya wafanyakazi kwa njia ya ununuzi wa moja kwa moja kwa kutumia kifungu cha 38(1) cha sheria ya Nambari 5 ya mwaka 2005 na haikutangazwa zabuni. Kamati ya Baraza haikubaliani na uamuzi

wa Mkurugenzi kutumia kifungu hicho kwani ununuzi wa gari haukuhitaji uharaka huo.

ii) Baraza kwa makusudi limekiuka kifungu 55 cha Kanuni za Baraza ambayo inamtaka Mkurugenzi kutoa tangazo la kuitisha zabuni katika ununuzi wa basi hilo.

iii) Kauli ya Ndugu Abdalla muuzaji wa basi aliyoitoa mbele ya Kamati ya Baraza ya kuwa aliuza gari mbili kwa Baraza kwa maombi tofauti katika miezi tofauti inapingana na barua ya tarehe 12 Mei, 2010 iliyotumwa na Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi katika hoja hii limependekeza kuwa watendaji wa Baraza la Manispaa wakiongozwa na Mkurugenzi wafuate matakwa ya sheria kikamilifu na sio kuyafumbia macho baadhi ya masharti kwa maslahi yao binafsi. Vile vile Baraza limependekeza kuwa maamuzi yote ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Manispaa yawasilishwe kwenye Baraza kwa kuidhinishwa, jambo hili litasaidia kila Diwani kujua kinachoendelea kwenye Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inakubaliana na hoja zilizotolewa na Baraza la Wawakilishi, kitendo cha baadhi ya wafanyakazi wa Baraza kukwepa kufuata sheria na kanuni zinazoongoza Baraza hakikubaliki na hivyo serikali imeshalifikisha suala hili katika Jeshi la Polisi kwa uchunguzi na hatua za kisheria dhidi ya wahusika wote. Aidha, serikali imelitaka Baraza la Manispaa kuwasilisha maamuzi yote ya Kamati za Kudumu za Mabaraza kwenye Baraza kwa kuidhinishwa. Hatua hii itasaidia kila Diwani kujua kinachoendelea kwenye Baraza la Manispaa.

Hoja nambari 29: Mhe. Mwenyekiti, hoja hii ina vipengele saba kama ifuatavyo:

i) Sheria na kanuni za uajiri na upandishaji wa vyeo katika Baraza la Manispaa hazifuatwi kwa baadhi ya watendaji.
ii) Ingawa uajiri wa wafanyakazi 83 uliofanywa kinyume na utaratibu lakini uajiri huo ulikuwa sahihi.
iii) Kwa kuzingatia dokezo la tarehe 30 Septemba, 2009 inadhihirisha wazi kwamba Ndugu Khamis ameteuliwa na Mkurugenzi Rashid kushika wadhifa huo kwa kuwa yeye ndiye aliyetia saini dokezo hilo.
iv) Utaratibu wa upandishwaji wa vyeo katika Baraza la Manispaa hauzingatii sifa kwa nafasi husika bali hufanywa kwa upendeleo.
v) Mkurugenzi anatumia madaraka aliyokuwanayo kwa maslahi yake binafsi.
vi) Watumishi wa Baraza la Manispaa hawapewi *Job Description* kitu ambacho ni kinyume na taratibu za kazi.
vii) Mkuu wa Idara ya Utawala na Sheria anafanya shughuli zaidi za Afisa Utumishi.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi limetoa mapendekezo mbalimbali katika kusaidia kurekebisha kasoro zilizoonekana katika Baraza la Manispaa. Miongoni mwa mapendekezo hayo ni kuwajibishwa na kuchukuliwa hatua aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa Ndungu Rashid Ali Juma kwa mujibu wa sheria za nchi. Serikali kuagiza wizara husika na masuala ya utumishi kuupitia upya muundo wa utumishi wa Baraza la Manispaa kwa lengo la kuweka utaratibu maalumu wa upandishaji vyeo pamoja na kuangaliwa kwa sifa za watumishi na watendaji waliopandishwa vyeo bila ya kuwa na sifa husika waondolewe mara moja na kuwekwa wale wanaostahiki. Aidha, pendekezo jengine ni kwamba watendaji wa Baraza watakiwe kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa taaluma na maadili yao ya kazi na kuachana na tabia za kufuata amri za Mkurugenzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Kamati imekiri kuwa uajiri uliofanyika ulikuwa sahihi, na kwa kuwa kipindi kilichofanyika

ajira hizo sheria ya Utumishi wa Umma ilikuwa bado haijaanza, hivyo serikali imeona ni busara kumchukulia hatua Mkurugenzi. Hata hivyo, Baraza la Manispaa limetakiwa kufuata sheria na kanuni za nchi kikamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria nambari 4 ya mwaka 2007 Baraza la Wawakilishi iliwasilishe Polisi na kwa Mkurugenzi wa Mashtaka suala la kumchukulia hatua aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa kwa kutoa taarifa za uongo mbele ya Kamati ya Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hoja ya baadhi ya watendaji wa Baraza la Manispaa kupandishwa vyeo bila ya kuwa na sifa, serikali imeona kasoro iliyoibuliwa na Baraza la Wawakilishi ingawa watendaji hawa watatu wana sifa za kielimu lakini imegundulika kwamba uzoefu wao ni mdogo. Hivyo katika kuliletea ufanisi Baraza la Manispaa serikali imeamua kuwaondoa wafanyakazi hao katika nyadhifa zao hizo na nafasi zao kupewa wafanyakazi wengine wenye sifa za kielimu na uzoefu wa kutosha katika kazi.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inakubaliana na pendelezo la Baraza la Wawakilishi la kuwataka watendaji wa Baraza la Manispaa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa taaluma na maadili yao ya kazi. Hata hivyo, watendaji hao ni lazima kufuata amri halali za Mkurugenzi wa Manispaa aliyeko sasa.

Hoja nambari 31: Mhe. Mwenyekiti, katika hoja hii Baraza la Wawakilishi limeainisha kasoro katika maeneo matano ambayo ni kama ifuatavyo:

i) Maamuzi ya Waziri kuliandikia barua Baraza la Manispaa ya kusitisha zoezi la kumhamisha mkodishwaji wa duka la *Diplomatic Supermarket* ni kinyume na masharti ya kifungu cha 62 cha sheria Nambari 3 ya 1995. Hii ni kutokana na kuwa kifungu hiki kinamtaka

kwanza Waziri afanye uchunguzi wa jambo husika na endapo atagundua kuwa Baraza la Manispaa linatekeleza majukumu yake kinyume na utaratibu, basi atoe taarifa kupitia Gazeti Rasmi la Serikali na hatua nyengine ziendelee. Kwa msingi huo kitendo cha Waziri kumuongezea muda mkodishwaji hakina uhalali.

ii) Baraza lina wasiwasi juu ya baadhi wa viongozi wakiwemo Mhe. Waziri na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa kupokea fedha kwa ajili ya kutoa maamuzi ya upendeleo.

iii) Baraza na Kamati ya Fedha na Uchumi zilizopitisha azimio la kujengwa kwa kuimarishwa eneo la Mazizini liliopo duka la *Diplomatic*.

iv) Hakuna tangazo lolote lililotolewa kuhusiana na uimarishaji wa eneo la *Diplomatic Supermarket*.

v) Kumbukumbu za Vikao vya Baraza zinaonesha kuwa kumbukumbu zimeandikwa mwanzo na vikao ndio vikafuata. Kwa mfano, kikao nambari 1/2012 kilifanyika tarehe 6 Machi, 2012 wakati kumbukumbu zimeandikwa tarehe 12 Machi, 2011. Aidha, kikao nambari 3/2012 kilifanyika tarehe 6 Juni, 2012 wakati kumbukumbu zimeandikwa tarehe 11 Juni, 2011.

Mhe. Mwenyekiti, katika hoja hizi Baraza lilitoa mapendekezo yake kama ifuatavyo:

1. Waziri kabla ya kuchukua hatua azingatie zaidi matakwa ya sheria mbali mbali kuliko utashi ili kuepuka mvutano usio wa lazima.
2. Serikali kwa kupitia Makamu wa Pili wa Rais ichunguze tuhuma zilizotolewa dhidi ya viongozi hawa na endapo itathibitika hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wote waliohusika.
3. Baraza la Manispaa kuitisha zabuni kwa ajili ya ujenzi wa eneo hilo.

4. Kwa kuwa kuna mgongano wa tarehe katika kumbukumbu za vikao, Baraza linawashauri watendaji wa Baraza wawe makini wakati wa kuandaa kumbukumbu mbali mbali za vikao.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inakubaliana na pendekezo la kamati la kumtaka Waziri kuzingatia matakwa ya sheria kabla ya kuchukua hatua. Aidha serikali imechunguza tuhuma kwamba Waziri na Mkurugenzi wamepatiwa fedha kwa ajili ya kutoa maamuzi ya upendeleo na haikupata ushahidi wowote juu ya tuhuma hizi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hoja hii serikali imelitaka Baraza la Manispaa kumalizana na mkodishwaji wa duka hilo kwa kukubaliana na kuendelea na mkataba naye kwa masharti mapya au kusitisha mkataba huo. Aidha, serikali imelitaka Baraza la Manispaa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuona utaratibu gani wa kumaliza mkataba mkodishwaji huyo ili kutoa fursa kwa Baraza la Manispaa kuliendeleza eneo hilo. Vile vile serikali imelitaka Baraza la Manispaa kuwa makini katika uandaaji na uwekaji wa kumbukumbu za vikao ili kusitokee utata juu ya taarifa za kumbukumbu hizo.

Hoja nambari 32: Maeneo ya Masoko kujengwa majengo ya maduka na kudhoofisha dhamira ya kuwa na masoko. Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hoja hii Baraza la Wawakilishi limependekeza kuwa Baraza la Manispaa liachane na tabia ya kujenga maduka ya kudumu katika masoko, na badala yake libakie na dhana ya kuwa na masoko.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri uliotolewa na Baraza la Wawakilishi ni wa busara na wa kimsingi. Serikali inakubaliana na mapendekezo yao. Hata hivyo, mtazamo wa Baraza la Manispaa wa kuchanganya maduka na soko ni wa kisasa zaidi na unatumika katika nchi mbali mbali duniani. Serikali imelitaka Baraza la Manispaa kuweka dhamira ya kuchanganya maduka na

soko tangu inapoandaliwa michoro na sio kuongeza mambo ambayo mwanzo hayakuwepo.

HITIMISHO:

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo na ufafanuzi huo wa serikali naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kutoa maelezo haya. Vile vile niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati Teule wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mhe. Salmin Awadh Salmin kwa kazi yao nzuri yenye mustakbali mwema wa nchi yetu. Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutekeleza majukumu yao kupitia kamati zao mbali mbali. Nawashukuru pia viongozi na watendaji wa Baraza la Manispaa kwa kusaidia kutoa maelezo yaliyoweza kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imeshaanza kazi ya kuyafanyia kazi mapendekezo mbali mbali yaliyotolewa na Baraza lako tukufu, ni imani yangu kuwa kila taasisi inayohusika na utekelezaji wa mapendekezo hayo itafanya kazi zake kwa umakini na uadilifu mkubwa kwa lengo la kuwezesha Baraza letu la Manispaa kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe naomba sana niwashukuru kwa uvumilivu na usikivu wenu wa hotuba hii. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, tangu asubuhi leo tulikuwa tunajadili taarifa moja nzito sana, kiasi ambacho kwa kweli mpaka ilipopita wengine vichwa vinauma sana, sio kwa upande wetu sisi *backbenchers* tu, lakini hata kwa Waheshimiwa Mawaziri. Ukiangalia ufafanuzi walioutoa wanahitaji wapate

mapumziko kidogo kusudi waweze kupata muda wa kuweza kusikiliza tena na kutafakari jinsi ya michango itakayotoka kwa Waheshimiwa.

Kwa mnasaba huo Mhe. Mwenyekiti, ili umakini na umahiri katika kuchangia hii hoja naomba kwamba tuakhirishe kikao hichi hadi kesho saa tatu asubuhi ili tuweze kuja kuchangia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe ni kweli hoja yako ina mantiki na inastahiki kufanyika kwa mujibu wa maombi ambayo umeyatoa na ukitilia maanani katika meza yangu hapa nina mchangiaji mmoja tu, ambaye tayari alikwishaleta jina lake mbele kwa ajili ya kuchangia. Nilikuwa namuona kwamba bado anaendelea na harakati za kujikamilisha zaidi ili aweze kuendelea kuchangia hoja hizo. Na kwa kuwa muda wetu bado tuna dakika 45 mpaka 75 za ziada, na kwa mambo ambayo yaliletwa na Mhe. Mjumbe tumuombe basi Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili tuweze kuweka kanuni kando na tutimize maoni hayo ya Mjumbe mwenzetu ambayo ameyatoa hapa ili tuweze kwenda kujipongeza na kujitayarisha kwa kazi nzito na pevu hapo kesho asubuhi pamoja na kufunga Baraza letu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru wewe lakini nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi wangu Mhe. Saleh Nassor kwa namna ambavyo yuko makini na anafuatilia afya za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Ni kweli Mhe. Mwenyekiti, kwa leo Wajumbe wamefanya kazi kubwa na nzuri na ya kupongezwa. Kwa msingi huo tungeliakhirisha Baraza lako mpaka kesho asubuhi ili tuweze kuendelea na shughuli mapema za kuwahudumia wananchi wetu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji basi wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaakhirisha Baraza hili kwanza nina tangazo hapa.

Waheshimiwa wote wa Baraza la Wawakilishi pamoja na watendaji mnaalikwa katika sherehe za Kombe la Ligi ya Mabenki zitakazofanyika kesho Jumanne tarehe 22/10/2013 baada ya kuakhirishwa kwa kikao cha asubuhi. Pahala patakuwa ni *cafeteria* inaonekana ni huko nyuma. Nyote mnakaribishwa.

Baada ya maelezo hayo sasa nichukue fursa hii kukushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa namna ambavyo tulishirikiana pamoja tukafanya kazi nzito na hatimaye tukaweza kufikia hapa leo, na nachukua fursa hii kuakhirisha Baraza hili hadi kesho siku ya Jumanne tarehe 22/10/2013 saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 12:55 jioni Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 22/10/2013 saa 3:00 asubuhi)